ADRIAN EBENS



# KUJIHATARISHA KWA MUNGU

UHURU WA KWELI KATIKA UPENDO WA BABA

# KUJIHATARISHA KWA MUNGU

Uhuru wa kweli katika upendo wa Baba



ADRIAN EBENS

FATHER
OF LOVE
fatheroflove.info

Adrian Ebens, 2021

Copyright © 2021, Adrian Ebens

Haki ya kimaadili ya mwandishi imethibitishwa.

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kuzalishwa tena kwa faida ya kibiashara, ikijumuisha kusambazwa kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodi au vinginevyo, bila kibali cha maandishi cha awali cha mchapishaji na wenye hakimiliki. Tafadhali kumbuka kuwa mwandishi amekoleza wino katika sehemu za aya ili kusisitiza jambo fulani lililokusanywa kutoka kwenye maandiko hayo.

Nukuu za Maandiko zimetolewa katika Biblia ya New King James Version, isipokuwa pale paliponyeshwa vinginevyo.

Copyright© 1982 na Thomas Nelson, Inc. Imetumiwa kwa ruhusa.

Nukuu za Maandiko zinazohusishwa na NLT zimetoka katika Biblia Takatifu, New Living Translation, New Living Translation copyright© 1996, 2004, 2007, 2013 na Tyndale House Foundation. Imetumiwa kwa ruhusa ya Tyndale House Publishers Inc.

Nukuu za Maandiko zinazohusishwa na NIV zimetoka katika Biblia Takatifu, New International Version, copyright©1973, 1978, 1984, 2011 na Biblica, Inc.® Imetumiwa kwa ruhusa.

Nukuu za Maandiko zinazohusishwa na NIRV zimetoka katika Biblia Takatifu, New International Reader’s Version®, copyright © 1995, 1996, 1998 na Biblica. Haki zote zimehifadhiwa.

Viunganishi vyote vya tovuti na maudhui yaliyonukuliwa ni ya kisasa kuanzia Desemba 2020

Namba zilizonukuliwa katika mabano ya mraba [ ] ni marejeleo ya mfumo wa namba wa Strong’s Concordance.

Kitabu hiki na machapisho mengine yote ya Father of Love yanapatikana kutoka katika tovuti yetu fatheroflove.info, ili kuagiza nakala za ziada tafadhali tuma barua pepe kwa adrian@life-matters.org

ISBN: 978-0-6488114-6-6

Kitabu hiki kimeandikwa na Adrian Ebens
Kimethibitishwa na Lorelle Ebens
Picha ya Jalada na iStockphoto
Aina 10.5/15 Palatino

Kimechapishwa Nchini Australia

# KUJIHATARISHA KWA MUNGU

Uhuru wa kweli katika upendo wa Baba

ADRIAN EBENS

# YALIYOMO


Sura ya 1: Utata Wa Kujua Yote Na Kuweza Yote.......................................5
Sura ya 2: Kujua Mwisho Tangu Mwanzo................................................11
Sura ya 3: Mwitikio Wa Kimungu Kwa Matendo Ya Binadamu ............19
Sura ya 4: Kristo Aliye Ukweli Wa Baba..................................................28
Sura ya 5: Mtoto Aliyefunzwa Au Fundi Stadi .......................................37
Sura ya 6: Kutokufa, Sheria Ya Maadili Na Uhuru Wa Kuchagua .........45
Sura ya 7: Nafasi Ya Maombi.....................................................................53
Sura ya 8: Huru Kweli Kweli ......................................................................61
Sura ya 9: Ngome Ya Lusifa ........................................................................65
Sura ya 10: Kanuni Ya Mbegu.....................................................................72
Sura ya 11: Mfumo Wa Muundo Wa Kimungu Na Upinzani Wake .....81
Sura ya 12: Kupatana Kwa Haki Na Rehema............................................85
Sura ya 13: Utawala Wa Mauti ..................................................................92
Sura ya 14: Anguko La Lusifa Na Malaika Zake ....................................101
Sura ya 15: Joka Aanzisha Makazi Yake Duniani ...................................106
Sura ya 16: Unabii Wa Juma La Uumbaji.................................................114
Sura ya 17: Kuumbwa Kwa Mfano Wa Mungu .......................................130
Sura ya 18: Utawala Katika Bustani Ya Edeni .........................................137
Sura ya 19: Paradiso Iliyopotea ...............................................................143
Sura ya 20: Nia Ya Mwili ..........................................................................155
Sura ya 21: Kujihatarisha Kwa Upendo Wa Agape................................160
Sura ya 22: Udhaifu Wa Mungu...............................................................167
Sura ya 23: Kumjeruhi Baba .....................................................................172
Sura ya 24: Tokeni Gizani .........................................................................176

SURA YA 1

# UTATA WA KUJUA YOTE NA KUWEZA YOTE

Biblia inatuambia katika mstari wake wa kwanza kabisa kwamba "hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi," Mwanzo 1:1. Swali moja ambalo watu wengi hujiuliza ni kwamba, "Je, Mungu alijua kwamba Adamu na Hawa wangetenda dhambi?"

Ukristo kwa haraka sana hujibu ndiyo kwa swali hili. Hapa kuna mifano michache.

> Mungu anajua yote (Zaburi 139:1–6), na Anajua yajayo (Isaya 46:10). Kwa hiyo alijua kwa hakika kwamba Adamu na Hawa wangetenda dhambi.[1]
>
> Ikiwa Mungu Alijua Kwamba Adamu na Hawa Wangetenda Dhambi, Basi, Kwa Nini Aliwaumba? Bwana hakushangazwa na dhambi ya Adamu na Hawa, kwa maana ilitimiza kusudi la mpango wa Bwana katika kumleta Yesu afe badala ya wenye dhambi na kufufuka ili kutoa uzima wa milele.[2]

---

[1] https://www.gotquestions.org/if-God-knew-Adam-Eve-sin.html

[2] https://www.christianity.com/wiki/bible/if-god-knew-that-adam-and-eve-would-sin-then-why-did-he-create-them.html

Swali hili linavutia zaidi tunapoanzisha wazo la adhabu. Ikiwa Mungu alijua kabla ya kuwaumba Adamu na Hawa kwamba wangetenda dhambi, basi kwa nini aliwaadhibu? Je, hii ni haki? Sikiliza jibu moja la Kikristo.

> Je, ni kufuru kufikiria kwamba Mungu alijua Adamu na Hawa wangetenda dhambi…kwa sababu Yeye ni Mungu na bado akawaadhibu?
>
> Hili ni swali zuri. Jibu fupi ni hapana, si kufuru kufikiri kwamba Mungu alijua kwamba Adamu na Hawa wangetenda dhambi. Ndiyo, alijua wangetenda dhambi na kwamba angewaadhibu. Hakika, Maandiko yanaweka wazi kwamba Mungu alijua wangetenda dhambi.
>
> Waefeso 1:3-4 "Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo."
>
> Kama kifungu hiki kinavyoweka wazi, Mungu alichagua wale ambao wangemwamini Mwana wake na kuokolewa (mstari 4). Kwa kuwa alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hiyo ina maana kwamba Mungu alijua kwamba tungekuwa wenye dhambi na kwamba Mungu angehitaji kumtuma Mwanawe ili kutoa wokovu. Hii ina maana alijua kwamba Adamu na Hawa wangetenda dhambi, kwa kuwa sisi ni wenye dhambi kwa sababu ya kosa la Adamu.[3]

Mnamo 2018 na 2019, ndege mbili za 737 Max katika matukio mawili tofauti zilianguka ghafla na kuua jumla ya watu 346. Katika uchunguzi huo iligundulika kulikuwa na hitilafu ya muundo katika ndege hiyo. Iligunduliwa pia kuwa Boeing ilificha dosari za muundo kutoka kwa

[3] https://www.versebyverseministry.org/bible-answers/is-it-blasphemous-to-think-god-knew-that-adam-and-eve-would-sin

marubani na wadhibiti.[4] Nani achukuliwe kuhusika na ajali za ndege hizi? Marubani au wabunifu wa ndege hiyo?

Ikiwa Mungu ndiye aliyekuwa mbunifu na Muumbaji wa jamii ya wanadamu na Alijua kwa hakika kwamba mfumo aliouumba ungeanguka na kusababisha vifo vya mabilioni ya watu, basi ni nani anayepaswa kuwajibika? Ni mwanadamu au Mungu? Ikiwa Mungu alijua mambo haya hata kabla ya kuumba jamii ya wanadamu, basi kwa nini Yeye, ikiwa anajua yote, asifanye mpango huo ili usishindwe?

Ukristo unaongeza tatizo hili zaidi kupitia fundisho lingine. Mungu anasemwa kuwa ni muweza wa yote. Ikiwa Mungu aliumba mfumo akijua kwamba utaanguka na alikuwa na uwezo wa kuzuia ajali hizo zisitokee, basi kwa nini hakuzuia wanadamu kuanguka? Je, hili ni swala la haki?

Mwanafalsafa Mgiriki Epicurus aliyeishi karibu miaka 300 kabla ya Kristo alifikia hitimisho lifuatalo kulingana na kile alichoelewa kumhusu Mungu wakati huo.

> "Je! Mungu yuko tayari kuzuia maovu, lakini hana uwezo huo? Basi kama ni hivyo si muweza wa yote. Je, ana uwezo huo, lakini hataki? Basi ni mbaya sana. Je, anaweza na yuko tayari? Basi ubaya hutoka wapi? Hana uwezo wala hataki? Kwa nini basi kumwita Mungu?" - Epicurus.

Mawazo yake yamepata mvuto mwingi zaidi ya miaka 100 iliyopita, pamoja na sauti zingine zinazopingana katika kujibu madai ya imani ya Kikristo. Madai ya kujua yote na kuweza yote yanapaswa kuhamasisha watu kujiamini kwamba Mungu ndiye anayetawala na kwamba tunaweza kumwamini kwa sababu anajua kabisa kile kinachoendelea.

Bado inaonekana kwamba kwa watu wengi, mafundisho hayo mawili ya kujua yote na uweza wa yote yamekuwa pembe mbili ambazo Ukristo umejishika. Ikiwa unajua kwa hakika kwamba hatua

---

[4] https://www.business-standard.com/article/international/boeing-hid-design-flaws-in-737-max-from-pilots-regulators-us-panel-120091602119_1.html

unazochukua kuunda kitu kitasababisha taabu na kifo cha mabilioni ya watu, basi inawezekanaje kutohusisha jukumu la mateso haya kwa muumba huyo?

Yesu mwenyewe alisema:

> Ndipo Yesu akawaambia, "Nawauliza ninyi, Je! Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya; kuponya roho au kuangamiza?" Luka 6:9

Yesu analinganisha mema na kuokoa maisha na mabaya na kuangamiza maisha. Ikiwa Mungu alijua kwamba kwa kuumba ulimwengu kwamba bila shaka kungesababisha kifo cha mabilioni, basi si kwa ufafanuzi wa Yesu - uovu? Kitabu cha Yakobo kinatuambia:

> Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi. Yakobo 4:17

Je, watu wanaamini kwamba ni vyema kwa mabilioni ya watu kuteseka na kufa? Je, kuna yeyote anayeamini hili? Ikiwa ni vyema kuokoa uhai na Mungu alijua kwamba kwa kuumba ulimwengu huu kwamba kungeangamiza uhai, basi kwa ufafanuzi huu huu Mungu ni mwovu.

Wakristo wengi hukasirika unapouliza swali lolote katika mwelekeo huu. Ni mashambulizi dhidi ya dhana zao za uungu, na kwa haraka sana unaweza kuambiwa kwamba ni kufuru kuwaza hivi na kwamba utapelekwa kuzimu usipotubu. Aina hii ya mawazo imesababisha majibu kama haya.

> "Dini ni imani ya kiimla, ni hamu ya kuwa mtumwa. Ni hamu ya kuwa na mamlaka isiyobadilika, isiyopingika, dhalimu ambayo inaweza kukusadikisha uhalifu wa mawazo ukiwa umelala, ambayo inaweza kukuweka chini ya uangalizi wa karibu kila saa kila uamkapo na usinziapo katika kila dakika ya maisha yako, kabla ya kuzaliwa na, mbaya zaidi na ambapo furaha ya kweli huanza, baada ya kufa..... Nani anataka hili liwe kweli? Ni nani isipokuwa mtumwa anayetamani Hatma ya kutisha hivi? Nimewahi kufika Korea Kaskazini. Ina mtu mbaya sana kama raisi wake, Kim Jong-Il ni mkuu wa chama na mkuu wa jeshi. Si

> mkuu wa nchi. Nafasi hiyo ni ya Baba yake aliyefariki, Kim Il-Sung. Ni necrocracy, thanatocracy. Kwa kifupi ni kama utatu ninaweza kuongeza. Mwana ni kuzaliwa upya kwa baba. Ni dhuluma mbaya na ya wazi na isiyo na moyo ambayo jamii ya binadamu imewahi kujihusisha nayo. Lakini angalau unaweza #$%ing kufa na kuondoka Korea Kaskazini!"– Christopher Hitchens.[5]

Je, Christopher Hitchens alikuwa na hoja au alikuwa mtu asiyeamini kuwa kuna Mungu? Je, yawezekana kwamba baadhi ya imani za kimsingi za Ukristo zilichangia kumwona Mungu na serikali Yake kwa njia hii?

Kuamini kwamba Mungu anajua kabisa kila kitu ndani yake kuna kidonge kichungu ambacho waumini wote wanapaswa kukimeza. Inamaanisha lazima ukubali kwamba Mungu alijua vifo na uharibifu huu wote ungetokea, lakini bila hata kujali aliendelea na kufanya hivyo. Hii inachangiwa na ukweli kwamba ikiwa unatilia shaka juu ya kwamba Mungu anajua kila kitu, basi una hatari ya kukataa uungu Wake na kwa hivyo unaweza kutupwa motoni. Kwa hiyo, si rahisi kwa Wakristo kujibu swali hili kwa njia ya wazi. Wakristo wengi wamefungiwa katika kanuni za imani zinazohitaji uamini kwamba Mungu anajua kila kitu na kuhoji juu ya jambo hili ni kuhatarisha uzima wako wa milele.

Sio jumuiya zote za Kikristo huendesha mambo hivi lakini nyingi hufanya hivyo - katika jumuiya nyingi za Kikristo, kuhoji misingi kamili ya mambo kama haya kutakufanya utengwe, ufukuzwe, au uuwawe (kama si na wafuasi wenyewe, basi na Mungu). Misingi hii ni pamoja na imani kwamba Mungu anajua kila kitu. Je, hii si sawa na Korea Kaskazini?

Mungu anatangaza kuwa Yeye ni upendo (1 Yohana 4:8), na kwamba hakuna hofu katika upendo (1 Yohana 4:18). Anataka tumwabudu kwa moyo wetu wote, kwa nguvu zetu zote, kwa roho zetu zote, na kwa akili zetu zote; na kutangaza hii kuwa amri kuu (Luka 10:27). Ikiwa ndivyo hivyo, basi ni wajibu wetu kushughulikia na kujibu swali hili, kwa ajili yetu wenyewe na kwa ajili ya wengine, kwa kuwa hatuwezi

[5] https://en.wikipedia.org/wiki/Christopher_Hitchens

kumpenda Mungu kwa moyo wote, kwa “akili zetu zote”, na ukosoaji wa kina wa Muumba wetu ukiendelea katika fahamu zetu....

Hebu tugeukie Maandiko ili tuone ni nini hasa kilichoandikwa.

SURA YA 2

# KUJUA MWISHO TANGU MWANZO

Biblia hutoa taarifa kadhaa kuhusu maarifa juu ya Mungu. Katika uelewa wa kawaida tunayo kauli ya thamani kama hii.

> Ee BWANA, umenichunguza na kunijua. Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea mbali. Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu, Umeelewa na njia zangu zote. Maana hamna neno ulimini mwangu Usilolijua kabisa, BWANA. Umenizingira nyuma na mbele, Ukaniwekea mkono wako. Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, Hayadirikiki, siwezi kuyafikia. Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko. Zaburi 139:1-8

Baba yetu wa mbinguni anajua kila kitu kutuhusu. Anajua mawazo yetu na mambo tutakayosema. Anajua tulipo kila wakati kwa njia ya Roho wake. Kwa wale wanaojua kwamba Mungu ni mwenye upendo, fadhili na rehema, hili ni wazo la faraja sana.

> "Je! Mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi." Luka 12:6-7

Baba yetu anajua idadi kamili ya nywele za vichwa vyetu. Hili pia hutujuza kwamba Yeye anajua mengi zaidi yatuhusuyo kuliko tunavyojijua sisi wenyewe.

> Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema,' Maana sisi sote tu wazao wake.' Matendo ya Mitume 17:24-28

Baba yetu ni mkuu sana. Huwapa uhai na pumzi kila kiumbe chenye uhai wafikao mabilioni kwa sasa. Yeye hufuatilia kila seli ya kila kiumbe hai, na huangalia mwingiliano wao na kila mmoja. Ni kwa jinsi gani mtu mmoja anaweza kuunganishwa kwa karibu sana na mabilioni mengi ya viumbe hai kwa wakati mmoja, hakika hili liko nje ya ufahamu wetu.

Zaidi ya hayo, inasemwa kwamba Mungu anajua mipaka na nyakati za kila taifa linalokuja juu ya dunia kabla halijatokea. Hili pia haliwezekani kwa mwanadamu kulifahamu. Ukweli wa maneno haya unaweza kupatikana katika Biblia katika sehemu kama vile kitabu cha Danieli ambapo kuinuka kwa mataifa kutoka wakati wake kunafunuliwa muda mrefu hadi wakati ujao. Wakati wakiishi katika ufalme wa Babeli, ilifunuliwa kwa Danieli kuhusu kuinuka kwa falme za Umedi-Uajemi na Uyunani ambazo zingekuja baada ya wakati huo.

> Yule kondoo mume uliyemwona, mwenye pembe mbili, hizo ndizo wafalme wa Umedi na Uajemi. Na yule beberu, mwenye manyoya mengi, ni mfalme wa Uyunani; na ile pembe kubwa iliyo kati ya macho yake ni mfalme wa kwanza. Danieli 8:20-21

Kitabu cha Danieli kiliandikwa katika karne ya 6 kabla ya Kristo. Kwa sababu ya usahihi wa utabiri wa Danieli, watu wengi wamehitimisha kwamba kitabu hiki hakingeweza kuandikwa wakati huo, na tarehe yake baada ya kuinuka kwa ufalme wa Uyunani. Ugunduzi wa magombo ya Bahari ya Chumvi (Dead sea scrolls) ulionyesha kwamba kitabu cha Danieli tayari kilikuwepo katika kanuni za kinabii za Kiebrania mwaka wa 150 KK, kumaanisha karne nyingi zimepita tangu kilipoandikwa. Kwa sisi tunaoamini kuwa Biblia ni neno la Mungu, tunaona ufunuo wa ajabu wa ujuzi wa Baba yetu wa mbinguni na uwezo wa kuona wakati ujao na kujua kitakachotokea.

Katika kushughulika Kwake na jamii ya wanadamu, Mungu amefichua uwezo Wake wa kueleza wakati ujao kama alama bainishi inayoonyesha Yeye ni Mungu.

> Hubirini, toeni habari; naam, na wafanye mashauri pamoja; ni nani aliyeonyesha haya tangu zamani za kale? Ni nani aliyeyahubiri hapo zamani? Si mimi, BWANA? Wala hapana Mungu zaidi ya mimi; Mungu mwenye haki, mwokozi; hapana mwingine zaidi ya mimi. Isaya 45:21

Tukisoma katika Zaburi tunapata unabii kadhaa wa kushangaza kuhusiana na Masihi. Katika Zaburi 22 tunaambiwa juu ya kusulubishwa na maneno yale yale ambayo yangesemwa katika jaribu la Kristo.

> Lakini mimi ni mdudu wala si mtu, nadharauliwa na watu wote. Wote wanaoniona wananidhihaki; wanarusha matusi, wakitikisa vichwa vyao. “Anamtumaini BWANA,” wasema, “BWANA na amwokoe; na amwokoe, kwa kuwa anampendeza.” Lakini ulinitoa tumboni; umenifanya nikutumaini wewe, hata katika matiti ya mama yangu. Tangu kuzaliwa nilitupwa juu yako; tangu tumboni mwa mama yangu umekuwa Mungu wangu. Usiwe mbali nami, kwa maana taabu iko karibu na hakuna wa kusaidia. Fahali wengi wananizunguka; mafahali wenye nguvu wa Bashani wamenizunguka. Simba wanaonguruma wanaorarua mawindo yao wamefungua vinywa vyao dhidi yangu. Namiminwa kama maji, na mifupa yangu yote imekatika. Moyo wangu umegeuka kuwa nta; imeyeyuka ndani yangu. Kinywa changu kimekauka kama kigae, na ulimi wangu umeshikamana na paa la kinywa

> changu; unanilaza katika mavumbi ya mauti. Mbwa wananizunguka, kundi la wabaya linanizunguka; wananichoma mikono na miguu. Mifupa yangu yote iko onyesho; watu wananitazama na kunishangaa. Wanagawana nguo zangu kati yao na kupiga kura kwa ajili ya vazi langu. Lakini wewe, BWANA, usiwe mbali nami. Wewe ni nguvu zangu; njoo haraka unisaidie. Zaburi 22:6-19 (NIV)

Huu ni unabii wa kushangaza ulioandikwa miaka 1000 kabla ya wakati wa Kristo. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba mambo mengi yaliandikwa kumhusu katika Zaburi na manabii wengine wa Agano la Kale.

> Akawaambia, Haya ndiyo niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi: Ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Luka 24:44 (NIV)

Unabii katika Zaburi 22 unajumuisha hata maneno yale yale ambayo yangesemwa na wale waliomdhihaki na kumuua Yesu: "Anamtumaini BWANA, BWANA na amwokoe. Hakuna shaka kwa kusoma Biblia kwamba Mungu ana uelewa wa ajabu. Imeelezwa hivi katika Zaburi.

> "Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, Akili zake hazina mpaka." Zaburi 147:5

Usemi wa Kiebrania wa neno la Kiingereza usio na mipaka ni "*Does not exist as a number*." Kwa maneno mengine, hakuna namba inayoweza kupima maarifa ya Mungu. Kulingana na mtazamo wetu hii ina maana bila kikomo, au kama wafasiri walivyoeleza, isiyo na kikomo. Kifungu kingine kinachonukuliwa kwa kawaida kinachotumiwa kueleza kile ambacho Mungu anakijua kinapatikana katika Isaya.

> kumbukeni mambo ya zamani za kale; maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote. Isaya 46:9-10

Mungu ana uwezo wa kutabiri ni wapi kitu kitaelekea mara tu kinapokuwa kimeanza. Kinachovutia kuhusu aya hii ni kwamba inadokeza kwamba Mungu anatabiri matukio yajayo kutokana na matukio ya awali ambayo yametukia ambapo katika hili andiko hukiita mwanzo. Zaidi ya hayo, neno lililotafsiriwa nyakati za kale linaonekana kwa mara ya kwanza katika Mwanzo 2 na 3.

> BWANA Mungu akapanda bustani upande wa mashariki [H6924] katika Edeni, na humo akamweka huyo mtu aliyemfanya. Mwanzo 2:8

> Basi akamfukuza mtu huyo; akaweka makerubi upande wa mashariki [H6924] wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima. Mwanzo 3:24

Mungu anaambia taifa la Israeli kukumbuka mambo ya zamani za kale na njia ambazo amewasaidia. Kisha anarejea neno hilo la Kiebrania linaloweza kurejea mambo ya kale lakini pia lina rejeo la mwelekeo wa kijiografia, yaani, mashariki. Kwa hivyo, katika mstari huu angalau, uwezo wa kutabiri wa Mungu unaunganishwa na matukio na hata jiografia.

Katika marejeo haya ya mashariki, je, kuna jambo ambalo Mungu anataka tuelewe? Je, inaweza kumaanisha kwamba Mungu alijua hasa mahali ambapo matukio yangeelekea mara tu dhambi ya kwanza ilipotukia katika bustani ya kale, kwa kuwa hapo ndipo mbegu ya matendo yote ya wakati ujao ya mwanadamu ilipopandwa? Ikiwa Mungu anasema kwamba alijua mwisho kuanzia wakati huu wa kuanzia, kwenye bustani iliyokuwa "mashariki mwa Edeni," je, ilimaanisha kwamba Hakujua kabla ya hapo, ni mwisho gani ambao Adamu na Hawa wangechagua?

Tutarudi kwenye swali hili mara kadhaa kupitia nyanja tofauti za mawazo. Ni hatua muhimu. Je, Mungu kujua mwisho tangu mwanzo kunamaanisha tu kwamba Anajua kila kitu kabisa, au ina maana kwamba mara tu kitu kikishapandwa au kuanzishwa au kuchaguliwa, Anajua hasa kitaishia wapi?

Tumechunguza maandiko machache ambayo wanafunzi wa Biblia wametoa kuhusiana na maarifa ya Mungu. Mkristo mmoja, akiandika

juu ya somo la maarifa ya Mungu, alimalizia yafuatayo kutokana na jinsi alivyojifunza Maandiko.

> Biblia inafundisha kwamba Mungu anajua yote (omniscient). Neno "omniscient" linatokana na maneno mawili ya Kilatini omnis yanayomaanisha yote, na scientia inayoashiria maarifa. Tunaposema kwamba Mungu ni omniscient (anajua yote) wa kila kitu ina maana kwamba ana uelewa kamili wa mambo yote. Sio lazima ajifunze chochote na hajasahau chochote. Si lazima Mungu atafakari mambo, achunguze mambo, au ajifunze hatua kwa hatua. Anajua kila kitu kilichotokea na kila kitu kitakachotokea. Mungu pia anajua kila jambo la muhimu linaloweza kutokea. Mungu hata anajua mambo ambayo wanadamu bado hawajagundua. Ujuzi huu ni kamili na haupatikani. Uelewa wa Mwenyezi Mungu unamaanisha kuwa ana ujuzi kamili, ufahamu kamili, na hekima kamilifu kuhusu jinsi ya kutumia ujuzi huo.[6]

Ni hitimisho la kuvutia kutoka kwenye Maandiko. Ikiwa Mungu anajua kila kitu kitakachotokea na kamwe hahitaji kutafakari mambo, basi mwingiliano Wake na wanadamu hauwezi kamwe kujikita katika mwitikio wa mahusiano hayo. Yote yatakuwa ni mambo yaliyokwisha kupangwa. Huu ndio msimamo wa wale wanaofuata mafundisho ya John Calvin. Mapenzi makuu ya Mungu yamekishapanga mambo yote. Tayari amekwishapanga wale ambao wataokolewa na wale ambao watapotea. Maamuzi unayofanya kwa namna yoyote ile hayabadilishi chochote kile ambacho Mungu alikuwa amekusudia.

> Kuamua mambo Kabla (Predestination), katika theolojia ya Kikristo, ni fundisho la kwamba matukio yote yamekusudiwa na Mungu, kwa kawaida kwa kurejelea hatima ya mtu binafsi. Ufafanuzi wa kuamuliwa mapema mara nyingi hutafuta kushughulikia "kitendawili cha hiari", ambapo ujuzi wa Mungu wa kujua yote unaonekana kutopatana na hiari ya mwanadamu. Katika matumizi haya, kuamuliwa kwa mambo kabla kunaweza

[6] https://www.blueletterbible.org/faq/don_stewart/don_stewart_359.cfm

> kuzingatiwa kama aina ya uamuzi wa kidini; na kwa kawaida uamuzi wa awali, unaojulikana pia kama uamuzi wa kitheolojia.[7]

Tutashughulikia somo la kitendawili cha uhuru wa kuchagua na Enzi Kuu ya Mungu katika sura inayofuata. Lengo letu hapa ni kutambulisha kwa urahisi upeo wa masuala ambayo yanahusiana na somo la Mungu kuwa na maarifa kamili. Acheni sasa utangulizi wa baadhi ya maandiko ya Biblia yanayojulikana sana ambayo huenda yakapinga wazo la mapenzi ya Mungu kupanga matukio yote yajayo.

> "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee**, ili kila mtu amwaminiye asipotee**, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16

Mafungu maarufu zaidi katika Biblia yanaonyesha kwamba mwitikio wa mwanadamu ndio huamua ikiwa mtu ataokolewa au atapotea. Ikiwa Mungu tayari alijua hili basi andiko hili linapaswa kusomeka hivi, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliwapenda wale aliowakusudia tangu awali hata akamtoa Mwanawe pekee ili wale aliowachagua wawe na uzima wa milele.

Aya kama hii inafanya mambo yawe magumu zaidi:

> "Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba." 2 Petro 3:9

Hapa tunaambiwa kwamba Mungu hapendi yeyote apotee. Hii ina maana kwamba mapenzi ya Mungu ni kwamba wote waokolewe. Lakini tunajua kwamba si kila mtu ataokolewa.

> "Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache." Mathayo 7:14

Hii ina maana kwamba mapenzi ya Mungu ya kwamba wote waokolewe, yanaweza kukwamishwa na mapenzi ya kibinadamu ambayo yanakataa kuitikia zawadi ya upendo wa Mungu ya wokovu. Je, hili linaweza kuelezea kina cha machozi ambayo Yesu aliyamwaga juu ya Yerusalemu?

---

[7] https://en.wikipedia.org/wiki/Predestination

> "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." (Mathayo 23:37-38).

Hili linatupeleka katika somo la maarifa ya Mungu kuhusiana na hisia za Mungu. Nimekuwa na uzoefu mwingi ambapo nilifikiwa na rafiki yangu akiwa na habari fulani maalum ambazo mtu mwingine alikuwa amenijulisha. Kwa vile tayari nilikuwa nafahamu habari hizo, sikuweza kutoa jibu la mwitikio wa kwanza – athari ya habari hiyo ilififia kwa sababu haikuwa ngeni kwangu. Hili linatoa kidokezo kwa ukweli kwamba uwezo wa kufahamu jambo kabla huathiri mwitikio wa kihisia.

Acheni sasa tuchunguze Biblia ili tuone visa kadhaa vinavyoweza kutufanya tutilie shaka mambo fulani kuhusu uwezo wa Mungu wa kujua mambo kabla.

SURA YA 3

# MWITIKIO WA KIMUNGU KWA MATENDO YA BINADAMU

Baada ya anguko la Adamu, jamii ya wanadamu ilizama polepole katika upotovu. Wakati wa Nuhu hali ilikuwa mbaya zaidi.

> "BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote. **BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani**, akahuzunika moyo. BWANA akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; **kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya."** Mwanzo 6:5-7

Je, kweli Mungu alijuta kwamba alimuumba mwanadamu? Je, hii ilikuwa hisia halisi ambayo Mungu alikuwa akihisi? Je, ni kwa jinsi gani kwa kusikitika Alimfanya mwanadamu alingane na kanuni yake ya kupanga matukio kabla? Neno la Kiebrania linalozungumzia kusikitika lina maana ya kuugua. Linamanisha tumaini lililokatishwa tamaa.

Inavutia kusoma maelezo ya John Wesley kuhusu kisa cha Nuhu:

> Kwamba alikuwa amemfanya kiumbe mwenye mamlaka hayo matukufu, na kumweka katika dunia hii, ambayo aliijenga na kuitengeneza kwa makusudi ili iwe makao ya starehe kwake; na ilimhuzunisha moyoni mwake. **Haya ni matamshi ya namna ya wanadamu, na ni lazima yaeleweke ili kutotafakari juu ya kutobadilika au uchangamfu wa Mungu**. Haisemi shauku au wasiwasi wowote ndani ya Mungu, hakuna kitu kinachoweza kuleta usumbufu kwenye akili ya umilele; bali hunena juu ya kutoridhishwa kwake kutakatifu na haki dhidi ya dhambi na wenye dhambi; kwa maana kwake hakuna kubadilika; lakini huzungumza mabadiliko ya njia yake. - John Wesley on Genesis 6:6

Je, Wesley anapendekeza kwamba kile kilichoandikwa katika Maandiko hakiwezi kuchukuliwa kuwa kinatumika kwa Mungu? Sababu kuu ya hili ni imani ya Wesley katika kutobadilika kwa Mungu. Mafundisho haya yanapendekeza kwamba Mungu hana mhemuko au hisia, kwani hili lingependekeza kubadilika kwa Mungu. Badala ya kusoma andiko hili kama Baba aliyevunjika moyo anayewalilia watoto wake linakuwa kielelezo cha kutoridhishwa kwake kutakatifu dhidi ya dhambi na wenye dhambi. Je, hii ni kweli?

Je, inawezekana kuona huzuni hapa katika kisa cha Nuhu kama tunavyoona Yesu akilia juu ya Yerusalemu? Baba alikuwa amefanya yote aliyoweza kuwaokoa wanadamu lakini wanadamu walifanya uamuzi wa kumkataa Mungu.

> Je! utaishika njia ya zamani, ambayo watu waovu waliikanyaga, waliokatwa kabla ya wakati wao, ambao misingi yao ilichukuliwa na gharika? Wakamwambia Mungu, Ondoka kwetu! Mwenyezi atawafanyia nini? Lakini alizijaza nyumba zao vitu vizuri; lakini shauri la waovu liko mbali nami. Ayubu 22:15-18

Karibu ulimwengu wote ulikuwa umemwambia Mungu aondoke kwao. Aliachwa bila kuwa na la kufanya ila kuheshimu matakwa yao na kuwaacha wavune walichokipanda duniani.

Imani katika uwezo wa kujua yote wa Mungu ingetuambia kwamba Mungu alijua hasa kile ambacho kingetokea. Kupata huzuni kwa kumfanya mwanadamu kunaleta changamoto katika msingi wa kuamini kuwa matokeo ya matukio yote yalipangwa na Mungu.

Italeta ahueni ikiwa tutachukulia kifungu cha Biblia jinsi kinavyosomeka. Tena, tunakumbushwa kwamba Mungu hakuwa tayari hata mmoja wao apotee bali wote wafikie toba.

Tukirejea mwanzoni mwa sura hii, tutagundua kichochezi ambacho huanzisha kipindi cha muda na hatima yake mahususi. Wana wa Mungu (wana waaminifu wa Sethi) walianza kuoa binti za wanadamu (binti wakaidi wa Kaini). Kutokana na matendo ya wanadamu, Mungu alitabiri kile ambacho kingetokea.

> "Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, **wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua**. BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; **basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini**." Mwanzo 6:1-3

Maneno matatu ya Kiebrania ya 'waliwaona' , 'wazuri', na 'wakajitwalia' ni sawa kabisa na maneno yaliyotumiwa kuelezea Hawa kuchukua tunda kutoka kwenye Mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Mungu angeweza kutambua jambo hili lilikuwa linaelekea wapi. Alijua kilichokuwa moyoni mwa mwanadamu na kwa hiyo alijua kwamba katika miaka 120 dhambi zilizokusanywa za wanadamu zingesababisha maafa. Kwa nini Biblia hutoa ratiba ya wakati ili kukabiliana na matendo ya wanaume kuoa wanawake waliojikita kwenye ibada ya sanamu?

Kuna mambo mengi ya kuzingatia katika kisa hiki , lakini kipengele cha msingi tunachotaka kukizingatia ni jinsi gani tunavyoichukulia lugha ya majuto na hisia za kina zinazoelezewa ndani ya Mungu? Je, tunalinganishaje hili na wazo kwamba Mungu tayari anajua kila kitu na bado zaidi, kama wengine wanavyodokeza, hahitaji kamwe kufikiria na kupima mambo? Fikiria kisa kingine:

> "Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. **Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni**, akasema, **Ibrahimu! Ibrahimu!** Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; **kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha**

> **Mungu,** iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.” Mwanzo 22:10-12

Anayezungumza na Ibrahimu ni Malaika wa Bwana. Kurudiwa kwa jina la Abrahamu mara mbili kunaonyesha jinsi Yesu alivyozungumza mara nyingi alipozungumza na watu. “Simoni, Simoni…” (Luka 22:31); “Martha, Martha ...” (Luka 10:41). Malaika wa Bwana si mwingine ila Mwana wa Mungu na anazungumza kama mwakilishi wa Baba yake. Je, inawezekana kuyachukulia maneno haya waziwazi kwamba mpaka wakati huu ndipo Mungu alijua kwamba Ibrahimu alimcha Mungu? Mtoa maoni John Gill anatoa mawazo haya:

> **......Lakini hili linasemwa kwa jinsi ya wanadamu,** ambao hujua uhakika wa mambo yanapotokea, na kuonekana wazi na dhahiri; au hili linaweza kueleweka kama uelewa wa kuidhinishwa, ambapo Bwana sasa alijua, na kuidhinisha imani, hofu, upendo, na utiifu wa Ibrahimu, ambao ulikuwa wazi sana katika jambo hili. - John Gill Commentary on Genesis 22:12

na tena, kutoka kwa John Wesley:

> Sasa najua ya kuwa wewe unamcha Mungu - **Mungu alijua kabla, lakini sasa Ibrahimu alikuwa ametoa ushahidi wa kukumbukwa juu yake.** Hahitaji kufanya zaidi, alichokuwa amefanya kilitosha kuthibitisha heshima ya kidini aliyokuwa nayo kwa Mungu na mamlaka yake. Ushahidi bora kabisa wa kumcha Mungu wetu ni kuwa tayari kumheshimu kwa kile ambacho ni kipenzi chetu zaidi, na kuwa tayari kuachana na vyote kwa ajili yake. - John Wesley Commentary on Genesis 22:12

Tunaona mgongano kati ya usemi huu wa Maandiko na kile kinachochukuliwa kwamba Mungu anajua yote. Ikiwa Mungu tayari alijua basi isingekuwa bora kusema “Sasa umefunua ukweli ambao niliujua tangu mwanzo kwamba unamcha Mungu?” Kuna mvutano kati ya aya halisi za Biblia na msingi kwamba mambo yote Mungu anayajua. Mfafanuzi wa Biblia anafafanua hili kwa kuonyesha kwamba huu ni usemi wa wanadamu, kumaanisha kwamba Mungu hasemi ukweli juu ya kile afikiriacho. Hivyo husemekana kwamba Mungu hutualika na kusema nasi kama mwanadamu. Lakini kwa nini

Afanye hivi? Hebu tuchunguze kisa kingine tunapotafakari mambo haya.

> "Neno la BWANA likamjia Yona mara ya pili, kusema, Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa; ukaihubiri habari nitakayokuamuru. Basi Yona akaondoka, akaenda Ninawi, kama Bwana alivyonena. Basi Ninawi ulikuwa mji mkubwa mno, ukubwa wake mwendo wa siku tatu. Yona akaanza kuuingia mji mwendo wa siku moja, akapaza sauti yake, akasema, Baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa." Yona 3:1-4

Yona anaagizwa aende na kuliambia jiji la Ninawi kwamba lingepinduliwa baada ya siku 40. Hakuna ujumbe mwingine unaotolewa. Hakuna kutajwa kwa masharti ya tukio hili kutofanyika. Mji wa Ninawi ulitubu dhambi zao na kutumainia rehema ya Mungu.

> "Mungu akaona matendo yao, ya kuwa wameiacha njia yao mbaya. Basi Mungu akalighairi neno lile baya, ambalo alisema atawatenda; asilitende." Yona 3:10

Inaonekana kwamba Mungu huguswa na matendo ya jiji hilo. Walitubu na hivyo Mungu akaghairi. Ikiwa tunasema kwamba Mungu alijua kwamba hatafanya hivyo, basi lugha ya Mungu kwa Yona kwamba "Nitauangamiza mji wako" haikuwa kweli. Isingekuwa kusema ukweli. Kwa hiyo, nini kinachoendelea hapa?

Kinachovutia kuhusu amri ya awali ya Mungu ya kuupindua mji ni kwamba neno la Kiebrania la kupinduliwa katika Yona 3:4 linaweza kuwa na maana ifuatayo:

[H2015] 1b) (Niphal)

> 1b1) kujigeuza, kugeuka, kurudi nyuma
> 1b2) kujibadilisha
> 1b3) kuwa potovu
> 1b4) kugeuzwa, kubadilishwa, kugeuzwa dhidi ya
> 1b5) kubadilishwa
> 1b6) kupinduliwa, kutupwa
> 1b7) kupinduliwa

Neno hili hili la Kiebrania katika kisa kimoja cha "Niphal" linatumika kuelezea moyo wa Mungu na hisia zake kwa Israeli.

> "Niwezeje kukuacha, Efraimu? Niwezeje kukuponya, Israeli? Niwezeje kukufanya kama Adma? Niwezeje kukuweka kama Seboimu? **Moyo wangu umegeuka**[H2015] ndani yangu, huruma zangu zimewaka pamoja." Hosea 11:8

Je, inawezekana kwamba kile ambacho Mungu alimwambia Yona kilikuwa kwamba 'Angepindua' mioyo ya watu wa jiji la Ninawi – akimaanisha kuwaleta kwenye toba? Na je, inawezekana kwamba Yona, kwa sababu ya upendeleo wake mwenyewe, alielewa neno la Mungu la kupindua lilimaanisha mji wenyewe, kupindua mji na kwa hiyo watu ndani yake? Je, inaweza kuwa kwamba badala ya kuharibu jiji, Mungu alikuwa akisema angepindua mioyo ya watu ndani ya siku 40?

Tunaona ushahidi wa aina hii ya kuchanganyikiwa kwa wale wanaoitikia mafundisho ya Yesu mara kadhaa. Yesu alipowaambia wale waliomzunguka kulivunja hekalu (Yohana 2:19). Wasikilizaji wake walifikiri kwamba alikuwa anazungumza juu ya jengo la hekalu, lakini alikuwa anajizungumzia Mwenyewe. Ni muhimu kutambua kwamba ni kutokuelewana huko ndiko kulikotumiwa kumhukumu Yesu kifo, akisema kwamba alitaka kulivunja hekalu. Yesu alipozungumza na mwanamke kisimani katika Yohana 4 kuhusu maji, alifikiri alimaanisha maji halisia lakini kwa hakika alimaanisha maji ya kiroho. Yesu alipowaambia wanafunzi wake wajihadhari na chachu ya Mafarisayo, walifikiri anazungumza juu ya mkate halisia lakini alikuwa anazungumza juu ya mkate wa kiroho.

Je, tunaelewaje basi lugha ya Yona 3:10 ambapo inasema kwamba Mungu alighairi maafa ambayo angewaletea na hakuyafanya. Je, hili linazungumza kulingana na jinsi Mungu alivyokuwa akitenda, au lilikuwa linazungumza kulingana na jinsi watu walivyofasiri matukio? Don Stewart, mwanatheolojia na mchambuzi wa Biblia, ametoa maoni yake kuhusu kisa hiki.

> Je, Mungu Alibadilisha Mawazo Yake Kuhusu Alichopaswa Kukifanya kwa Watu wa Ninawi?

> Katika Kitabu cha Yona kuna habari ya watu wa Ninawi kutubu katika mahubiri ya Yona. Katika mwitikio wa toba ya watu Biblia inasema kwamba Mungu alighairi kile ambacho alikuwa karibu kuwatendea watu.
>
> Hii imetumika kama mfano halisi wa Mungu kubadilisha mawazo yake kutokana na watu kujinyenyekeza na kuomba msamaha Wake. Inaaminika pia kwamba mipango ya Mungu inabadilika kwa sababu ya matendo ya wanadamu. Hitimisho ni kwamba siku na matukio yajao hayajapangwa. Mambo huweza kubadilika kulingana na tabia ya wanadamu.
>
> Walakini hii sio njia pekee ya kuangalia kifungu hiki. Kwanza, hakukuwa na ujumbe wa toba katika mahubiri ya Yona. Hakuna! Alisema kwamba jiji la Ninawi lingeangamizwa. Nukta. Hakuna tumaini lililotolewa, hakuna msamaha ulioongezwa. Wakiwa peke yao, watu wa Ninawi walijinyenyekeza na kuomba msamaha wa Mungu. Kwa mtazamo wa kibinadamu Mungu alibadilisha mawazo Yake na hakuangamiza Ninawi. **Lakini hatupaswi kudhani kwamba Mungu alibadilisha mpango wake. Kwa kuwa Yeye anajua sana wakati ujao, alijua kwamba wangetubu. Kwa hiyo, ujumbe wa kuangamizwa kwa Ninawi haukuwa jambo ambalo Mungu aliamuru kwamba lingetokea.**[8]

Tunaona jinsi Don Stewart, anavyofasiri maandiko kulingana na wazo lisilohamishika akilini mwake la kujua kwa ukamilifu siku zijazo. Anatoa jambo zuri kuhusu Yona kujua kwamba Mungu alikuwa mwenye rehema. Yona kimsingi anasema – "Nilijua ungefanya hivi!"

> "Lakini jambo hili lilimchukiza Yona sana, naye akakasirika. Akamwomba BWANA, akasema, Nakuomba, Ee BWANA; sivyo hivyo nilivyosema, hapo nilipokuwa katika nchi yangu? Hii ndiyo sababu nalifanya haraka kukimbilia Tarshishi; **kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa**

[8] https://www.blueletterbible.org/Comm/stewart_don/faq/does-god-know-everything/27-did-god-change-his-mind-about-nineveh.cfm

**huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya."** Yona 4:1-2 (KJV)

Je, Yona angewezaje kujua huruma ya Mungu ili kuamua matokeo bora kuliko Mungu Mwenyewe? Hilo haliwezekani. Mungu anaweza kusoma moyo wa mwanadamu. Anajua yaliyo katika akili za wanadamu. Tunaposoma katika Zaburi, Mungu anajua maneno nitakayosema kabla sijasema. (Zaburi 139:1-7). Kusema kwamba Mungu hakujua matokeo ya Jiji la Ninawi siku 40 kabla ya tukio lililotajwa huonekana kupunguza hekima ya Mungu na uwezo Wake wa kusoma mioyo ya wanadamu. Ikiwa Mungu angeweza kutabiri katika Zaburi ya 22 maneno yale ambayo wale waliomsulubisha Yesu wangetamka miaka 1000 katika siku zijazo, basi bila shaka angeweza kujua jinsi ambavyo watu wa Ninawi wangeitikia siku 40 zijazo.

Don Stewart anatoa hoja hiyo katika msingi wa kujua kikamilifu siku zijazo kutokana na uwezo wa Mungu kujua yote. Inaweza pia kujadiliwa kwa vigezo vingine ambavyo tutachunguza katika kitabu hiki. Hoja yangu katika kuibua kisa hiki ni kwamba baadhi ya watu wanaotetea kwamba Mungu hajui mambo yote haswa katika siku zijazo wanaweza kuwa na nguvu katika kutumia mfano huu. Tunahitaji kuchunguza ushahidi kwa uangalifu na kwa utaratibu.

Katika kisa cha Yona, maswala ni magumu zaidi kuliko labda ilivyofikiriwa hapo awali. Ikiwa Mungu angemwambia Yona aende Ninawi na kuwaambia "Najua mtatubu," haingeleta matokeo sahihi. Kwa namna hiyohiyo Yesu alimwambia mwanamke Mkanaani "Si vema kutwaa mkate wa watoto na kuwatupia mbwa" (Mathayo 15:26), hivyo Mungu alimpa Yona ujumbe kwamba ataupindua mji huo. Yona alitamani watu wa Ninawi wafe. Mungu alimpa Yona ujumbe ambao alijua Yona angeubeba kwa sababu Yona angeweza kukataa kuufanya ikiwa Mungu angesema tofauti.

Kama tulivyogundua, neno *kupindua* [H2015] katika Kiebrania linaweza kueleweka kwa njia mbili tofauti. Kama vile ambavyo Yesu hakumwita yule mwanamke mbwa bali alisema tu kwamba si sawa kuwapa mbwa chakula cha watoto, Mungu hakusema angeangamiza jiji hilo kwa jinsi ya kimwili bali alitumia neno lililomaanisha jambo tofauti kiroho. Kama vile ambavyo mwanamke alifikiri kwamba Yesu alimwita mbwa lakini aling'ang'ania na kudai wokovu, ndivyo

Waninawi walivyofikiri kwamba Mungu angewaangamiza na wakatubu na kupokea wokovu.

Ni kweli kwamba kama Waninawi hawangetubu jiji lao lingekabiliwa na maafa, lakini maelezo ya jambo hili yako nje ya upeo wa sasa wa kitabu hiki. Kusudi la sura hii lilikuwa kuchunguza Biblia na kufichua mvutano unaoonekana kuwepo katika Maandiko kati ya uwezo wa Mungu wa kujua yajayo na mwingiliano Wake na wanadamu na kile kinachoonekana kuwa mwitikio wa kihisia na mabadiliko ya lile lililokusudiwa.

Nyanja inayofuata tunayotaka kuongeza kwenye swali hili la maarifa ya Mungu ni kupitia Yesu. Katika mazungumzo na wanafunzi wake, Yesu alisema maneno haya mazito:

> Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba yangu; Yohana 14:6-7 (KJV)

Kuja kwa Baba kupitia kwa Mwana ndio muktadha wa Yesu kuwa njia, ukweli na uzima. Yesu ndiye ukweli juu ya Baba na kwa hivyo ndiye njia pekee ya kwenda kwa Baba. Umuhimu wa maneno haya ni wa ndani zaidi kuliko uwezo wa kusali kwa Baba. Inajumuisha kila kitu tunachoweza kujua kuhusu Mungu ambacho kinajumuisha somo la kujua yote.

SURA YA 4

# KRISTO ALIYE UKWELI WA BABA

Katika kutafuta kwetu ukweli juu ya Mungu ni lazima tukumbuke baadhi ya mambo muhimu.

> “Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.” Isaya 55:8-9

Kwa kuwa mawazo ya Mungu si yetu, haiwezekani sisi kuwaza chochote kuhusiana na Mungu nje ya kile kilichofunuliwa na Mwanawe. kitabu cha Waebrania kinasema hivi juu ya Mwana wa Mungu:

> …**Yeye kwa kuwa ni mng’ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake**, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; Waebrania 1:3

Kristo ndiye sura halisi au mwakilishi kamili wa Baba. Yeye ndiye mng’ao wa utukufu wa tabia ya Baba. Katika kuuvaa asili ya kibinadamu, Kristo alitengeneza daraja pekee linalowezekana kwetu kuja kwa Baba. Kuja huku kwa Baba hakuhusiani tu na ukaribu au jiografia bali pia mitazamo yetu kuhusu Mungu ni nani.

Akili ya mwanadamu, kwa sababu ya dhambi, iko katika giza zito juu ya Mungu kiasi kwamba ilimbidi Yesu aje kumfunua kwetu.

> “Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.” Warumi 8:6-7

Adamu na Hawa walipofanya dhambi, waliiweka jamii ya wanadamu katika mwelekeo ambao ulikuwa na uadui kwa Mungu. Akili zetu kwa asili haziendani na Mungu au njia zake. Kutomwamini kwetu kwa asili kunatufanya tushindwe kuamini kiurahisi chochote Anachokisema. Kimsingi "tunapenda giza kuliko nuru, kwa sababu matendo yetu ni maovu," ingawa sheria hii ya mwili wetu inajidhihirisha kwa njia nyingi tofauti na kwa ujumla hatujui kiwango kamili cha asili na matendo yetu (Yohana 3:19).

> Kama Maandiko yanavyosema, “Hakuna mwenye haki, hata mmoja. Hakuna aliye na hekima ya kweli; hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamekengeuka; wote wamekuwa bure. Hakuna atendaye mema, hata mmoja.” Warumi 3:10-12 (NLT)

Biblia inatuambia kwamba katika hali yetu ya asili ya kuanguka hatumtafuti Mungu. Ina maana haiwezekani kwetu kuweza kuelewa Mungu ni nani au jinsi alivyo isipokuwa kwa njia ya Yesu Kristo. Inamaanisha kwamba chochote tunachosoma kuhusu Mungu katika Biblia kitapindishwa moja kwa moja na kupotoshwa kwa njia inayomshambulia Mungu na kutuweka gizani isipokuwa tukija kwa Kristo na kuzaliwa mara ya pili kutoka juu.

> “Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;” Yohana 1:10-12

Hata watu wa Mungu wenyewe, ambao walifundishwa mengi sana juu ya Mungu, walimkataa Kristo alipokuja duniani. Hawakumtambua alipokuja kwa sababu taifa zima lilikuwa limepotosha maneno ya manabii ambayo Mungu aliwatuma kwao. Badala ya kumkubali Yesu kuwa Masihi, waligeuza maneno ya Yesu kwa njia ya kumuua.

Je, lingekuwa jambo la hekima kwetu kufikiri kwamba sisi ni tofauti na Israeli wa kale? Je, kuna sifa fulani tuliyo nayo ndani yetu ambayo

hutuwezesha kutenda kwa njia tofauti na wao? Haya ni mambo muhimu ya kuzingatia katika harakati zetu za kumjua Mungu na kile anachokijua.

> "Maana nataka ninyi mjue jinsi ilivyo kuu juhudi yangu niliyo nayo kwa ajili yenu, na kwa ajili ya wale wa Laodikia, na wale wasioniona uso wangu katika mwili; ili wafarijiwe mioyo yao, **wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo; ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika**." Wakolosai 2:1-3

Mtume Paulo akiwa amevuviwa anatuambia kwamba siri ya Mungu, ambayo Yeye huipanua kumaanisha Baba na Kristo, ijumuishayo hazina zote za hekima na maarifa.

Tungethibitisha kwamba watu wengi wanaamini kwamba Mungu ana hazina zote za hekima na maarifa; lakini jambo ambalo Paulo anakazia ni kwamba katika kujua Baba na Mwana ni nani na upendo walio nao, tuna ufunguo wa kuwa na uhakika kamili wa kuelewa. Na kwa vile Kristo ndiye njia pekee ya kumjua Baba, hili lina maana kwamba tunapojua ukweli kuhusu Mwana wa Mungu, basi tunakuwa na ufunguo wa kujua hazina za hekima na maarifa.

Tunakumbuka kwamba Yesu hakusema tu kwamba ana ukweli, bali Yeye ndiye ukweli. Katika kumjua Yeye - jinsi alivyo - tuna ufunguo wa kujua ukweli juu ya Mungu. Hilo linatia ndani ukweli kuhusu mambo ambayo Mungu anayajua, kwa kuwa Yesu ndiye ukweli wa kila jambo.

> …"bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu." 1 Wakorintho 1:24

Ikiwa Kristo ndiye hekima ya Mungu, basi njia pekee ya kuelewa hekima hii ni kwa kumjua Mwana wa Mungu. Kuna tofauti kati ya kujua kumhusu Yeye na kumjua Yeye haswa. Njia pekee ya kumjua Kristo ni kujazwa na Roho wake. Huwezi kumjua kama huna Roho wake anayeishi ndani yako, kwa sababu moyo wa mwanadamu kwa kawaida unapingana na Kristo na unageuza kila kitu kumhusu kuwa uongo. Ni kwa kujisalimisha kwa moyo tu - kukubali kwamba sisi ni waovu na tuna hatia ya kifo cha Mwana wa Mungu, lakini

tumesamehewa - tunaweza kupokea Roho Wake na kisha kumjua. Wakati Roho wa Kristo anapokaa ndani yetu, tunaweza kusema pamoja na Paulo:

> Maana, "Ni nani awezaye kuyajua mawazo ya BWANA? Ni nani ajuaye kutosha kumfundisha?" Lakini tunaelewa mambo haya, kwa kuwa tunayo nia ya Kristo. 1 Wakorintho 2:16 (NLT)

Ni ajabu jinsi gani kujua mawazo ya Bwana tunapokuwa na nia ya Kristo! Tunarudia jambo hili muhimu kwamba katika kujua tu utambulisho wa kweli wa Mwana wa Mungu na wakati huo huo kumkumbatia Yesu - Mwana wa Adamu - tunaweza kupokea Roho wa Yesu na kujua Mungu ni nani na mawazo yake ni yapi. Sasa tunaingia kwenye ufafanuzi wa Biblia wa uzima wa milele.

> "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." Yohana 17:3

Uzima wa milele ni kumjua Mungu wa pekee wa kweli ambaye ni Baba na Yesu Kristo ambaye Baba alimtuma kwetu. Njia pekee ya kumjua Baba ni kupitia Yule aliyetumwa kwetu. Kwa hiyo, jambo la kwanza tunalopaswa kulikiri kwa ajili ya uzima wa milele ni kuamini kwamba Baba ndiye Mungu wa pekee wa kweli na ya kwamba Mungu alimtuma Mwanawe kwetu.

> "lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo." 1 Wakorintho 8:6

Mstari huu ambao tumetoka kuusoma unatuletea ufunguo[9] wa hazina za hekima na maarifa yote yanayopatikana ndani ya Baba na Mwana (Wakolosai 2:2-3) Baba ndiye chanzo cha vitu vyote na ni Mwanawe ambaye kupitia yeye tunapokea yote aliyo nayo Baba.Tusipokubali haya basi hatuwezi kupata njia ya kwenda kwa Baba na hatuwezi kuelewa ni nini maana ya yeye kujua yote. Hebu nielezee hili kiundani

---

[9] Kujifunza zaidi kuhusu somo hili kwa ajili ya kufungua hazina zote za hekima na maarifa angalia kijitabu *Divine Pattern of Life* kinachopatikana katika fatheroflove.info. Kwa uwasilishaji zaidi wa kanuni hizi angalia kitabu *Escaping the Pentagon of Lies* ambacho pia hupatikana katika fatheroflove.info

zaidi kwa kadri ambavyo kanuni hii inavyoweza kuwa ngumu kuifahamu.

> “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, **naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho**; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina;” Wafilipi 2:5-9

Yesu hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho. Ukristo wote unaamini kwamba Kristo ni sawa na Baba. Jambo kuu la kujua ni nini kinachomfanya Mwana kuwa sawa na Baba? Hebu tugeukie imani maarufu ya Athanasia na tuone jinsi inavyoamua usawa wa Baba na Mwana na Roho.

> Kwa maana kuna Nafsi moja ya Baba; nyingine ya Mwana; na nyingine ya Roho Mtakatifu. Lakini Uungu wa Baba, wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, wote ni mmoja; **wana utukufu sawia, Ukuu wa milele**. Kama vile Baba alivyo; ndivyo alivyo Mwana; na ndivyo alivyo Roho Mtakatifu. **Baba asiyeumbwa; Mwana asiyeumbwa; na Roho Mtakatifu asiyeumbwa. Baba hana kikomo; Mwana hana kikomo; na Roho Mtakatifu hana kikomo. Baba wa milele; Mwana wa milele; na Roho Mtakatifu wa milele**. Na bado wao si wa milele watatu; bali mmoja wa milele. Vile vile hakuna watatu ambao hawajaumbwa; wala watatu wasio na mwisho, bali mmoja asiyeumbwa; na moja asiye na mwisho. Vivyo hivyo **Baba ni Mwenyezi; Mwana Mwenyezi; na Roho Mtakatifu Mwenyezi.** Na bado wao si Wafalme watatu; bali Mwenyezi Mungu mmoja. **Kwa hiyo Baba ni Mungu; Mwana ni Mungu; na Roho Mtakatifu ni Mungu.** Na bado wao si Miungu watatu; bali Mungu mmoja. Vivyo hivyo **Baba ni Bwana; Mwana Bwana; na Roho Mtakatifu Bwana.** Na bado si Mabwana watatu; bali Bwana mmoja. Kwa maana kama vile tunavyolazimishwa na ukweli wa Kikristo; kukiri kila Nafsi peke yake kuwa Mungu na Bwana; Vivyo hivyo tumekatazwa na dini

> ya kikatoliki; kusema, Kuna Miungu watatu, au Mabwana watatu. Baba hakufanywa na yeyote; hakuumbwa, wala hakuzaliwa. Mwana ni wa Baba peke yake; hajafanywa, wala hajaumbwa; bali kuzaliwa. Roho Mtakatifu ni wa Baba na wa Mwana; wala hakutengenezwa, wala hakuumbwa, wala hakuzaliwa; lakini anatoka kwao. Kwa hiyo kuna Baba mmoja, si Mababa watatu; Mwana mmoja, si Wana watatu; Roho Mtakatifu mmoja, si Roho Mtakatifu watatu**. Na katika Utatu huu hakuna aliyekuwepo kabla, au baada ya mwingine; hakuna aliye mkuu, au mdogo kuliko mwingine. Lakini Nafsi zote tatu ni za milele, na zinalingana**. Ili katika mambo yote, kama ilivyosemwa hapo juu; Umoja katika Utatu, na Utatu katika Umoja, unapaswa kuabudiwa. Kwa hiyo atakayeokoka, na afikirie hivi juu ya Utatu.
> - Dondoo kutoka kwa Imani ya Athanasian. (karne ya 5 BK)

Imani hii inafafanua usawa wa Baba na Mwana kwa maneno kama haya: utukufu, ukuu, kutoumbwa, kutokuwa na mipaka, milele, Mwenyezi, Mungu, Bwana. Baba, Mwana au Roho Mtakatifu, hakuna ambaye ni "mkuu au mdogo kuliko mwingine," lakini badala yake wote "ni sawa na wa milele."

Usawa kama unavyoonyeshwa katika Utatu ni usawa wa nguvu, nafasi, ukuu. Ni usawa wa sifa za asili za kibinafsi. Uungu unaonyeshwa kupitia nguvu, utawala, enzi ya milele.

Tofauti na hili, Mwana mzaliwa wa Biblia atoa picha tofauti ya usawa. Hebu tuchunguze baadhi ya Maandiko yanayofunua utambulisho Wake wa kweli.

> Ambaye ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake… Waebrania 1:3

> "Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, **wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako**, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma." Yohana 17:8

> "BWANA alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. **Nalitukuka tokea milele**, tangu awali, Kabla haijawako dunia. **Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa,** Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji." Mithali 8:22-24

> "Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa." Zaburi 2:7

> "Lakini wewe, Ee Bethlehemu Efrata, ni kijiji kidogo tu kati ya watu wote wa Yuda. Lakini mtawala wa Israeli atakuja kutoka kwako, **ambaye asili yake ni kutoka zamani za kale**." Mika 5:2 (NLT)

Ukweli wa utambulisho wa Mwana wa Mungu ni kwamba alizaliwa na Baba katika umilele. Aliletwa kutoka kwa Baba na kuanzishwa kutoka milele. Mwana wa Mungu alipokea kila kitu alichonacho kutoka kwa Baba yake. Alirithi kila kitu kutoka kwa Baba yake. Hili ndilo linalomfanya kuwa mng'ao wa utukufu wa Baba.[10] Huyu ni Mwana tofauti kabisa na yule anayetajwa katika kanuni ya imani ya Athanasian. Imani inasema kwamba Kristo amezaliwa, lakini hili linapotea katika kauli za usawa kupitia uwezo, nafasi na enzi ya milele. Linalazimishwa katika fumbo lisiloeleweka nje ya ukweli wa Maandiko.

Mwana mzaliwa wa kweli alirithi uungu wake na kwa hiyo usawa wake kwa Baba unategemea zawadi ya Baba ya urithi na juu ya amri ya Baba. Si nguvu za Mwana zinazomfanya Mwana kuwa sawa na Baba, bali ni neno la Baba ndilo linalomfanya Mwana kuwa sawa na Baba.

> Bali kwa Mwana [Baba] asema, Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, ni cha milele na milele; fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki."—Waebrania 1:8. (KJV)

Tofauti hii ya usawa ndiyo ufunguo wa kuelewa tofauti kati ya ujuzi (omniscient) wa kweli wa kibiblia na ule wa uwongo, ambao ni ibada ya sanamu ya mwanadamu ya maarifa yanayoelekezwa mbinguni.

Mwana wa Mungu tunayemwabudu anafafanua mfumo tunaotumia kutathmini sifa. Mitazamo yetu ya usawa hufichua mfumo wa thamani tulio nao kuhusu kile ambacho ni cha muhimu zaidi. Ikiwa usawa wa Yesu unategemea ukuu, nguvu, utukufu na enzi ya milele,

---

[10] Kujifunza zaidi kuhusiana na suala hili angalia kitabu *Wisdom of God* na *My Beloved* vinavyopatikana katika *fatheroflove.info*

basi unalazimika kushinikiza sifa hizi zote kwa kiwango cha juu zaidi kinachoweza kuwakilishwa na kumwita huyu Mungu . Katika mfumo huu, matamko ya Mungu kuhusu thamani ya Mwanawe; Mungu akimfufua Mwanawe kwa upendo; Mungu akimtangaza Mwanawe kama mungu kwa sababu Mwanawe wa pekee ndiye anayemjua Yeye - yote haya yanachukuliwa kuwa hayatoshi kumpa Mwana uungu, kwa sababu haijalishi kwetu ni kigezo gani cha Baba cha kumtangaza Kristo kikamilifu. tuna vigezo vyetu na tunadai Yesu aendane na vigezo hivyo.

Katika mfumo huu wa Utatu tunaunda mfumo wa thamani wa usawa ambao unalazimisha maarifa Yao kuwa kila kitu kabisa ili ichukuliwe kuwa ya kiungu, na kisha tunalazimisha Maandiko kuendana na dhana hii. Tunaishia kufafanua kile ambacho ni cha kimungu sisi wenyewe, badala ya kumwacha Mungu afafanue kile ambacho ni cha kimungu. Maelezo yetu juu ya uungu ni nini yanashinda maelezo yake ya uungu ni nini - kosa ambalo wanafalsafa wengi wa kale wa Kigiriki walioingia katika Ukristo walilifanya, ndiyo maana, karne nyingi baada ya kifo cha Yesu, Utatu ulikuja kuelezwa kwa mara ya kwanza kabisa.

Kutoka gizani juu ya somo hili haiwezekani bila dawa ya macho ya kimungu. Baada ya kupokea zawadi ya nuru ya kimungu, inahitajika kwenda hatua kwa hatua ili kutambua udanganyifu ambao Shetani ameutumia kufunga akili ya Kikristo na fundisho la Utatu. Ni mfumo unaoharibu kabisa utambulisho wa kweli wa Mwana wa Mungu na kufanya isiwezekane kwa mawazo yetu kuwa mawazo ya Mungu na njia zetu njia zake. Ndiyo maana Yohana anasema:

> "Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:12
>
> "Kila amkanaye Mwana, hanaye Baba; amkiriye Mwana anaye Baba pia." 1 Yohana 2:23

Mwana pekee ndiye njia ya pekee ya kwenda kwa Baba: kwa kuukubali Uana wa kweli wa Yesu tunayo nafasi ya kuuacha uwongo wa usawa kupitia uwezo na nafasi, na kujiweka upya katika uhusiano wa kweli wa usawa wa Baba na Mwana. .

Utatu huifunga akili ya mwanadamu katika mtazamo wa kujua yote (omniscient) unaotoleteleza matokeo mbalimbali ya kutisha, ambapo lililo kuu ni imani kwamba Mungu alijua kwa hakika kwamba wanadamu wangeanguka kabla ya kuwaumba. Baada ya kukubali dhana hii, mantiki bila shaka hutuongoza katika kuamini kwamba Mungu ndiye anayehusika na dhambi zote za ulimwengu huu, au kwamba kwa namna fulani taabu na kifo cha mabilioni hudhihirisha hekima na upendo Wake. Je, inashangaza kutambua kwamba wengi wa wakazi dunia hawakubaliani na wazo hili?

Mwana pekee ndiye njia pekee ya kujua ukweli wa Baba. (Yohana 3:18).

SURA YA 5

# MTOTO ALIYEFUNZWA AU FUNDI STADI

Ni muhimu kutofautisha tofauti hii kati ya Mwana pekee na 'Mungu Mwana' kwa jinsi tunavyomwendea Mungu na kile tunachoelewa kumhusu. Mahali pa kuvutia pa kuchunguza ni katika Mithali 8.

> "Mimi, hekima, nimefanya werevu kuwa kao langu; Natafuta maarifa na busara. Kumcha BWANA ni kuchukia uovu; Kiburi na majivuno, na njia mbovu, Na kinywa cha ukaidi pia nakichukia. Shauri ni langu, na maarifa yaliyo sahihi; Mimi ni ufahamu, mimi nina nguvu. Kwa msaada wangu wafalme humiliki, Na wakuu wanahukumu haki. Kwa msaada wangu wakuu hutawala, Na waungwana, naam, waamuzi wote wa dunia." Mithali 8:12-16

Je, mtu huyu anayezungumza ni nani? Mwanzoni katika sura hiyo hekima inaelezwa kama ni mwanamke.

> "Je! Hekima halii? Ufahamu hatoi sauti yake? Juu ya mahali palipoinuka karibu na njia, Penye njia panda, ndipo asimamapo. Karibu na malango, mahali pa kuingia mjini, Mahali pa kuyaingilia malango anapiga kelele." Mithali 8:1-3

Hata hivyo, tukisoma baadaye katika sura hiyo, hekima inaelezewa katika sifa ya mwanamume (masculine).

> "Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama **stadi wa kazi**; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake;" Mithali 8:30

Neno lililotafsiriwa hapo juu fundi stadi liko katika umbo la kiume na kwa hiyo linaonyesha mwanamume badala ya mwanamke. Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu kama kuna uhusiano kati ya mtu huyu anayeitwa hekima na Yesu Kristo. Wale wanaokataa uhusiano huo wanasema hekima ni mtu tu.[11] Wale wanaokubali uhusiano huo[12] wanataja rejea kama hizi:

> "bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, **ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu**. Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, a**liyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu,** na haki, na utakatifu, na ukombozi;" 1 Wakorintho 1:24,30

> "ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo; **ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika**." Wakolosai 2:2-3

Ikiwa tunaruhusu Biblia ijitafsiri yenyewe, je, haitakuwa dhahiri kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Kristo na hekima? Moja ya sababu zinazofanya kuweko na kusitasita kufanya uhusiano huu ni kwa sababu ya mistari tuliyonukuu katika sura iliyotangulia inayomwasilisha hekima kama *aliyezaliwa na kutukuka.*

Katika makala niliyotaja hapo juu katika rejea ya 11, mojawapo ya hoja zinazotolewa ili kukataa uhusiano wa hekima na Kristo ni kwa sababu Mashahidi wa Yehova hutumia mistari hiyo kuthibitisha kwamba Mwana wa Mungu ni kiumbe aliyeumbwa. Kwa sababu Ukristo haukubaliani na kwamba Kristo ni kiumbe aliyeumbwa, mwandishi anataka kuvunja uhusiano wa wasomaji uliopo kati ya hekima na Kristo. Lakini je, tunapaswa kukataa jambo fulani kwa sababu ya yale ambayo kundi fulani huyadai? Mwana pekee si kiumbe aliyeumbwa. Kutumia mtazamo wa kundi lingine juu ya andiko fulani ili kumfanya mtu aelekee upande fulani ni tatizo sana, lakini kama tulivyosema

---

[11] https://www.equip.org/article/who-is-wisdom-in-proverbs-8/

[12] https://www.reformation21.org/articles/does-proverbs-speak-of-jesus.php

katika sura iliyotangulia, mfumo wa Utatu na mawazo yake una uwezo huu wa kuziba akili ya mwanadamu kufikiri katika mwelekeo fulani na kukataa muunganiko ulio dhahiri.

Vipi basi kuhusiana rejea ya hekima kuwasilishwa katika sifa ya kike (feminine)? Je, hii haipaswi kupunguza muunganiko uliofanywa?

> .....”na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.” Ufunuo wa Yohana 1:13 (YLT)

Maelezo ya Kristo hapa yanajumuisha rejea ya matiti. Neno hili kwa Kigiriki ni mastos. Hili ni neno linalomanisha matiti ya kike. Kwa kiingereza tuna neno mastitis lenye maana ya kuvimba kwa titi. Kwa nini Yesu anatajwa kwa neno linalomaanisha matiti ya kike? Hii inatupa uhusiano na aya kama hizi.

> “Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu;” 1 Petro 2:2

> “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Yohana 1:1

Pia tunamwona Yesu akijizungumzia Mwenyewe akitumia sifa za kike katika mistari kama hii:

> “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, **kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake** chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!” Mathayo 23:37

Kwa hiyo kuelezea hekima katika sifa ya kike hupata maana kamili. Kristo ni wazi anafunua sifa zote mbili za kiume na za kike, kwa maana wote wawili, mwanamume na mwanamke, wameumbwa kwa mfano wa Mungu.

Kwa kuzingatia mambo haya hebu tuchimbue zaidi maandishi yanayomzungumzia fundi stadi.

> Kisha nilikuwa karibu naye, **kama mtu aliyelelewa naye**[H525];
> na kila siku nilikuwa furaha yake, nikifurahi daima mbele zake.
> Mithali 8:30 (KJV)

Ikiwa tutaondoa maneno yaliyoongezwa, litasomeka. "Kisha nilikuwa naye, mmoja aliyelelewa." Kwa nini KJV inatafsiri neno hili kama *mtu aliyelelewa badala ya fundi stadi?*

Neno la Kiebrania ni *'âmôn*[H525]. Mzizi wa neno hili ni '*âman* [H539] ambalo linamaanisha "kujenga au kutegemeza; kukuza kama mzazi au muuguzi." Neno lingine kama hilo linalobeba maana ya fundi stadi ni '*âmân*.[H542]. Kwa hivyo kutafsiri neno '*âmôn* kama mbunifu au fundi stadi ni tafsiri sahihi kwa sababu hii imejumuishwa katika maana. Inafurahisha kuona jinsi ambavyo matoleo mbalimbali na hata lugha tofauti zimetafsiri neno hili.

| Toleo | Lugha | Maana |
|---|---|---|
| New Living | Kingereza | Mbunifu |
| Revised | Kingereza | Mtendakazi mkuu |
| Geneva | Kingereza | Mnawilishaji |
| New International | Kingereza | (Halijatafsiriwa) |
| Luther Bible | Kijerumani – Werkmeister | Msimamizi |
| Staten Vertaling | kiholanzi – Voedsterling | Uleaji |
| Synodal Text | Kirusi – художницею | Msanii |
| Biblia Hebraica | Kiebrania Interlinear | Kupapasa |
| LXX | Kigiriki Harmozō | Kujiunga, kubembeleza, kuchumbiwa |
| Brenton | Tafsiri ya kingereza ya LXX | Kujitosheleza kwake |

Tunaona maana tofauti tofauti kutoka kwenye kanuni ya karibu zaidi ya kulelewa au kunawilishwa hadi kwenye msisitizo wa mfanyakazi mwenye ujuzi. Tukichukua tafsiri ya King James, Geneva au Kiholanzi tunaona picha ya mtu ambaye alilelewa kwa upendo, kulishwa, kunawilishwa na kutunzwa na mzazi. Neno lililotafsiriwa katika Biblia Hebraica ni kupapasa, lisichanganywe na tendo la kupapasa kwa sababu neno hilo katika Kiebrania ni nomino. Maana ya kale ya Kiingereza ya neno hili kama nomino ni mtu anayependwa sana.[13]

Picha iliyotolewa hapa ni ya Baba mpole ambaye anampenda sana mtoto Wake. Pia inatoa picha ya kulea mtoto huyu na kumfundisha. Maana hii inapata mvuto katika maneno ambayo Baba alizungumza na Mwanawe wakati wa ubatizo wake.

> Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni mwanangu mpendwa, ninayefurahishwa naye. Mathayo 3:17 – Tyndale

Hii inaunganisha kwa uzuri zaidi katika Mithali 8:30 ambapo inasema katika toleo la King James kwamba "Nilikuwa furaha yake kila siku."

Kwa hekima isiyo na kikomo ya Mungu, Kiebrania humpa msomaji uwezo wa kutafsiri maandishi kama fundi stadi au mtoto wa thamani, anayelelewa ambaye amefunzwa na Baba Yake. Unaona nini? Uchaguzi unaofanya unakuambia kitu kuhusu Baba. Je, huyu ni Baba mpole anayemtunza Mwanawe wa thamani na kumfurahia? Au je, huku ndiko kujisifu kwa Kristo kwamba Yeye ni fundi stadi ambaye kwa ustadi wake alimfurahisha Baba?

Tukichagua chaguo la fundi stadi, tunaweza kuficha maana ya kwamba Kristo alifunzwa na kufundishwa na Baba Yake. Neno hili peke yake linazungumza tu juu ya uwezo wake na sio uhusiano wake na Baba.[14]

Mwishoni mwa sura ya 3, tulisema yafuatayo:

> Kuja kwa Baba kupitia kwa Mwana ndio muktadha wa Yesu kuwa njia, ukweli na uzima. Yesu ndiye ukweli juu ya Baba na

---

[13] https://en.wiktionary.org/wiki/fondling

[14] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na utofauti huu tazama kitabu *Identity Wars* kinachopatikana katika *fatheroflove.info*

> kwa hivyo ndiye njia pekee ya kwenda kwa Baba. Umuhimu wa maneno haya ni wa ndani zaidi kuliko uwezo wa kusali kwa Baba. Inajumuisha kila kitu tunachoweza kukijua kuhusu Mungu ambacho kinajumuisha somo la kujua yote.

Yesu alipokuja katika dunia hii, alidhihirisha kile kisichoonekana. Hii ni sehemu kuu na ya muhimu ya kazi ya Yesu.

> "naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote." Wakolosai 1:15

Fikiria mistari ifuatayo kwa uangalifu katika nuru ya ukweli huu kwamba Kristo ndiye anayefanya asiyeonekana, kuonekana.

> "Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake." Luka 2:40

> "Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." Luka 2:52

Je, mistari hii inazungumzia tu maisha ya Kristo duniani au inafichua yale yaliyokuwa yamefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu?

> "Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na **ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele,**" Warumi 16:25

Maisha ya Yesu duniani yalivuta pazia la umilele na kukafunuliwa kwetu mambo yaliyokuwa yamefichwa tangu zamani. Katika utoto wa Kristo duniani, tumefunuliwa kwetu Ubaba wa upendo wa Mungu ambaye alimfunza Mwanawe kwa upole katika ulimwengu wa umilele. Hili linatoa nuru kubwa zaidi kwa kauli zifuatazo za Yesu:

> "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, naye humwonyesha[G1166] yote ayatendayo mwenyewe; hata na kazi kubwa zaidi kuliko hizo atamwonyesha, ili ninyi mpate kustaajabu." Yohana 5:19-20

Kamusi ya Kigiriki ya Thayer inatoa maana ifuatayo la neno *kuonyesha:*

1) kuonyesha, kufichua mbele ya macho yako
2) kisitiari
2a) kutoa ushahidi au uthibitisho wa jambo
2b) kuonyesha kwa maneno au kufundisha

Yesu anatuambia y kwamba Baba yake alimfundisha mambo yote. Wazo hili limepanuliwa katika Zaburi. Je, Kristo hakuwaelekeza wanafunzi wake kwenye Zaburi ili kuwafundisha kumhusu Yeye? (Luka 24:44).

> "Ndipo niliposema, Tazama nimekuja, (Katika gombo la chuo nimeandikiwa,) Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:7-8

> "Ee BWANA, unijulishe njia zako, Unifundishe mapito yako, Uniongoze katika kweli yako, Na kunifundisha. Maana Wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, Nakungoja Wewe mchana kutwa." Zaburi 25:4-5

> "Ee BWANA, unifundishe njia yako, Na kuniongoza katika njia iliyonyoka; Kwa sababu yao wanaoniotea; Usinitie katika nia ya watesi wangu; Maana mashahidi wa uongo wameniondokea, Nao watoao jeuri kama pumzi." Zaburi 27:11-12

Mwana mpendwa wa Mungu anatufunulia upendo kama wa mzazi mpole, wa Baba anayemlea Mwanawe. Ukweli huu unatupatia maana halisi ya maarifa kwetu. Katika Utatu, maarifa ndicho kitambulisho kinachokupa thamani yako ya asili na hivyo yeyote anayedhaniwa kuwa wa thamani katika nyanja yake itamlazimu kuwa anayejua kila kitu. Mwana wa Mungu aliyejifunza kila kitu kutoka kwa Baba yake anafafanua upya maana ya maarifa. Ni dhahiri kwamba Mwana wa Mungu si tu kwamba hakujua kila kitu lakini kwa kweli Hakujua chochote na Baba alimfundisha kila kitu.

Ndani ya Utatu hakuna picha ya wazi ya kusikiliza, kujifunza na kukua ndani ya Uungu. Kiini hasa cha maneno Baba na Mwana huzungumza kwetu kuhusu upendo, mwongozo na mtu wa kugeukia kwa ajili ya mafundisho. Ikiwa Mwana wa Mungu unayemwabudu hana uwezo huu katika utu Wake, basi unavutwa zaidi kuelekea wazo la kujua mambo na kuwa na majibu daima. Pia hudokeza kwamba

kuomba mwongozo ni udhaifu kwa sababu 'Mungu Mwana' hafanyi hivyo kwa sababu tayari anajua kila kitu. Tunapomfikiria Mwana ambaye hamhitaji Baba, si ajabu kwamba tunaona uhusiano wetu na Baba yetu wa mbinguni kuwa mgumu sana?

Nimesukumwa na upendo kushiriki nawe picha ya neno katika hatua hii. Ninapotafakari mambo haya, nasikia sauti ya minyororo mikubwa ikilegea na kisha kukatika-katika. Mzigo mkubwa juu ya mgongo wangu unashuka na niko huru, nikiwa huru dhidi ya ibada ya utumwa ya maarifa ambayo yanawasukuma wanadamu kujua-yote kwa sababu wanamwabudu 'Mungu Mwana' ambaye uungu wake hutambulikana na Yeye kuwa na maarifa ya kujua yote - ambaye hawawezi kujifunza lolote kutoka kwa Baba Yake.

Ikiwa Mwana wa Mungu anajua yote, basi hawezi kutupatia kielelezo cha mwanafunzi, isipokuwa kwa maisha yake hapa duniani. Hili limefichwa katika picha kubwa ya 'Mungu Mwana' ambaye anajua mambo yote na hakufundishwa chochote na mtu yeyote.

Katika Mwana pekee, tumeonyeshwa mbele yetu uhalisi wa thamani wa mwanafunzi mwaminifu ambaye anaongozwa na mkono wa ulinzi wa Baba Yake. Je, huwezi kusikia sauti ya uhuru katika maneno haya?

SURA YA 6

# KUTOKUFA, SHERIA YA MAADILI NA UHURU WA KUCHAGUA

Uelewa wetu wa uhusiano wa Mwana wa Mungu na Baba una athari ya moja kwa moja kwenye mtazamo wetu wa maarifa na umuhimu wake katika ulimwengu wa kiungu. Hili nalo huathiri ufahamu wetu kwa Mungu juu ya kufahamu mambo yajayo. Kipengele kingine ambacho pia huathiri ufahamu wetu juu ya ujuzi wa Mungu wa kujua mambo kabla, mapenzi yake kwetu, na hatima yetu, ni suala la kutokufa.

Ikiwa sisi ni watu wasioweza kufa, basi uhusiano wetu na Mungu na sheria yake ni tofauti kabisa kuliko ikiwa sisi ni watu wa kufa na tunamtegemea Mungu kila wakati kwa ajili maisha na pumzi. Nimechunguza matokeo ya swali hili kwa undani katika sura ya 2 ya kitabu cha Life Matters ambacho kinapatikana katika *fatheroflove.info.*

Nitajaribu kuchukua kidogo mawazo ya yale niliyoandika hapo awali katika kitabu cha "Life matters" na kukupa kiini cha jinsi imani yetu kuhusu nafsi ya mwanadamu inavyoathiri uelewa wetu wa utii kwa Mungu na uhuru wa kuchagua.

> "Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." (Mwanzo 3:4-5).

Shetani alianzisha wazo hilo kwa mwanadamu la kutokufa kiasilia. Aliwaambia wazazi wetu wa kwanza kwamba kufanya mambo bila kutegemea mapenzi ya Mungu hakungepelekea kwenye kifo bali kwa kweli kungewapelekea kwenye uhuru mkubwa zaidi. Neno la Mungu linatuambia huu ni uongo. Kumbuka hapo awali ambapo tumeona jinsi uhusiano wa Mungu na viumbe hai vyote ulivyo:

> Yeye [Mungu] ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote… kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu, kama vile baadhi ya washairi wenu walivyosema, Kwa maana sisi pia tu uzao wake. Matendo 17:25,28

Biblia inatuambia kwamba tunaishi ndani yake. Muda baada ya muda, Mungu hutupa pumzi. Tena, sambamba na mada hiyo hiyo:

> Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote, na katika yote na ndani yenu wote. Waefeso 4:6

Inasema kwamba Mungu yuko katika yote na ndani yenu wote. Maisha yetu yameunganishwa moja kwa moja na Baba yetu. Tunaishi kila wakati tukiwa tumeunganishwa kwa kina Naye. Hili ni kwa sababu Biblia inafundisha kwamba ni Mungu pekee asiyeweza kufa.

> Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kufa, asiyeonekana, Mungu pekee aliye na hekima, heshima na utukufu milele na milele. Amina. 1 Timotheo 1:17

> [Mungu] ambaye peke yake hapatikani na mauti… 1 Timotheo 6:16

> Kutokufa huku alimpa Mwanawe. Kwa maana kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake, vivyo hivyo amemjalia Mwana kuwa na uzima ndani yake. Yohana 5:26

Biblia inasema kwamba mwanadamu anakufa, si asiyeweza kufa.

> Je, mtu anayekufa anaweza kuwa na haki zaidi kuliko Mungu? Je, mtu anaweza kuwa msafi kuliko Muumba wake? Ayubu 4:17

Kwa hiyo, wanadamu wanatafuta kutokufa. Huwezi kutafuta kitu ambacho tayari unakimiliki.

> …utafuteni utukufu, heshima, na kutokufa.Warumi 2:7

Kwa nini Mungu alimpa Mwana kuwa na uzima ndani Yake? Yohana anatuambia kwa nini hili liko hivyo:

> "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile." Yohana 5:19

Mwana hawezi kufanya lolote bila ya Baba yake. Ameyakabidhi mapenzi yake kabisa kwa Baba milele.

> "Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi**, nami ni hai kwa Baba**; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi." Yohana 6:57

Mwana wa Mungu amechagua daima kuishi kwa Baba. Ndiyo maana anaitwa Amina. Chochote ambacho Baba yake anasema, Mwana anachagua kusema Amina.

> …**Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina**, Shahidi Mwaminifu na wa Kweli, Mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Ufunuo 3:14.

Kwa hiyo amepewa kuwa na uzima ndani Yake. Hiki si kitendo kisichokuwa na maana kwa upande wa Baba. Ni shauku kuu ya Baba kufanya hivi lakini inaweza kutolewa tu kwa moyo unaopokea. Baba alimimina zawadi Zake zote juu ya Mwanawe na Mwana alifurahi kuzipokea na kwa kuchagua daima kusimama na Baba Yake, Baba angeweza kuruhusu kwamba uzima Wake wa kutokufa daima uwe ndani ya Kristo.

> [**Mungu**] **yeye peke yake asiyeweza kufa**, anayekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, **ambaye hakuna mtu aliyemwona au awezaye kumwona**; Heshima na uweza una yeye hata milele Amina. 1 Timotheo 6:16

Baba peke yake ndiye asiyeweza kufa. Ni yeye pekee ambaye mwanadamu hajawahi kumwona. Mwana anapokea kutokufa katika muungano wa dhati na Baba Yake, kwa hiyo Mwana ana hali hiyo hiyo ya kutokufa. Uzima wa Baba unakaa ndani yake daima. Kwa hiyo, ndani ya Mwana wa Mungu kuna maisha asilia ya Baba.

Hili ni jambo muhimu sana la kufahamu. Ulimwengu wa Kikristo unafundisha kwamba Kristo ana hali ya kutokufa ndani yake ambayo hakuipokea kwa yeyote. Kutokufa kunaonyeshwa kama sifa aliyo nayo kiasilia. Lakini Biblia inaonyesha uzima kwa njia tofauti.

> "Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; **maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima."**Yohana 6:63

> "Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4

Mwanadamu anawezaje kuishi kwa kila neno la Mungu isipokuwa Kristo kutupatia kielelezo kitakatifu cha jinsi ya kufanya hivi?

> Mimi Mwenyewe siwezi kufanya lolote. Kama nisikiavyo, ndivyo nihukumuvyo… Yohana 5:30

Hii ndiyo sababu Yesu anaitwa Neno la Mungu. Hii ni kwa sababu Yeye anaishi kwa kila neno ambalo Baba yake anazungumza Naye na kisha Yeye hulifanya lijulikane.

> "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Yohana 1:1

Kinyume chake, kanuni ya imani ya Athanasian inawasilisha uzima wa milele wa Kristo kama wa kujitegemea lakini hapohapo kwa namna ya fumbo akiwa umoja na Baba.

> Baba asiyeumbwa; Mwana asiyeumbwa; na Roho Mtakatifu asiyeumbwa. Baba hana kikomo; Mwana hana kikomo; na Roho Mtakatifu hana kikomo. Baba wa milele; Mwana wa milele; na Roho Mtakatifu wa milele. Na bado wao si wa milele watatu; bali mmoja wa milele. - Excerpt from Athanasian Creed.

Imani hii haisemi kwamba Mwana ni wa milele kwa sababu ya uhusiano wake na Baba. Inasema kwa urahisi Yeye ni wa milele au hafi. Hii inafanya uzima wa milele wa Kristo kuwa kanuni inayojitegemea, asili inayothibitisha kuwa Yeye ni Mungu badala ya uzima wa milele uliopo kupitia upendo na imani aliyonayo kwa Baba yake.

Ni ibada hii ya uwongo ya Mwana wa Mungu ambayo inakuza wazo la kwamba mwanadamu ana hali ya kutokufa ndani yake pia, kwa maana kwa kutazama unabadilishwa kuwa sura ile ile.

Dhana hii ya uwongo ya kutokufa inabadilisha sana mtazamo wetu wa sheria ya Mungu na kusudi lake na maana katika maisha yetu. Kutokufa ndani yetu wenyewe kunamaanisha kwamba uwezo wa kuzalisha maisha yetu wenyewe uko ndani yetu wenyewe, na si kutoka kwa Mungu. Kwa maana nafsi ambayo huona kwamba nafsi yao haiwezi kufa (ama moja kwa moja au kwa njia ya ibada ya 'Mungu Mwana'), neno la Mungu kwao, kupitia sheria, hunena kwa sauti ya kulazimisha - inayowahitaji kunyenyekea na kufanya bila ukamilifu yale ambayo Mungu anawaamuru kutokana na uwezo wao wenyewe unaokaa ndani yao. Katika mfumo huu amri za Mungu zitachukuliwa kuwa ni zenye kuwalemea na kuudhi.

Kwa roho ambazo zinajua kwamba hazina kitu ndani yao na badala yake huishi dakika baada ya dakika kutokana na uhai ambao Mungu huwapa, sheria ya Mungu hunena tu kwa maneno ya ahadi. Si kubana hiari ya maisha ya asili ya mwanadamu, bali ni ahadi ya uzima kupitia utii wa hiari ya mwanadamu. Katika mfumo huu amri za Mungu zinachukuliwa kuwa za malezi ya mzazi na za kudumisha uhai.

Tofauti kati ya mawazo haya mawili ni kubwa. Fundisho la kutokufa kwa nafsi kwa asili hubadili mtazamo wa mwanadamu juu ya Neno la Mungu. Ni lazima ieleweke kama kikwazo juu yake, ambacho Mungu basi humpa thawabu ikiwa mtu atatii na kumwadhibu kama ataasi. Wazo hili husababisha kanuni za utii na hiari wa kuchagua kupingana, na kutengeneza kitendawili ambacho Ukristo unahangaika kukieleza. Mwanadamu anawezaje kuwa na uhiari wa kuchagua wakati Mungu anaweka juu ya mwanadamu sheria yake? Mwanadamu anawezaje kutumia hiari yake ya kuchagua wakati Mungu anawaadhibu wale wanaovunja sheria Yake? Je, hili linaweza kweli kuchukuliwa kuwa hiari ya kuchagua?

Mgogoro huu wote unatokana na uongo wa kutokufa kwa nafsi. Biblia inafundisha kwamba Mungu hawezi kufa na kwamba Kristo pekee ndiye anayeshikilia kutokufa huku katika milki yake kupitia uhusiano wake mkamilifu na Baba. Katika kuukubali ukweli huu, utakuwa na ufunguo unaofungua mgongano huu kati ya utii kwa sheria ya Mungu

na hiari ya kuchagua. Kukataa fundisho la nafsi isiyoweza kufa hubadilisha sheria ya Mungu kutoka kwenye sheria ya maagizo hadi sheria huru inayolinda ustawi wetu.

Katika muktadha huu Amri 10 zinakuwa unabii wa kile tunachokuwa tunapompenda Mungu na Mwanawe. Amri zitaandikwa mioyoni mwetu, si kwa matendo yetu yanayoongozwa na hali ya kutokufa, bali kwa Roho wa Kristo atendaye kazi ndani yetu, kutaka na kutenda kwa mapenzi yake mema.

Sababu ya kwanini swali hili kuwa muhimu sana ni kwa sababu ikiwa mtu ana mtazamo wa Mungu kulazimisha mapenzi yake kupitia sheria yake, basi uwezo wa Mungu kufahamu mambo kabla huwa adui wa uhuru wa kuchagua. Sheria iliyowekwa humfanya Mungu kama mtawala. Adhabu kwa sheria iliyowekwa humfanya Mungu kuwa dhalimu. Mungu dhalimu ajuaye yote ni jinamizi lisilochukulika.

Nafsi ya mwanadamu huitikiaje jinamizi kama hilo?

1. Hujaribu sana kumtuliza na kumfurahisha dhalimu huyu kwa matendo mema na humsihi asikuangamize.
2. Kutafuta kuiepuka hatma yako, kuishi maisha machungu matupu ya kutafuta kujiondoa kutoka kwenye hatima hiyo kabla ya kukabili adhabu.
3. Kuwa mtu asiyeamini kuwa kuna Mungu ili kujiondoa kutoka kwenye picha hii ya kutisha na utafute kuendesha maisha yako mwenyewe.

Gundua utambulisho wa kweli wa Yesu na usikilize kile Alichofundisha hasa kuhusu Baba Yake na uingie ufalme mpya Anaozungumzia.

Kwa muhtasari, fundisho la nafsi isiyoweza kufa hulazimisha Mungu aonekane kuwa mtawala na asiye na maana. Hii imekuwa nia ya Shetani wakati wote alipowadanganya Adamu na Hawa kuhusu chanzo cha maisha yao. Anataka kumwonyesha Mungu kama dhalimu ili kutufanya ikiwezekana kujaribu kumtuliza, kufanya ibada yetu ijikite katika msingi wa woga na sio upendo, au kumwangamiza, kwa kuacha kuamini kuwa yuko.

Tena, tunakumbushwa kwamba kujua ukweli wa utambulisho wa Yesu, Mwana wa Mungu, ndiyo njia pekee ya kumjua Baba. Kama tulivyojifunza katika sura ya 4, imani kwamba Kristo amezaliwa na Baba ni muhimu ili kubadili mitazamo yetu kuhusu jinsi Mungu anavyoyachukulia maarifa. Pili katika ukweli kwamba kutokufa kwa Mwana hutokana na uhusiano Wake na Baba, tunaweza kuachana na fundisho la giza la kutokufa kwa nafsi na kugundua kwamba kutokufa huja kupitia uhusiano wa kudumu na Mungu. Tunarudia maneno ya Yesu.

> "Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, **nami ni hai kwa Baba**; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi." Yohana 6:57

Tunaweza kuwa na uzoefu sawa na Yesu, kupitia kuishi ndani Yake, kama anavyoishi katika Baba yake. Kutokufa si suala la uwezo wa asili, bali ni suala la uhusiano kamili wa upendo.[15]

Hebu tufanye muhtasari wa mambo mawili muhimu ambayo yatakuwa msingi wa mjadala wetu kuanzia hatua hii kwenda mbele:

1. Katika ukweli kwamba Mungu alimzaa, alimkuza, na kumfundisha Mwanawe kila kitu anachojua, maarifa kamili hukoma kuwa sehemu muhimu ya uungu. Maarifa ya Mungu hayawezi kuhesabika wala kupimwa na mwanadamu.

2. Ukweli wa kwamba Mwana wa Mungu anaishi kwa uzima wa Baba yake humaanisha kwamba katika kumtazama Kristo tunaona kwamba uzima huja kupitia uhusiano na Baba. Kufikiri kwamba uhai ni uwezo wa asili ulio ndani yetu hutufanya tufikiri kwamba hatumhitaji Mungu kwa ajili ya uzima. Kuona kwamba Kristo anamtegemea Baba yake kwa uzima huturuhusu kukubali kwamba sisi pia tunaweza kumtegemea Mungu, bila kuhisi kudanganywa na kutawaliwa.

Sasa tuko tayari kuchunguza kisa cha mwanzo wa ulimwengu wetu kama kinavyofunuliwa katika Maandiko. Kabla hatujafanya hivi

---

[15] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na kanuni hizi tazama vitabu *Life Matters* na *Escaping the Pentagon of Lies* vinavyopatikana katika _fatheroflove.info_

nataka kuonyesha athari kwa vitendo ya kumwona Mungu kama anayelazimisha mapenzi yake juu yetu.

SURA YA 7

# NAFASI YA MAOMBI

Akiandika katika gazeti la *New York Times* miaka kadhaa iliyopita, kijana mmoja asiyeamini kwamba kuna Mungu alihimiza kisa chake katika makala yenye kichwa "Maombi hayafai na yana Mapungufu."

> Ingawa kusudi kuu la maombi linaweza kuwa kusaidia wengine, lakini hayafanyi hivyo kamwe. Maombi yanawanufaisha wale tu waumini wanaoyasema au kuyasikia. Maombi huwapa faraja. Yanawaruhusu kufikiria kuwa wana udhibiti fulani juu ya hali ambayo inaweza kuwa nje ya uwezo yao. Ni suluhisho la mwisho la watu ambao wameishiwa na mawazo, na njia ya kwanza ya watu ambao hawakuwahi kujisumbua kufikiria jinsi wanavyoweza kurekebisha tatizo linalo wakabili.
>
> Hili sio hatari. Kuna ubaya sana wa kuomba. Huwapelekea waumini katika hisia za uongo za kufanikiwa. Hatuwezi kutatua matatizo yetu – sembuse ya ulimwengu – kupitia maombi. Mara nyingi tunaona watu wenye nia njema wakiwaombea waliofikwa na msiba, lakini maombi hayafai bila matendo, na matendo hayo yanafanya maombi kutokuwa na umuhimu. kufafanua Robert Green Ingersoll mkuu, mikono inayosaidia ni bora zaidi kuliko midomo inayosali.[16]

Baada ya kufanya msukumo huu, mwandishi sasa anakamilisha kazi yake ya kumwangamiza Mungu ambaye alifundishwa habari zake.

---

[16] https://www.nytimes.com/roomfordebate/2013/06/27/should-atheists-pray/prayer-is-useless-and-has-a-downside

> Sina shida na "maombi" kama kitendo cha kutafakari. Kwa kweli, watu wengi wasioamini kuwa kuna Mungu wanaweza kukuambia faida ya kujitafakari kimya kimya. Udanganyifu hutokea unapofikiri mtu mwingine anasikia mawazo yako na kuyafanyia kazi.[17]

Sasa mwandishi anafichua mfumo wake wa msingi na sababu ya kwa nini amekataa wazo la Mungu.

> Inapokuja juu yake, maombi hayana mantiki, hata kwa maneno ya kidini. Ikiwa Mungu ana mpango, kwa nini ujaribu kuuzuia? Ikiwa Mungu anaweza kuongozwa na maombi, ni Mungu wa aina gani angeruhusu mambo ya kutisha tunayoona ulimwenguni?[18]

Hapa inafunuliwa sumu ya fundisho la Kikristo la kujua yote. Ikiwa Mungu ana mpango, kwa nini ujaribu kuuzuia? Hili ni swali la kiungwana sana katika kujibu madai ya Ukristo. Kumbuka kile ambacho wengi katika Ukristo wanafundisha juu ya jambo hili ambalo tulilichunguza katika sura ya 1?

> Mungu anajua yote (Zaburi 139:1–6), na anajua siku zijazo (Isaya 46:10). Kwa hiyo alijua hakika kwamba Adamu na Hawa wangetenda dhambi.[19]

Ikiwa unaamini hili basi ni vigumu sana kuepuka mstari wa pili wa hoja kutoka kwa mwandishi katika *New York Times.*

> Ikiwa Mungu anaweza kuongozwa na maombi, ni Mungu wa aina gani angeruhusu mambo ya kutisha tunayoona ulimwenguni?[20]

Mwandishi yuko sahihi. Hili halina mantiki, halina maana. Ikiwa Mungu alikuwa na mpango, basi hakuna kitu unaweza kufanya ili

---

[17] Ibid
[18] Ibid
[19] https://www.gotquestions.org/if-God-knew-Adam-Eve-sin.html
[20] https://www.nytimes.com/roomfordebate/2013/06/27/should-atheists-pray/prayer-is-useless-and-has-a-downside

kuubadilisha. Unapoutazama mpango huu wenye kutisha na vifo vyote vilivyomo, ni Mungu wa aina gani angepanga hili?

Inaweza kuonekana kwamba kwa njia fulani zile nafsi tatu za Utatu ni onyesho la miungu watatu wapangao hatima ya mambo.

> Nafsi zipangazo hatima zilitajwa kama wanawake watatu wazee sana ambao huzungusha nyuzi za hatima ya mwanadamu. Majina yao yalikuwa Clotho (Spinner), Lachesis (Allotter), na Atropos (Inflexible). Clotho alisokota "uzi" wa hatima ya mwanadamu, Lachesis akaisambaza, na Atropos akakata uzi (hivyo kuamua wakati wa kifo cha mtu huyo). Warumi walitambua Parcae, ambaye asili yake ni sifa ya kuzaliwa kwa mtoto, na Hatima tatu za Kigiriki. Miungu ya kike ya Kirumi iliitwa Nona, Dekuma, na Morta.[21]

Makanisa ya Kikristo kwa kawaida yangejitenga na msimamo huu katika juhudi zao za kudumisha fundisho la uhuru[22] lakini ni vigumu.

Mtu huyu anaeleza kwa ufasaha kutopatana kwa kimantiki kwa tatizo la mungu ajuaye yote, mwenye uwezo wote na maombi.

> Hata hivyo, kama matumizi ya mantiki rahisi yanavyoonyesha, sala yoyote inayomwomba Mungu jambo lolote haina maana. Je, sala itamwonyesha Mungu hitaji ambalo hakuwa akilifahamu hapo awali? Je, itamshawishi kufanya kitu ambacho hakuwa tayari kukifanya? Yote haya hayawezekani kwa Mungu ajuaye yote. Kinyume chake, ikiwa Mungu ni mjuzi wa yote, tayari anajua matamanio ya kila mtu bila kuhitaji kuambiwa. Vivyo hivyo, muda mrefu kabla ya muumini yeyote kuanza kumwomba Mungu achukue hatua fulani, akili yake isiyo na kikomo itakuwa imekwisha kufahamu kila sababu inayowezekana ya au dhidi ya kuchukua hatua hiyo, imeamua matokeo ya kufanya dhidi ya kutofanya na itapunguza athari zote zisizohesabika za kila uamuzi, na hatimaye kujikita juu ya uamuzi kwamba anajua kilicho bora ili kufikia malengo yake. Je, wasioamini kuna Mungu, kwa kujiamini kuwa ni wadogo na wasio na maana kulinganishwa na Mwenyezi, wanatumai basi kubadili mawazo

[21] https://www.britannica.com/topic/Fate-Greek-and-Roman-mythology
[22] https://www.newadvent.org/cathen/06259a.htm#anc

yake? Je, wanatumaini kugeuza mipangilio ya kimungu kwa mnong'ono wa dua yao? Ombi kwa Mungu la kumtaka afanye jambo ambalo tayari alikuwa anaenda kulifanya halina maana kabisa; maombi ya kumtaka Mungu kufanya jambo ambalo hakuwa tayari kulifanya ni bure.

Njia pekee ya aina hii ya maombi ingeweza kufanya kazi, ikiwa Mungu angeamua kwamba angefanya jambo fulani ikiwa tu idadi ya kutosha ya watu ingeliomba ili afanye hivyo. Lakini hili linasema nini kuhusu tabia yake? Je, humwongelea Mungu kwamba, angeona uhitaji wa tendo fulani na kujua kwamba lingekuwa na matokeo mazuri ikiwa angelifanya, lakini bado angeshindwa kuchukua hatua isipokuwa kama aliombwa kufanya hivyo? Mtu mungwana mwenye maadili, akigundua hitaji la mwingine, sio lazima aombwe kusaidia.

Zaidi ya hayo, ikiwa mafundisho ya dini nyingi ni ya kweli, Mungu hangejibu kamwe maombi yoyote ambayo yanaathiri au kuathiri mwanadamu mwingine kwa njia yoyote - kama vile maombi yale yanayoombwa na wasioamini kuna Mungu (theists) ili Mungu awaongoze wasioamini kama mimi. Ikiwa Mungu alituumba tukiwa na uhuru wa kuchagua kwa sababu anataka tujichagulie wenyewe, ili yeye aingilie kati, kupindua chaguo huru la mtu na kubadili mwelekeo wa maisha yake kwa kulazimisha tendo fulani au hali fulani ya kiakili itakuwa ukiukaji wa mpango wake mwenyewe. Kinyume chake, katika ulimwengu wote ambapo kuna mambo yaliyokwisha kupangwa, Mungu atakuwa tayari amepanga maisha ya kila mtu kabla ya wakati, kwa hiyo tena, jitihada za kubadili mwendo wa matukio kupitia sala zitakuwa bure.

Na hatimaye, je, si kwa njia ya kiburi kwa asiyeamini kuna Mungu kumwomba Mungu kuchukua hatua fulani? Je, si madai ya kwamba wanajua vizuri zaidi kuliko yeye jinsi mambo yanavyopaswa kuwa? Kwani, ikiwa Mungu ni mjuzi wa yote na ni muweza wa yote, hakuna kinachoweza kutokea ikiwa hataki jambo hilo litokee. Hakuna kinachoweza kutokea kinyume na mapenzi yake. Kwa hiyo, hali yoyote ya mambo ambayo asiyeamini kuna Mungu anataka kuyabadili kwa njia ya maombi

> lazima yawe mapenzi ya Mungu, na kwa kutafuta kuyabadilisha, kimsingi wanasema kwamba kile ambacho Mungu amekifanya tayari si kizuri vya kutosha, au ni makosa ya wazi kabisa.23

Aina hizi za hoja zinazosimamiwa na watu kama vile Richard Dawkins na Christopher Hitchens[24] zinapokelewa kwa urahisi na Kizazi Z, kizazi cha hivi punde sasa katika ujana wao. Katika idadi ya vijana wa sasa, mwelekeo wa Kuamini kuwa hakuna Mungu ni mara mbili ya kizazi kilichopita.[25]

Nimefanya kazi kama mchungaji kwa karibu miaka 30 na mara nyingi nimekutana na swali kutoka kwa watu. "Kuna maana gani ya kuomba? Mungu tayari anajua kila kitu na ameamua kila kitu." Haya ni matunda ya kuamini kwamba Mungu huweka mapenzi yake ya kujua yote juu ya viumbe vyake. Biblia inatuambia jambo tofauti.

> "Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote;" 2 Wakorintho 5:14

Upendo humsukuma mtu kutoka ndani. Ni kitendo cha hiari ambacho hakihitaji vitisho, nguvu au adhabu. Yesu aliomba kwa Baba yake kwa sababu alimpenda. Ilimpa furaha kubwa kuwa naye.

Picha ya maombi tuliyopewa na Mwana wa Mungu alipokuwa duniani ni upanuzi wa asili wa uhusiano wa kweli ambao aliudumisha na Mungu tangu mwanzo. Kama tulivyogundua katika sura ya 5, Mwana wa Mungu alipendwa, alilelewa, alifunzwa na kubarikiwa na Baba Yake. Alipewa kuwa na uzima kutoka kwa Baba yake. Huu ndio muktadha unaoleta maana ya maombi.

Uwasilishaji wa Kristo kama mungu anayejitosheleza mwenye uwezo wote, anayejua yote hufanya maombi yaonekane kama mchezo wa kuigiza. Huenda ikasemwa kwamba Yeye anatuonyesha jambo fulani kwa manufaa yetu, lakini faida hii inapotea tunapoona kwamba Yeye Mwenyewe haihitaji.

---

[23] https://www.patheos.com/blogs/daylightatheism/essays/nothing-fails-like-prayer/

[24] https://en.wikipedia.org/wiki/New_Atheism

[25] https://www.impact360institute.org/articles/atheism-rise-generation-z/

> “Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu.” Luka 6:12

Moja ya mambo ya kuvutia sana tunayoona katika maisha ya Kristo duniani ni ufunuo wa jinsi Mwana wa Mungu daima anavyohusiana na Baba yake.

1. Asili ya utegemezi wake kwa Baba. Yohana 5:19
2. Uhitaji wake wa baraka na upendo wa Baba yake. Mathayo 3:17
3. Ibada yake kwa Baba yake. Yohana 4:22; Yohana 20:17
4. Shukrani yake kwa Baba yake. Yohana 11:41

Picha hii ya uhusiano wa Kristo na Baba yake inapanuliwa sana wakati Yesu alipowaambia wanafunzi wake kwamba Zaburi nyingi zilikuwa ufunuo wake na jinsi anavyohusiana na Baba yake.

> Kisha akawaambia, “Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.” Luka 24:44

Tunaona kanuni hii katika maeneo kama haya.

> “Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha? Mbona U mbali na wokovu wangu, Na maneno ya kuugua kwangu?” Zaburi 22:1

> “Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Mathayo 27:46

Msikilize Mwana wa Mungu akijieleza katika maombi katika sehemu iliyosalia ya Zaburi hii.

> “Usiwe mbali nami maana taabu i karibu, Kwa maana hakuna msaidizi. Mafahali wengi wamenizunguka, Walio hodari wa Bashani wamenisonga; Wananifumbulia vinywa vyao, Kama simba apapuraye na kunguruma. Nimemwagika kama maji, Mifupa yangu yote imeteguka, Moyo wangu umekuwa kama nta, Na kuyeyuka ndani ya mtima wangu. Nguvu zangu zimekauka kama gae, Ulimi wangu waambatana na taya zangu; Unaniweka katika mavumbi ya mauti Kwa maana mbwa wamenizunguka;

> Kusanyiko la waovu wamenisonga; Wamenizua mikono na miguu. Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; Wao wananitazama na kunikodolea macho. Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura. Nawe, BWANA, usiwe mbali, Ee Nguvu zangu, fanya haraka kunisaidia. Uniponye nafsi yangu na upanga, Mpenzi wangu na nguvu za mbwa. Kinywani mwa simba uniokoe; Naam, toka pembe za nyati umenijibu. Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu, Katikati ya kusanyiko nitakusifu. Ninyi mnaomcha BWANA, msifuni, Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo, mtukuzeni, Mcheni, enyi nyote mlio wazao wa Israeli." Zaburi 22:11-23

Ni thamani iliyoje kuweza kutazama mazungumzo ya kina ya Mwana wa Mungu kwa Baba yake. Ukweli wa ndani zaidi ni kwamba tukio lililoelezewa hapo juu katika Zaburi lilikuwa halisi kwa Mwana wa Mungu katika siku za Daudi kama vile alipokuwa hapa duniani. Kwa Jinsi gani?

> **"Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa;** kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale." Isaya 63:9

> "Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Mathayo 25:40

> …Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na **Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao,** ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo. 1 Petro 1:11

Mwana mpendwa aliyelelewa, kukuzwa na kufunzwa na Baba yake mpendwa daima humwendea Yeye, katika hali zote nzuri na mbaya. Akiwa amevikwa ubinadamu, akitembea katika ulimwengu huu wenye giza, Yeye daima anamwendea Baba Yake na kumwomba ambariki, amwinue na kumsaidia. Anafanya hivyo kwa sababu Baba ndiye chanzo cha vitu vyote. (1 Wakorintho 8:6). Ni roho hii ya maombezi na utegemezi wa Mwana wa Mungu ambayo inashikilia ulimwengu wote pamoja. (Wakolosai 1:17).

> "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba." Wagalatia 4:6

Abba ni neno la mapenzi; ni kama kusema "baba" kwa ajili yetu. Ikiwa Mungu pekee ndiye asiyeweza kufa, basi Mwana wa Mungu lazima awe na serikali mabegani mwake kupitia kuendelea kumwendea Baba na kumtegemea kwa ajili ya uhai, pumzi na vitu vyote. Huku kumwendea na kudumisha ukaribu na Baba yake ndiko yesu huupatia kila kiumbe aliyeumbwa. Uumbaji unamjua Mungu wake kupitia Kristo.

Kama tutakavyoeleza zaidi katika sura inayofuata, Shetani alitaka kuishi bila kutegemea roho ya utegemezi ya Mwana wa Mungu. Alitamani kujitegemea. Alitamani kuwa Mungu Wake mwenyewe. Adamu alikumbatia kanuni za Shetani hapo mwanzo na kuweka jamii ya wanadamu kwenye njia ya dhambi kwa njia ya kuamini uongo kwamba "hakika hamtakufa." Hili lilimfanya mwanadamu wa asili kumwona Mungu kama adui (Warumi 8:7); Hili husababisha shida hii:

> Hakuna aliye na hekima kweli; hakuna amtafutaye Mungu. Warumi 3:11 (NLT)

Kristo ndiye hekima ya Mungu kwa sababu Yeye ndiye pekee ambaye daima anamtafuta Baba, kwa kina akiwa na upendo Naye na kutamani kuwa pamoja Naye. Tunapomkataa Kristo, basi tunaacha kumtafuta Mungu, kwa kuwa Kristo ndiye pekee anayemtafuta na ndiye pekee anayemjua.

Hili ndilo jambo la msingi: Maombi yanaonekana yakukanganya kupitia mwonekano wa 'Mungu Mwana' mwenye kufahamu yote, mwenye uwezo wote ambaye usawa wake na Baba yake hutokana na yeye kuwa na uelewa na nguvu sawa na Baba yake. Maombi hupata upatanifu na mantiki yake kupitia mwonekano wa Mwana wa Mungu, ambaye alilelewa kwa upole na Baba yake na kuongezeka kimo na hekima na kupendwa na Baba yake.

SURA YA 8

# HURU KWELI KWELI

Muhtasari hadi sasa: Unapojua utambulisho wa kweli wa Mwana wa Mungu, unaingia katika nyanja ya ufahamu ambayo hukuweka huru dhidi ya chochote kilichohusianishwa na nguvu, udhibiti au kulazimisha. Yesu alituambia:

> "Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa sikuzote. **Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli**. Yohana 8:35-36 (KJV)
>
> Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; **mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.** Yohana 10:10 (KJV)

Ukweli wa Mwana wa Mungu ni kwamba Baba yake alimzaa, akamfundisha kila kitu na kumpa kila kitu. Mwana wa Mungu, kutokana na uhuru wake mwenyewe wa kuchagua , anamtumikia Baba Yake si kama mtumwa bali kama Mwana Wake.

> "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, **wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.**" Wagalatia 4:6-7

Neno la Kigiriki lililotumika kama "huru" katika "Basi Mwana akiwaweka huru" (Yohana 8:36) humanisha:

> G1658 asiyezuiliwa (kuenenda kwa starehe), yaani, (kama raia) si mtumwa (iwe ni mzaliwa huru au asiyefungwa), au (kwa ujumla)

ametengwa (kutoka kwenye wajibu au dhima): - (mwanamume, mwanamke) huru, kwa uhuru.

Mwana wa Mungu hazuiliwi kabisa si kwa sababu ana asili ya kujua yote na uwezo wote. Hana kizuizi na yuko huru kwa sababu Baba ni *pendo*[26]; Baba hutoa bure bila uhitaji, bila nguvu na bila udhibiti.

Hii ndiyo sababu Mwana wa Mungu anaweza kusema:

> "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; **Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba,** huyu ndiye aliyemfunua." Yohana 1:18.

Mwana wa Mungu hahitaji kupima akili na uwezo wake dhidi ya ule wa Baba yake, kwa maana Baba ndiye aliyempa vitu hivi vyote bure. Cha kusikitisha ni kwamba, wengi bila kujua wanaamini kwamba usawa ambao Yesu hakuona kuwa ni kitu cha kushikamana nacho ulikuwa ule usawa wa uwezo, akili na enzi ya milele. Kile ambacho watu wengi hushindwa kutambua ni mfumo tunaompima Mwana wa Mungu kwa kweli huwa mkuu kuliko mtu Mwenyewe.

Hii ndiyo sababu Wakristo wachache sana wa kawaida wanaamini kwamba Yesu ni Mwana wa kweli wa Mungu. Ukristo unaamini kwamba Kristo hata sasa yuko katika mchakato wa kuzaliwa au kwamba hajazaliwa kabisa katika umilele. Hili huangamiza ukweli kwamba Kristo amezaliwa na Baba kweli.

Utambulisho wa Mwana wa Mungu unapatikana katika jina - Mwana. Yeye ni Mwana wa Baba katika ukweli na upendo. Thamani yake kama mtu binafsi haitegemei kipengele chochote cha nje. Haitokani na nguvu, akili au ubora fulani wa asili. Ni thamani ambayo amepewa wakati Alipozaliwa katika umilele na ambayo haiwezi kamwe kuondolewa.

> "Wana wa wana ndio taji ya wazee, **Na utukufu wa watoto ni baba zao**." Mithali 17:6

Yesu anatufunulia mahali ambapo thamani yetu inatoka kama ifuatavyo:

---

[26] Neno la kigiriki la upendo uliojaa wema

> “Je! Mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. **Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi**.” Luka 12:6-7

Thamani yetu kama watoto wa Mungu haipatikani katika uwezo wetu; hupatikana katika mawazo ambayo Baba yetu anatuwazia. Thamani yetu inatoka kwa Baba na sio kutoka kwetu sisi wenyewe. Hili ni kweli kwa Kristo kwanza, na sisi tunaomwamini sote tuko katika nyanja hiyo.

> “Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.” Warumi 8:29

Sikiliza neno la Mungu uone ni wapi tunapata utukufu na thamani.

> “BWANA asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA,” Yeremia 9:23-24

Hivi ndivyo Kristo anavyoishi. Anaishi kwa neno la Baba yake. Anajitukuza kwa Baba yake na kupata thamani yake kwa Baba yake na si ndani yake mwenyewe. Huu ndio mwamba ambao juu yake Kanisa la Mungu limejengwa. Ni ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu aliye hai. Kristo ni Mungu, si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho wa Baba yake.[27]

Usisahau kwamba Mwana wa Mungu ana nguvu zote za Baba Yake na amefundishwa mambo yote anayojua. Lakini hakuna hata moja ya mambo haya yanayofafanua thamani ya Mwana wa Mungu, wala hayawezi kutumiwa kuthibitisha usawa wa Mwana na Baba. Kufanya vipimo hivyo husababisha utumwa. Huwezi kupata pumziko kifuani mwa yule unayejilinganisha naye kwa nguvu na akili.

---

[27] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na hili tazama kitabu *Identity Wars* katika fatheroflove.info

Hili ndilo jambo zuri zaidi kuhusu ibada ya Mwana wa Mungu.

Katika kumtazama Yeye, unaweza kuwa huru kutokana na hitaji la kujithibitisha kwa akili yako, nguvu, na sifa nyingine zozote unazoweza kudai kuwa nazo.

Mwana halisi wa Mungu anakufanya uwe huru kabisa kutojilinganisha tena au kushindana na kitu kingine chochote katika uumbaji wa Mungu. Inatuweka huru kutoa kwenye kiburi chetu. Inatuzuia tusihisi haja ya "kuwa kama miungu." (Mwanzo 3:5, KJV). Haya yote ni kwa sababu ndivyo yalivyo kwa Mwana wa Mungu. Thamani yake iko kwa Baba Yake pekee, si ndani Yake Mwenyewe.

Uhuru huu wote unatolewa kwetu kwa njia ya Roho aliye ndani ya Kristo Yesu. Unapomjua na kumpenda, basi utapata uzoefu wa uhuru ulio sawa na Yeye.

> "Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:12

Utambulisho wa kweli wa Mwana wa Mungu unaonyesha kwamba Mungu mmoja wa kweli alimpa Mwanawe uhuru kamili, bila kizuizi na woga. Hakuweka juu yake kanuni za kisheria za kufuata, bali aliandika juu ya moyo wa Mwanawe tabia yake ya upendo, uhuru na furaha - sheria ya uzima.

Ni vigumu sana kwa moyo wa mwanadamu kufahamu jambo hili. Ni njia ya mlango mwembamba ambao ni wachache katika ulimwengu huu watakaoupata. Walakini ni rahisi sana kuelewa. Unaalikwa mahali pa siri pa Aliye Juu Zaidi; unakaribishwa katika kifua cha Baba. Acha Roho wa Mwana wa Mungu akujaze na kukuweka huru kutokana na kulinganishwa, woga, hasira na huzuni ambayo inatokana na kujaribu kupata thamani ya asili ndani yako. Toka kwenye ngome ambayo Shetani aliiumba na utembee kwenye nuru.

SURA YA 9

# NGOME YA LUSIFA

Biblia iko wazi sana kuhusu ni nani aliyeumba vitu vyote.

> "Vyote vilifanyika kwa huyo; [Yesu] wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.." Yohana 1:3

Mwana, akiwa amelelewa na Baba Yake na kupewa kila kitu, pamoja na uhuru kamili wa kufanya maamuzi, alikuwa na vitu vyote vilivyohitajiwa ili kuumba ulimwengu. Sifa za shukrani kwa Baba, hisia ya kuendelea kumtegemea Baba, na furaha na uhuru uliokuwa ndani ya Mwana, vilikuwa muunganiko kamili wa kuumba ulimwengu.

Lusifa, mbeba nuru, alikuwa kiumbe wa kwanza wa Baba na Mwana. Alikuwa wa pili kwa heshima baada ya Kristo. Upendo wote, furaha, baraka na uhuru ambao Baba alimpa Mwanawe ulitolewa kwa Lusifa kwa namna hiyo hiyo. Mwana wa Mungu hakuweza kuumba chochote ila kile Alichokuwa ameonyeshwa na kuwa na uzoefu nacho Mwenyewe. Lusifa alikuwa mzuri, kiumbe mkuu. Kama vile Baba alivyompa Kristo vyote, Mwana alitoa yote anayoweza kwa kiumbe aliyeumbwa. Mbingu yote ilikuwa pale kwa ajili ya Lusifa kufurahia.

> "Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako." Ezekieli 28:14-15

Yote haya yalitegemea sharti moja rahisi. Kumbuka kwamba wewe ni mwana wa Aliye Juu kupitia Mwana wake wa pekee. Alihitaji tu maneno haya yaandikwe moyoni Mwake.

> …"lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo." 1 Wakorintho 8:6

Kama Lusifa angalikumbuka hili, basi kama vile ambavyo Mwana wa Mungu alivyokuwa mng'ao wa utukufu wa Baba, ndivyo ambavyo Lusifa angekuwa mng'ao wa utukufu wa Mwana. (Waebrania 1:3).

Baba alikuwa amefanya kila mpango ili kuuongoza ulimwengu katika mwelekeo wa nuru na ukweli. Kujitolea hatarishi kwa Baba katika kumpa Mwanawe uhuru kamili wa kuchagua bila kizuizi kulikuwa kumefanikiwa. Mwana alikuwa ameamua kwa uthabiti:

> "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:8

Lusifa alimiminiwa upendo wa Mwana wa Mungu. Ushirika ambao Baba alishiriki pamoja na Mwanawe ulifika hadi kwa Lusifa. Lusifa angeweza kusema hapo mwanzo:

> "....na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo." 1 Yohana 1:3

Licha ya faida zote ambazo Lusifa alipewa, tunasoma:

> "Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama." Ezekieli 28:17

Kila kitu ambacho Mwana wa Mungu alikuwa amempa Lusifa kilikuja kuchukuliwa kama cha kwake binafsi. Alianza kutazama mwangaza na fahari yake kama inayotoka kwake mwenyewe. Njia pekee ambayo angeweza kujiruhusu kuamini kwamba mambo haya yametoka kwake mwenyewe ilikuwa ni kukataa uwana aliokuwa nao kwa Mwana wa Mungu.

Lusifa polepole akawa malaika aliyejitukuza katika hekima na uwezo wake badala ya kupata utukufu katika ufahamu na kumjua Baba yake na kutulia kifuani mwa Mwana wa Mungu alipopumzika na Baba yake.

Kutengwa kwa Lusifa kulikuwa kubaya sana kiasi kwamba alipanga njama ya kumuua Mwana wa Mungu.

> "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. **Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake.** Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo." Yohana 8:44

Kubadilika kwa Lusifa kwenda kuwa Shetani kunarudiwa katika kisa cha Kaini na Habili. Kaini alikuwa wa yule mwovu (1 Yohana 3:12), ikimaanisha kwamba alionyesha kanuni za Shetani kuhusiana na ndugu yake Abeli. Baada ya Kaini kumuua kaka yake, alijikuta katika ngome ya mahangaiko ya kihisia.

> "utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani." Mwanzo 4:12

Shetani akawa mkimbizi akitafuta kimbilio katika uongo. Neno la Kiebrania linalomaanisha mkimbizi lina maana ya mtu anayeyumba-yumba na kutikisika. Kwa nini hili lingetokea kwake? Katika maneno ya mfalme wa kwanza wa Babeli tunapata mwangwi wa mawazo ya Shetani.

> Mfalme akanena, akasema, "Mji huu sio Babeli mkubwa nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu, ili uwe utukufu wa enzi yangu?" Danieli 4:30

Shetani aliamua kuutoa uwana wake kwa Mungu kwa ajili ya jambo ambalo alihisi lilikuwa jambo bora zaidi. Alichagua kupuuza kwamba vyote vilivyokuwa vyake alipewa. Alianza kwanza kutafuta nafasi ya Mwana wa Mungu. Hatimaye, hili lilimpelekea kutamani cheo cha Mungu Mwenyewe.

> "Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu." Isaya 14:14

Lusifa, ambaye sasa ni Shetani, aligundua ya kwamba baada kukataa utambulisho wake kama mwana wa Mungu kwamba sasa alikuwa amejawa na hisia za mfadhaiko zilizomfanya atetemeke.

Kabla ya mabadiliko haya ya upendo kutoka kwa Mwana wa Mungu hadi kwake mwenyewe, ikiwa mtu angemuliza Lusifa wewe ni nani, angeweza kujibu – "Mimi ni mwana wa Mungu kupitia Kristo Mwana pekee." Baada ya kujikita katika kujitafutia utukufu na heshima zote, angewezaje kujibu swali hili? Angeweza tu kutaja mambo ambayo yalikuwa yamemjaribu kwanza kumsahau Yule aliyembariki.

Alionyesha fahari, mwangaza, na hekima yake kuwa msingi wa thamani yake. Hili liliunda misingi ya ngome yake mwenyewe. Hangeweza kamwe kuepuka hisia kwamba hakuwa mzuri vya kutosha. Alikuwa na msukumo wa mara kwa mara ambao alipaswa kujithibitisha na kuonyesha ujuzi wake ili kuizima sauti ya Roho wa Mungu ambayo ilikuwa inamwita arudi kwenye utambulisho wake wa kweli. Maneno haya yanasisitizwa katika moyo wa Shetani ndani ya gereza lake mwenyewe.

Tumia muda wako wote kusubiri nafasi hiyo ya pili
Kwa mapumziko ambayo yangefanya iwe sawa
Daima kuna sababu fulani ya kujisikia si mwema vya kutosha
Na ni ngumu mwisho wa siku
Ninahitaji usumbufu fulani. Oh, toleo zuri
Kumbukumbu hutoka kwenye mishipa yangu
Acha niwe mtupu. Oh, na uzito na labda
Nitapata amani usiku wa leo

Nimechoshwa na mstari wa moja kwa moja, na kila mahali unapogeuka
Kuna tai na wezi nyuma yako
Dhoruba inaendelea kupotosha, unaendelea kujenga uongo
Kwamba unafidia yale yote unayokosa
Haileti tofauti yoyote, kutoroka mara ya mwisho
Ni rahisi kuamini wazimu huu mtamu

Oh, huzuni hii tukufu inayonipelekea kupiga magoti.[28]

Katika juhudi zake za ujanja za kupindua na kuharibu jamii ya wanadamu, Shetani amebuni mtandao wa uongo kwa kutumia maneno, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ili kuwatia wanadamu katika ngome ile ile anayoishi. Akiwa amewajaza watu roho yake, anahimiza wao kufikiria kwamba Kristo hakuona kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho kwa sababu ya uwezo wake wa asili, fahari na hekima. Hata hivyo, hivi ndivyo hasa alivyofanya kwa fundisho la Mwana wa Mungu. Mfumo wa thamani ulioanzishwa na Lusifa wa kupata thamani kutokana na sifa zako za asili, aliuonyesha kuwa ni wa Mungu kupitia fundisho la Utatu. Mfumo wa thamani ambao fundisho hili linaunga mkono una nyenzo zile zile zilizojenga ngome ambayo Shetani anashikiliwa ndani yake.

Kama mtume Yohana, ninastaajabishwa sana na mfumo huu ambao Shetani aliusitawisha ili kuwavuta wanadamu kwake. Ikiwa Utatu utainuliwa, Shetani anaweza kuwa na uhakika wa kuwavuta karibu wote kwake. Fundisho hili, pamoja na fundisho la kutokufa kwa nafsi limefanyiza sehemu kubwa ya kazi kuu ya udanganyifu ambayo Shetani ameukuza ili kuhakikisha ulimwengu wote uko mikononi mwake.

Mkakati wa Lusifa wa kuwafanya wanadamu wageuze mtazamo wao kutoka kwenye urithi wao wa kweli kutoka kwa Mungu hadi kwenye nguvu ya uongo inayokaa ndani yao unafichuliwa katika majaribu yake kwa Kristo.

> Mjaribu akamjia akamwambia, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.” Mathayo 4:3

Shetani alitaka Kristo atetee utambulisho Wake kupitia onyesho la nguvu za kimiujiza. Wakati wa jaribu hili ni muhimu, kwa maana maneno ya mwisho yaliyoandikwa aliyoambiwa Yesu yalitoka kwa Baba Yake siku 40 kabla.

---

[28] Sarah McLachlan, Angel from the album City of Angels, November 1998

> Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye." Mathayo 3:17

Ikiwa Kristo angeanguka kwenye jaribu hili ili kudhihirisha Uwana Wake kwa njia ya onyesho la nguvu, ingedhihirisha mashaka juu ya kile ambacho Baba yake alikuwa amemwambia tayari. Huu ndio uhuru unaopatikana katika kulikubali Neno la Baba. Sio lazima uthibitishe chochote kwa wale wanaokupa changamoto. Unapumzika na kutulia katika Neno la Baba juu yako. Yeye ndiye anayefafanua utambulisho wako badala ya wewe kujielezea mwenyewe. Hiki ndicho kiini cha vita ya utambulisho.

Mwana mzuri wa Mungu anafunua jinsi ya kukabiliana na changamoto hizi:

> "Naye akajibu akasema, "Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4

Yesu anashinda vita hii ya utambulisho kwa kutegemea Neno la Baba yake. Hana haja ya kuhangaika kuthibitisha Yeye ni nani. Kwa upande mwingine, Shetani anahitajika daima kuthibitisha yeye ni nani kwa yale anayofanya na yale anayodai kuwa anayo. Alibadilisha utambulisho wake kama mwana wa Mungu kwa utambulisho kupitia hekima ya kibinafsi, utukufu, na nguvu. Lakini badiliko hilo lilimletea huzuni, utupu, ukosefu wa usalama, jeuri, na hasira.

> "Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi;......"Ezekieli 28:16

> "**Joka akamkasirikia** yule mwanamke**, akaenda zake afanye vita** juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari." Ufunuo wa Yohana 12:17

Ni kutoka ndani ya ngome hii ambapo mfumo wa thamani unaojumuishwa katika mafundisho ya kujua yote, uweza wa yote, na kuwepo tokea milele, ukiunganishwa pamoja ili kumruhusu Shetani kuwasilisha sifa zake kuwa ni za Mungu. Shetani alisema, kwamba angeinua kiti chake cha enzi, na katika mafundisho haya

yaliyochafuliwa kupitia mfumo wa thamani wa mtazamo wa nguvu asilia, Shetani anafanikisha malengo yake.

Ni kupitia fundisho la Utatu kwamba ulimwengu wa Kikristo unaunganishwa na wafalme wa dunia na utakuwa na nia moja na mnyama na watamsujudia yule joka.

> "Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?....Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia." Ufunuo 13:4,8

Kitabu cha Uzima kinaweza tu kuwajumuisha wale wanaomwabudu Mwana pekee wa Mungu.

> "Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima." 1 Yohana 5:12

Ibada ya Mwana wa Mungu ni ibada kwa yule ambaye anakaa kabisa katika upendo wa Baba kwa ajili ya utambulisho Wake. Huu ni uzima wa milele. Hii ndiyo sababu Kristo ndiye njia, ukweli na uzima wa Baba. Kinyume chake, ibada ya 'Mungu Mwana' ni ibada ya mtu ambaye anatambuliwa kwa nguvu za asili, hekima na uwezo vitokanavyo na yeye mwenyewe. Hii ndiyo ibada ya joka na mnyama anayemtawala.

Ikiwa umetambua kanuni hizi mpaka hatua hii, basi tuko tayari kuchunguza nyanja ya upendo wa kiungu wa kujihatarisha, upendo wa kweli wa Agape.

SURA YA 10

# KANUNI YA MBEGU

> “nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na **kati ya uzao wako** na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.” Mwanzo 3:15

> “Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo.” Wagalatia 3:16

Biblia hutaja uzao wa aina mbili, ambao wote uko kamili na uko tayari kutoa mavuno. Mwana wa Mungu na Shetani wote wana uzao. Uzao wa Mwana wa Mungu umekita mizizi katika maneno haya:

> “Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu. Nimehubiri habari za haki katika kusanyiko kubwa. Sikuizuia midomo yangu; Ee BWANA, unajua. Sikusitiri haki yako moyoni mwangu; Nimetangaza uaminifu wako na wokovu wako. Sikuficha fadhili zako wala kweli yako Katika kusanyiko kubwa.” Zaburi 40:8-10

> “Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Mathayo 4:4

Uzao wa Shetani uko kinyume na hili. Uzao wake unadharau sheria ya Mungu na kutafuta kutangaza haki yake mwenyewe kama alivyoifafanua. Uzao wa Shetani unatafuta kuishi kwa mkate tu bila neno la Mungu. Uzao huu wa uasi unajidhihirisha kwa njia hii.

> "Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake;" 2 Wathesalonike 2:7-8

> "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo." Yohana 8:44

Lusifa aliendehsa mipango yake kwa usiri kabisa. Kwa ujuzi wake wote, inaonekana kwamba hakuwazia kwamba Mungu na Mwana Wake wangeweza kusoma mawazo yake. Maandiko yanatuambia juu ya uwezo wa Mungu kusoma mawazo na makusudi ya moyo.

> "Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Waebrania 4:12

Usemi 'neno la Mungu' bila shaka pia linarejelea Kristo. Akiwa duniani, Alionyesha uwezo huu wa kusoma mioyo ya wanadamu.

> "Na Yesu alijua hoja zao, akajibu akawaambia, Mnahojiana nini mioyoni mwenu?" Luka 5:22

Akizungumza katika Zaburi tunaambiwa pia:

> "Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea mbali." Zaburi 139:2

Baba na Mwanawe walisoma mawazo ya Lusifa. Walikuwa wanajua kabisa mawazo yake. Katika Roho, walisikia kila mazungumzo ambayo Lusifa alikuwa nayo na malaika. Walishuhudia mashaka ambayo alikuwa akiyaweka katika akili za malaika. Kwa huzuni Walishuhudia hisia ambazo Lusifa alikuwa anazikuza na shauku yake ya kumuua Mwana wa Mungu.

Mambo haya yote yalifichwa kwa malaika. Hawakujua Shetani alikuwa akiwaza nini. Iwapo Baba na Mwana wangemkabili Lusifa kabla ya malaika kutambua kulikuwa na tatizo, Lusifa angeweza kupata ushawishi kutoka kwa malaika na kuendeleza mpango wake kwa urahisi zaidi wa kumwonyesha Mungu kama mwenye kulaani na kutawala kimabavu.

Tuliona hapo awali kwamba Roho anayeshuka kutoka kwa Mwana wa Mungu ni wa uhuru. Hana kizuizi. (Yohana 8:32,36). Sharti lake pekee ni upendo. (2 Wakorintho 5:14). Lusifa aliwezeshwa kuishi ndani ya mfumo huu bila kuzuiliwa kabisa. Tunaliona hili kwa sababu roho ya uhuru ndani ya Kristo kiuhalisia ni sheria.

> "Lakini aliyeitazama **sheria kamilifu iliyo ya uhuru** [G1657], na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake." Yakobo 1:25

Neno *uhuru* hapa katika Kiyunani linatokana na neno la msingi sawa na neno ambalo Yohana alilitumia kuelezea uhuru katika Yohana 8:36. Tena, neno hili hili linatumiwa hapa na Paulo:

> "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha **huru** [G1659], mbali na sheria ya dhambi na mauti." Warumi 8:2

Mwana wa Mungu alikuwa amempa Lusifa kila kitu bure. Lusifa aliishi kwa uzima uliokuwa ndani ya Mwana wa Mungu. Kristo alikuwa akishiriki maisha haya pamoja naye. Lusifa hangeweza kuwa na uzima mbali na Mwana wa Mungu. Yohana alimwita Yesu Neno la Uzima (1 Yohana 1:1) na tena kama tulivyochunguza, wale walio na Mwana wana uzima. (1 Yohana 5:12).

Kila kitu alichokuwa nacho Lusifa alipewa na Mwana wa Mungu. Uongo wa kutokufa kwa nafsi unaweza kuwapofusha wasomaji wa Biblia wasiuone ukweli kwamba kila pumzi aliyoivuta Lusifa, muda baada ya muda, aliipokea kutoka kwa Mwana wa Mungu bila malipo yoyote.

> "Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya

> wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; **kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.**" Matendo ya Mitume 17:24-25

Uhai na pumzi ambayo Mungu huwapa vitu vyote si zawadi ya mara moja, kwa vile Paulo anavyoendelea:

> "**Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu**. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema, Maana sisi sote tu wazao wake." Matendo ya Mitume 17:28

Je, tunaweza kufahamu ukweli wa Mwana wa Mungu anayesoma matamanio ya Lusifa ya kumuua yule anayempa uhai muda baada ya muda? Ni uzima na uhuru pekee unaoshuka kutoka moyoni mwa Mwana wa Mungu kama mto mkubwa. Hakuna mauti, hakuna kizuizi cha nje na hakuna nguvu ya kulazimisha iliyo ndani ya moyo Wake.

Kwa hiyo, Mwana wa Mungu angeweza kumvuvia Daudi kuandika, si tu kwa uzoefu wake mwenyewe, bali kuhusu uzoefu wa Mwana wa Mungu katika kuzungumza na Baba Yake:

> "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji. Waandaa meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika." Zaburi 23:4-5

Katika kujua mawazo ya Lusifa, Baba na Mwana walijua matokeo yangekuwa ni kitu gani. Mawazo yaliyopotoka ya Lusifa yalikuwa "mwanzo" na Mungu na Mwanawe walijua ni wapi yangeishia. (Isaya 46:10). Pale mawazo ya Lusifa yalipoumbika katika akili yake, mbegu na matokeo yake vilikuwa ndani yake. Hakuna mwingine ambaye angeweza kuona mbegu hiyo isipokuwa Baba na Mwana. Hakuna mtu mwingine aliyejua mahali ambapo njia hii ingeelekea isipokuwa Baba na Mwana.

Uzao wa Mwana wa Mungu pia ulikuwa umeumbika kikamilifu na tayari ulikuwa umeanza kuzaa matunda katika amani na utulivu wa mbinguni. Baba na Mwana pia walijua tunda la mbegu ambayo ilikuwa ndani ya Kristo. Pia wangeweza kuzungumza juu ya wakati

ujao kutokana na zile mbegu mbili, uzao wa Kristo na uzao wa Shetani, kwa kadri ambavyo wakati ujao ulivyokuwa mgumu, kwa kuwa Walikuwa wamejenga ukaribu na hali ya kujaliana kama hiyo—inayoelezwa kama Kristo aliye katika "kifuani cha Baba."

Hii ndiyo tofauti kati ya uelewa wa kiungu wa mambo yajayo na mitazamo ya mwanadamu ya kujua yote (omniscient). Ufahamu wa kiungu wa kujua mambo yajao hutokana na tunda la mbegu za kiroho ambazo zimepandwa katika akili za viumbe vilivyoumbwa. Mafundisho ya mwanadamu ya kujua yote hayana kanuni ya mbegu lakini yanafanya kazi katika mazingira ya kujitegemea ya kujua kila kitu kabisa.

Ndani ya kanuni ya kimbingu ya kupanda mbegu na kuzaa matunda, mojawapo ya matatizo makubwa zaidi ya fundisho la kujua yote ni kwamba ikiwa Mungu alijua kwa hakika kwamba Lusifa angeanguka kabla ya kuumbwa kwake, basi Mungu mwenyewe ndiye muumbaji wa Shetani, kwa kuwa wazo hilo lilianzia kwake. Hili kwa upande wake lazima limfanye yeye kulaumiwa na kuwajibika kwa tatizo la dhambi, kwa maana Yeye alikuwa wa kwanza kulifikiria na kulitazamia.

Mungu ana ujuzi sahihi sana wa wakati ujao kwa sababu aliumba ulimwengu na anajua taratibu zake kwa ukaribu. Pia anaweza kusoma mawazo ya viumbe vyake na kwa hiyo kujua athari za mawazo hayo. Anaweza pia kupima kwa upole azimio la mapenzi ya viumbe Wake kwa kuwapulizia Roho juu yao ili kupima mwitikio wao wa ndani.

> "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho." Yohana 3:8

Mambo haya yote yanatoa utofauti kati ya ukweli wa ukuu wa maarifa ya Mungu na uongo kwamba Mungu anajua kila kitu. Hapa tunao ushahidi wa mambo ambayo hayakuingia akilini mwa Mungu na kwa hiyo ni mambo ambayo Hakuyajua kabisa:

> ..."nao wamemjengea Baali mahali pake palipo juu, ili kuwachoma moto wana wao, wawe sadaka za kuteketezwa kwa Baali; tendo nisiloliamuru mimi, wala kulinena, **wala halikuingia moyoni mwangu;**" Yeremia 19:5

Wazo la dhabihu ya mtoto kwa ajili ya dhambi kamwe halikuingia akilini mwa Mungu. Ukweli huu peke yake unathibitisha dhana ya uongo kwamba Mungu alianzisha wazo kwamba haki yake ingetoshelezwa tu kwa kuuawa kwa Mwanawe mwenyewe. Hili halikuingia akilini Mwake. Alichokijua ni hatari za kuwapa viumbe huru wa kuchagua na uwezekano ambao ungeweza kutokea.

Mwitikio wa asili wa Kikristo ni kujitenga na wazo kwamba Mungu hayuko katika udhibiti wote na kamili kama wanavyofikiria. Anadhibiti kupitia kanuni ya mbegu yaani mbegu, ukuaji na mavuno. Bado utofauti huu kati ya ujuzi mkubwa wa Mungu na uongo wa kujua kila kitu hutoa nafasi kwa ukweli mzuri wa pendo la kiungu la kujihatarisha.

Mungu na Mwanawe walijihatarisha kwa Lusifa na malaika. Walipanda mbegu ya upendo, furaha, uhuru, subira na baraka ndani yao. Hawakuweka kizuizi juu yao kwa sababu malaika hawakuwa na kutokufa kwa asili na kwa hivyo hakuna neno lolote la Mungu lingeweza kueleweka kuwa lililazimishwa. Waliunganishwa kwa karibu sana na Mungu na Mwanawe; walikuwa wakidhihirisha mbegu ambayo Baba na Mwana walikuwa wameipanda ndani yao - hadi siku ile uovu ulipoonekana ndani ya Lusifa.

> "Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa,
> hata uovu ulipoonekana ndani yako." Ezekieli 28:15

Kupata kitu ni mchakato wa ugunduzi. Andiko halisemi, "hata uovu ulipopandwa ndani yako." Hili ni kwa sababu Lusifa alifanywa mkamilifu. Kwa hiyo ni jambo la kimantiki kwamba Mungu na Mwanawe walichoweza kukiona baadaye ni uovu ndani ya Lusifa. Haikuwa kitu walichokipanda pale, wala hawakujua kwa hakika hili lingetokea. Katika kuwapa malaika uhuru wa kuchagua, walijua hatari waliyokuwa wakichukua lakini walitoa kila kitu kilichohitajika ili kuruhusu ufanisi na baraka.

Wengi wanaochukua msimamo wa wale wasioamini kuna Mungu hupata msimamo huu usiovumilika. Wazo lao ni kwamba ikiwa kuna Mungu na Yeye ndiye aliyeumba kila kitu, basi angepaswa kuviweka sawa na kuhakikisha kwamba hakuna jambo lolote baya lingetokea. Kwa hiyo, kuna aina ya utoshelevu katika kuona Wakristo

wanashikilia fundisho la kujua yote, linawaandalia tu mazingira mazuri ya kumkataa Mungu na kumhukumu kwa kuruhusu dhambi kuja katika ulimwengu. Wasioamini kuna Mungu (Atheism) ni kinyume cha kimantiki cha fundisho la Kikristo la kujua yote. Upendo wa kiungu wa kujihatarisha ni onyesho la kimantiki la Mungu mwenye hekima yote, mwenye upendo wote, atoaye uhuru.

Ukristo na wasioamini kuna Mungu wapo katika umoja wa lahaja. Wote wawili wanaanza na dhana kwamba Mungu alijua kwamba uovu ungekuja ulimwenguni. Ukristo unajaribu kuhalalisha matendo ya Mungu, wakati wasioamini kuna Mungu wanayalaani. Haya yote yanaweza kuepukwa kwa kuja katika uhalisi wa kanuni ya mbegu ya Mungu na kuingia katika upendo wa Agape wa Baba na Mwana. Kwa ajili ya upendo na shauku ya uhuru, Mungu alijihatarisha kwa kuumba ulimwengu wa uchaguzi huru.

Lusifa alikataa urithi wake, akajidanganya na akachagua kuamini kwamba zawadi zote alizopewa zilikuwa zake. Alimdharau yule aliyempa vyote na akatamani kumuua na kuchukua mahali pake. Matendo haya hayakuwa katika mawazo ya Baba na kwa hiyo hayakuwa katika mawazo ya Mwana wa Mungu. Hawakufikiria ubaya huo kabla ya Lusifa kuuwaza. Walijua kwamba kwa uumbaji wao kuchagua kinyume na mapenzi ya Mungu kungehusisha maumivu, huzuni, na kifo hata hivyo kabla ya hatua hizo kuchukuliwa haikujulikana matokeo yangekuwaje.

Shetani alipoanza kujiepusha kutoka katika ushikamanifu wake kwa Mungu na Mwana Wake, ikawa wazi zaidi ni nini kingetokea. Shetani alipoazimia kuasi mbingu na kuchagua njia yake mwenyewe, Mungu alijua kabisa mwisho ungekuwa nini. Hili ni kwa sababu mbegu ilikuwa tayari imekwishaumbika na isingebadilishwa. Iliwekwa na kwa hiyo lazima izae matunda yaliyomo ndani yake.

Ingekuwa kwamba Shetani ndiye peke yake ambaye alikuwa amechukua njia hii, matunda ya njama za Shetani yangeweza kutambuliwa haraka. Ukweli ni kwamba karama ambazo Shetani alikuwa amezipokea, alizielekeza kwenye mpango wa hila na mahesabu wa kupindua serikali ya Mungu, akipanda mafarakano na wasiwasi katika akili za viumbe vyote. Kiini cha mpango wake kilikuwa nadharia yake mpya ya haki.

Ili tuweze kuzama katika sehemu hii ya hadithi mbinguni, tunakumbuka kanuni hii iliyotajwa katika Maandiko. Hii ni nyanja inayofuata ya kanuni ya mbegu.

> "Yaliyokuwako ndiyo yatakayokuwako; na yaliyotendeka ndiyo yatakayotendeka; wala jambo jipya hakuna chini ya jua." Mhubiri 1:9

> "Yale yaliyoko yamekuwako; na hayo yatakayokuwako yamekwisha kuwako; naye Mungu huyatafuta tena mambo yale yaliyopita." Mhubiri 3:15

> "Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani." 1 Wakorintho 10:11

> "Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini." Warumi 15:4

Mbegu ya fulani hutoa matunda ya aina hiyo hiyo. Hii ndiyo sababu vita vilivyotokea mbinguni vinarudiwa tena duniani kwa uwazi zaidi na zaidi. Tunaposoma hadithi za Biblia, tunapata picha iliyo wazi zaidi kuhusu masuala yaliyotukia mbinguni. Dunia kwa kuanguka kwake katika dhambi imekuwa hatua ambayo juu yake mawazo ya siri ya Shetani yanadhihirishwa kikamilifu

Uzuri wa kanuni ya mbegu ni kwamba tunaweza kufuatilia uthibitisho wa uzao wa Kristo na uzao wa Shetani katika matendo ya jamii ya wanadamu yanayoelezwa katika Biblia. Shetani alikuwa muuaji tangu mwanzo. Mbegu hii iliruhusiwa kupandwa katika maisha ya watu kama Kaini, Nimrodi, Absalomu na wengine. Tutaangalia hadithi hizi ili kuunganisha masuala muhimu ya vita ya asili mbinguni.

Mwana wa Mungu alipofanyika mtoto mchanga huko Bethlehemu, kanuni zilizofichwa za mbegu hizo mbili zilifunuliwa kwa undani zaidi. Katika nia ya Herode iliyodhihirishwa ya kutaka kumuua mtoto Yesu (Mathayo 2:16), tunaona kufunuliwa shauku iliyofichwa ya kumuua Mwana wa Mungu hapo mwanzo.

> "Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha **Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.**" Ufunuo wa Yohana 13:8 (KJV)

Kama tulivyoeleza hapo awali katika sura ya 5, ndani ya kanuni hii ya mbegu tunaweza kupenyeza matukio tangu mwanzo wa wakati, kwani mbegu daima huzaa matunda yale yale. Hii ndiyo kanuni kama inavyoonyeshwa katika Isaya 46:10; ni kupitia kanuni ya mbegu kwamba Mungu anajua "mwisho tangu mwanzo." Kama vile ambavyo miti ya shambani inavyozaa matunda yale yale kila mwaka, vivyo hivyo matukio ya historia huzaa matunda yale yale kutoka kwenye mbegu iliyopandwa hapo mwanzo. Kuzaliwa kwa Kristo, uzima na kifo chake katika ulimwengu huu hutufunulia mambo ambayo yamefichwa tangu mwanzo. Mambo yaliyofichwa ya giza yanaletwa kwenye Nuru.

> "Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, **sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, ikadhihirishwa wakati huu** kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii Imani." Warumi 16:25-26

Katika njama na hila za Mafarisayo tunapata ufunuo wa utendaji kazi wa Shetani katika kutafuta kumwangamiza Kristo na wafuasi wake tangu mwanzo hadi sasa.

SURA YA 11

# MFUMO WA MUUNDO WA KIMUNGU NA UPINZANI WAKE

Kabla ya kuangalia hadithi hizi katika Agano la Kale, tunahitaji kuzingatia nyanja nyingine. Hii inahusiana na mifumo miwili tofauti iliyoundwa na mwitikio wa Mwana wa Mungu na wa Shetani juu ya nneo la Baba. Hili ni la muhimu kulielewa kwa sababu ni sehemu ya mchakato wa mbegu na hujitokeza tena na tena katika Maandiko. Fikiria uhusiano uliofunuliwa kati ya Baba na Mwana katika aya hii.

> "lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, **aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake**, nasi tunaishi kwake; yuko na **Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo**, na sisi kwa yeye huyo." 1 Wakorintho 8:6

Mwana wa Mungu anamtii Baba yake kwa uhuru na kwa furaha. Maneno na matendo ya Baba hupitia kwa Mwana. Baba ndiye chanzo na Mwana ndiye njia. Vitu vyote ni vya Baba na vitu vyote hupitia kwa Mwana. Utaratibu huu huleta matokeo yafuatayo:

> "Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake,...." Waebrania 1:3

Utukufu wa tabia ya Baba unafanywa kuwa angavu zaidi unapopitishwa kupitia kwa Mwanawe. Huu ni ukuaji wa asili wa mawazo ya Baba yaliyopandwa ndani ya moyo wa Mwanawe. Mwana

hukuza kile ambacho Baba yake anakifanya. Hukifanya kuwa kikubwa na na chenye kung'aa zaidi. Biblia husema haya kuhusiana na Kristo:

> "BWANA akapendezwa, kwa ajili ya haki yake, **kuitukuza sheria, na kuiadhimisha**." Isaya 42:21 (KJV)

Yesu anakuza sheria ya Baba yake kupitia maisha yake, maneno na matendo yake. Kwa sababu anasema "Amina" kwa Baba yake, mawazo na maneno ya Baba yanapanuliwa kupitia Mwanawe. Ni kwa kanuni hii ambapo Kristo anaweza kuwaambia wanafunzi wake:

> "Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na **kubwa kuliko hizo atafanya**, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba." Yohana 14:12

Mfuasi wa Kristo anaposema "Amina" kwa kile ambacho Kristo anamwomba, kanuni ya ukuzajij inapanuka zaidi ili kwamba kazi kubwa zaidi ziweze kufanywa. Si mwanafunzi anayedai sifa kwa ajili ya kazi, kwa sababu inafanywa ndani yake na Kristo na ni Baba anayefanya kazi katika Kristo. Hili huleta kuporomoka kwa haraka kwa ufalme wa mbinguni. Kwa maelezo mapana juu ya Muundo wa Kimungu tafadhali soma kijitabu ***"The Divine Pattern of Life"*** kinachopatikana katika *fatheroflove.info*

Katika muundo wa Kimungu hakuna mvutano kati ya chanzo na njia. Kanuni hii hufanya kazi katika nyanja zote za ufalme wa Mungu. Kwa sababu njia inaamini chanzo, kuna amani kamilifu tu. Hii ni kwa sababu njia imetoka kwenye chanzo na inakaa katika utambulisho huo.

> "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini." Isaya 26:3

Kanuni ya pili ya Muundo wa Kimungu ni kwamba chanzo kwa kawaida hakionekani, huku njia ikionekana.

> "naye[Kristo] ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote." Wakolosai 1:15

Kristo, kama Neno la Mungu, ni mawazo ya Baba yanayodhihirishwa ili wote wayasikie, (Yohana 1:1,14). Muundo huo umeigwa katika

maeneo mengi katika ulimwengu wetu. Kama viumbe wenye akili tunaeleza mawazo yetu ya ndani kupitia maneno, na kufanya mchakato wetu wa mawasiliano kuwa chanzo kisichoonekana kinachoonyeshwa kupitia njia inayoonekana (njia ya kusikika).

Hili litakuwa muhimu kulikumbuka tunapoendelea. Muundo anaotumia Shetani unaweza kuelezewa vyema zaidi katika fikra za kimagharibi kama nadharia, upingaji, unaoongoza kwenye usanisi ambao wakati mwingine huitwa lahaja za Hegelian (Hegelian Dialectic). Katika mawazo ya mashariki tunaweza kueleza hili kama Yin na Yang katika duara moja. Ni kanuni zinazopingana ambazo zinaunganishwa pamoja na migogoro, mjadala, mabishano na vita. Muundo huu ulianzishwa na maneno ya Shetani.

> "Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu." Isaya 14:13-14

Shetani alitamani kiti chake cha enzi, alitaka kufanana na Mungu. Hii inaunda vyanzo viwili. Uwepo wa vyanzo viwili hujenga mvutano wa moja kwa moja. Nani atakuwa wa kwanza na nani atakuwa wa pili? Haiwezekani kukawa na cha kwanza na cha pili, lazima viunganishwe pamoja kama vipinganavyo kwa namna ya fumbo.

Kanuni ya upinzani ni ya asili sana kwetu. Serikali zote za kidemokrasia zina upinzani uliochaguliwa serikalini. Serikali na upinzani zimeunganishwa pamoja kama bunge moja.

Kama jaribio rahisi, tunaweza kufikiria jinsi Akili ya Muundo wa Kimungu unavyofanya kazi tofauti na mfumo wa upinzani wa Shetani. Chukua kwa mfano neno:

NURU

Katika mfumo wa Shetani kwa kawaida ungefikiria neno hili:

GIZA

Lakini katika mfumo wa Muundo wa Kimungu ungefanya kazi kama hii.

Mfumo wa Shetani unafikiri kinyume. Mfumo wa Mungu unafikiri vivyo hivyo bado imekuzwa. Hili linakuwa muhimu tunapoingia kwenye somo letu linalofuata na vita vilivyotokea mbinguni.

SURA YA 12

# KUPATANA KWA HAKI NA REHEMA

Kama tulivyojadili hapo awali, Shetani aliziona karama ambazo Kristo alikuwa amempa kama vitu ambavyo alikuwa navyo kiasili ndani yake. Alimkasirikia Mwana wa Mungu na hatimaye akafika mahali alipopanga kumuua. Jinsi Shetani alivyopanga mashambulizi yake inaweza kuonekana hasa katika kisa cha Danieli katika tundu la simba na kisa cha Absalomu.

Kama tulivyozungumza katika sura ya 6, imani ya Shetani kwamba uhai wake ulitokana na yeye mwenyewe ilibadili mtazamo wake kuhusu sheria. Hapa ndipo ulaghai ulipoanza kudhihirika.

> "Je! Kiti cha udhalimu kishirikiane nawe, Kitungacho madhara kwa njia ya sheria?" Zaburi 94:20 (KJV)

Mawazo ambayo Shetani alianza kuyahisi dhidi ya Mwana wa Mungu yalielekea kwenye uharibifu.

> "Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi;...." Ezekieli 28:16

Wazo la udhalimu ni usemi unaoashiria upinzani. Shetani aliamini kwamba uhai na uwezo aliokuwa nao ni wake mwenyewe. Alihisi kwamba Mwana wa Mungu alisimama katika njia yake. Alikuwa na mawazo ya kutumia nguvu zake alizokuwa nazo ili kumshinda Mwana wa Mungu. Hata hivyo, ilimbidi atafute njia fulani ya kumnasa

Mwana wa Mungu. Tunaweza kuchukua sehemu katika kisa cha Danieli ambayo itatupatia mwanga zaidi katika hili.

> "Ilimpendeza Dario kuweka juu ya ufalme maliwali mia na ishirini, wawe juu ya ufalme wote; na juu yao akaweka wakubwa watatu, na Danieli alikuwa mmoja wao; ili maliwali hawa watoe hesabu kwao, mfalme asipate hasara. **Basi Danieli huyo alipata sifa** kuliko wakubwa na maliwali, **kwa kuwa roho bora ilikuwa ndani yake; naye mfalme akaazimu kumweka juu ya ufalme wote**. Basi mawaziri na maamiri wakatafuta sana kupata sababu za kumshitaki Danieli kwa habari za mambo ya ufalme; lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa; kwa maana alikuwa mwaminifu, wala halikuonekana kosa wala hatia ndani yake. **Ndipo wale watu wakasema, Hatutapata sababu ya kumshitaki Danieli huyo, tusipoipata katika mambo ya sheria ya Mungu wake**. Basi wale mawaziri na maamiri wakakusanyika pamoja mbele ya mfalme, wakamwambia hivi, Mfalme Dario, uishi milele. **Mawaziri wote wa ufalme, na manaibu, na maamiri, na madiwani, na maliwali wamefanya shauri pamoja ili kuweka amri ya kifalme; na kupiga marufuku, ya kwamba mtu ye yote atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku thelathini, ila kwako, Ee mfalme atatupwa katika tundu la simba."** Danieli 6:1-7

"Roho bora ilikuwa ndani ya Danieli." Hiki ni kielelezo cha Roho bora ndani ya Mwana wa Mungu. Kristo aliwekwa juu ya nyanja zote. Tunaona kwamba wale waliokuwa chini ya Danieli mara moja hawakumkabili Danieli moja kwa moja au kumdhuru moja kwa moja, bali walimwendea mfalme na ombi lililoonekana kumheshimu mfalme. Walitaka kutoa amri kwamba mtu yeyote asiombe mungu yeyote isipokuwa mfalme. Amri hii ilionekana kuimarisha cheo cha mfalme. Ililenga kumwangamiza Danieli.

Kwa habari ya Mwana wa Mungu, Shetani na wale waliokuwa pamoja naye walitumia njia tofauti ili kuleteleza matokeo sawa na yaliyompata Danieli. Hili linapatikana katika kisa cha Absalomu.

> "Tena Absalomu huondoka asubuhi na mapema, na kusimama kando ya njia ya lango; kisha ikawa, mtu ye yote aliyekuwa na neno, lililokuwa halina budi kufika kwa mfalme ili kuhukumiwa,

> Absalomu humwita mtu huyo kwake, na kumwuliza, Wewe u mtu wa mji gani? Naye akasema, Mtumwa wako ni mtu wa kabila fulani ya Israeli. Naye Absalomu humwambia, Tazama, maneno yako ni mema yenye haki; lakini hapana mtu aliyeagizwa na mfalme kukusikiliza. Tena Absalomu husema, Laiti mimi ningewekwa kuwa mwamuzi katika nchi hii, ili kila mtu mwenye neno au daawa aje kwangu, nimpatie haki yake! Tena ikawa hapo alipokaribia mtu ye yote kumsujudia, hunyosha mkono wake, na kumshika, na kumbusu. Hivyo ndivyo Absalomu alivyowatendea Israeli wote, waliomwendea mfalme ili wapate hukumu; na hivyo Absalomu akawadanganya watu wa Israeli." 2 Samweli 15:2-6

Jina Absalomu maana yake ni baba wa amani, lakini siri iliyojificha chini ya jina hili ilikuwa tabia ya chuki na vita. Absalomu alitaka baba yake amwadhibu Amnoni, kaka yake wa kambo, ambaye alimnyanyasa kingono dada wa Absalomu, Tamari. Kwa sababu mfalme Daudi hakutekeleza hukumu dhidi ya Amnoni, Absalomu alimdharau baba yake na kuamua kumpindua. Absalomu alichukua mambo mkononi mwake na kumuua Amnoni kwa haki aliyoona inafaa. Kisha akaanza kuivuta mioyo ya ufalme wa Israeli.

> "Mfalme akamwambia, Kwa nini aende nawe? Lakini Absalomu akamsihi sana, naye akamwacha Amnoni na wana wote wa mfalme waende naye. Kisha Absalomu akawaamuru watumishi wake, akasema, Angalieni basi, moyo wake Amnoni utakapofurahiwa kwa mvinyo; **nami nitakapowaambia, Mpigeni Amnoni, ndipo mwueni, msiogope; si mimi niliyewaamuru? Iweni hodari, iweni na ujasiri.** Basi watumishi wa Absalomu wakamfanyia Amnoni kama alivyoamuru Absalomu. Ndipo wakaondoka wana wote wa mfalme, wakapanda kila mtu nyumbu wake, wakakimbia." 2 Samweli 13:27-29

Shetani, ambaye awali alikuwa Lusifa, hakufurahishwa na ukweli kwamba Mwana wa Mungu aliinuliwa juu yake. Alihisi kuwa ni dhuluma kwake na akaazimia kumpindua Mwana wa Mungu. Baba yake aliweka wazi kwa wote kwamba malaika wote walipaswa kumwabudu Mwana wa Mungu.

> Na alipomleta Mwanawe mkuu ulimwenguni, Mungu alisema, "Na wamwabudu malaika wote wa Mungu." Waebrania 1:6 (NLT)

Kifungu hiki kinarejelea kuja kwa Kristo duniani, lakini kanuni ya mbegu inaturudisha kwenye mwanzo wa vita mbinguni.

> **"ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba**. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka." Yohana 5:23

Lusifa alikataa kujisalimisha kwa hili. Aliazimia kuupindua ufalme wa Mungu. Alijishindia malaika wengi upande wake. Kama vile katika kisa cha Absalomu, suala lililokuwapo lilikuwa likihusiana na haki.

> "Tena Absalomu husema, Laiti mimi ningewekwa kuwa mwamuzi katika nchi hii, ili kila mtu mwenye neno au daawa aje kwangu, **nimpatie haki yake**!" 2 Samweli 15:4

Uvumi wa Absalomu ulikuwa kwamba mfalme hakuwa akiwapa raia wake haki, lakini dai hili lilikuwa la uongo. Katika kitabu cha Samweli tunasoma:

> "Daudi akatawala juu ya Israeli wote; **naye Daudi akawafanyia hukumu na haki watu wake wote**." 2 Samweli 8:15

Daudi alikuwa akiwatendea haki raia wake, lakini haikuwa haki ambayo Absalomu alifikiri ilihitajiwa. Daudi alionyesha rehema kwa sababu rehema za Mungu zilikuwa pamoja naye na kuuimarisha ufalme wake.

> "Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu; akitenda maovu nitamwadhibu kwa fimbo ya binadamu na kwa mapigo ya wanadamu; **lakini fadhili zangu hazitamwondoka**, kama vile nilivyomwondolea Sauli, niliyemwondoa mbele yako. **Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako. Nacho kiti chako kitafanywa imara milele."** 2 Samweli 7:13-16

Absalomu hakutaka ufalme uliojengwa juu ya haki inayoonyesha rehema. Alitaka uadilifu unaowahukumu wakosaji bila huruma. Kama tunavyoona katika kisa cha Danieli, ni mtu wa tatu mwenye mamlaka katika ufalme, baada ya mfalme na mtu wa mkono wa kuume wa mfalme, aliyeanzisha amri ya kifo kwa kukosa uaminifu kwa mfalme. Lusifa alianza kuchochea nadharia mpya ya haki iliyodai adhabu kwa mkosaji. Huu ulikuwa udhalimu ambao alikuwa akiufanya kupitia sheria.

Sheria ya Mungu ilikuwa sheria ya uzima na uhuru. Kwa vile Baba ndiye pekee ambaye kwa asili alikuwa na hali ya kutokufa na Mwanawe alimiliki kutokufa huku kwa upendo na heshima ya Baba yake, malaika wengine wote walipewa uzima huu kupitia Mwana wa Mungu, kila wakati.

Lusifa aliigeuza sheria ikaonekana kama kanuni ambayo malaika wanapaswa kuitii na kwamba wale wasioitii wanapaswa kuadhibiwa. Hii ndiyo aliyoiita haki. Hii ilikuwa tofauti na haki ya Mungu. Zingatia kwa makini aya ifuatayo.

> "Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako: Fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako. Zaburi 89:14 (KJV)

Andiko hili la Biblia ni la muundo wa sentensi wa Kiebrania. Sentensi ya pili ni ufafanuzi wa ile ya kwanza. Inarejelea kanuni za sehemu ya kwanza kwa njia iliyokuzwa. Hivi ndivyo Muundo wa Kimungu unavyofanya kazi. Kando na hili, uwekaji wa alama za uandishi wa Kiingereza pia hutoa kanuni hii. Nukta pacha baada ya neno kiti chako ina maana kwamba kinachofuata ni kueleza kilicho nyuma ya Nukta pacha.

1. Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako

   Ni sawa na

2. Fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako

Hiki kinachosemwa hapa ni kwamba haki inaonyeshwa kama rehema na hukumu inaonyeshwa kama ukweli. Hii inalingana kikamilifu na Muundo wa Kimungu. Haki ni jambo sahihi, na jambo sahihi ambalo Mungu hufanya ni kuonyesha rehema.

Lusifa alitumia mfumo wake wa upinzani kufanya haki kuwa kinyume cha rehema. Haki maana yake ni adhabu na ikiwezekana hata kifo. Rehema maana yake ni kuahirishwa kwa adhabu au kuhamishia adhabu kwa mtu mwingine. Shetani alianzisha wazo kwamba kila dhambi lazima iadhibiwe na kwamba ikiwa Mungu angeiondoa adhabu hiyo, basi hangekuwa Mungu wa kweli na haki.

Tunaona katika kisa cha Absalomu kwamba aliweza kuiteka mioyo ya taifa la Israeli kwa njia ya ulaghai.

> "Kwa hiyo Absalomu akaiba mioyo ya watu wa Israeli." 2 Samweli 15:6 (KJV)

Kwa njia hiyo hiyo Lusifa aliweza kuwahamishia malaika WOTE kwenye njia hii mpya ya kushughulika na haki na rehema. Ilieleweka kabisa kwao kwamba heshima ya kweli kwa Mungu ilimaanisha kwamba kuwe na amri ya kifo kwa wale wanaomvunjia Baba heshima. Waliona mantiki ya Shetani kuwa ya kumheshimu Mungu, bila kutambua kwamba ilidhoofisha utawala wa Mungu.

Kanuni hii ambayo Shetani alikuwa akiianzisha ilikuwa chukizo kwa Mungu. Tabia yake ilikuwa ya rehema, neema, mvumilivu na mwingi wa wema na ukweli. (Kutoka 34:6).

Kama tunavyoona katika kisa cha Danieli, si mfalme aliyeanzisha amri ya kifo kwa ajili ya kukosa uaminifu, bali ni mtu wa tatu katika ufalme na baadhi ya wale walio chini yake.

Mungu si mwanzilishi wa kifo. Kifo ni adui wa Mungu; kifo ni kinyume na sheria ya uzima na uhuru. Ikiwa sheria ya Mungu ingekuwa na amri ya kifo ndani yake basi hapangekuwa na uhuru. Kunaweza tu kuwa na woga utokanao na kutazamia adhabu ikiwa umeshindwa kufanya jambo sahihi.

Biblia inamwonyesha Shetani kuwa ndiye aliye na nguvu na mamlaka ya mauti, si Mungu.

> "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili **kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi,**" Waebrania 2:14

Sasa tuko tayari kuingia kwa kina katika somo hili katika sura zijazo. Sote tumefundishwa kwamba haki ya Mungu inadai kifo cha mkosaji. Ukweli ni kwamba huu ni mfumo wa haki wa Shetani uliowekwa juu ya sheria ya Mungu. Sheria ya uzima na uhuru isingeweza kamwe kuhusishwa na kifo. Haki ya Mungu ni kuonyesha rehema. Shetani alifanya haki na rehema kuonekana zinapingana. Aliipindisha sheria kwa namna ambayo angeweza kuwashawishi malaika wa mbinguni kwamba dhambi lazima iadhibiwe kwa nguvu na kwamba hili lilikuwa linaboresha serikali ya Mungu.

SURA YA 13

# UTAWALA WA MAUTI

Sasa tunaingia kwenye matokeo ya mwisho ya mbegu mbili. Tunda la uzao katika Kristo ni uzima: huru, wazi, bila kikomo, furaha, maisha yasiyo na mipaka. Mwana wa Mungu ni uzima. Imani yake kama ya mtoto na upendo kwa Baba Yake ndio msingi wa maisha ya kila kiumbe mwenye maadili katika ulimwengu. Sikia maneno ya Mwokozi - ni ya uzima tu.

> "Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;" Yohana 11:25

Mwana wa mbarikiwa anajitofautisha na yule anayeua na kuangamiza:

> "Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; **mimi nalikuja** ili **wawe na uzima**, kisha wawe nao tele." Yohana 10:10

Tabia ya Yesu ni nzuri sana hivi kwamba ufunuo wake wa Baba ulikomesha kifo.

> "na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; **aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili;"** 2 Timotheo 1:10

Ikiwa Yesu alikomesha kifo, basi haiwezekani kwake kujihusisha, au kudhihirisha jambo ambalo alilikomesha. Yesu alikomesha kifo kwa jinsi gani? Kupitia nuru ya injili.

Injili ni nini?

> "Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu." Marko 1:1

Mwana wa Mungu ni injili. Mwana wa Mungu alifanya nini?

> "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye." Yohana 17:4

Mwana wa Mungu alitukuzwa ikiwa ina maana alidhihirisha tabia ya Baba kwa ulimwengu. Kumbuka alimwambia Filipo: "Yeye aliyeniona mimi amemwona Baba." (Yohana 14:9). Ufunuo huu wa tabia ya Mungu ulikomesha kifo. Hii lazima iwe hivyo kwa sababu Yesu alisema kwamba alimaliza kazi ambayo Baba alimpa aifanye kabla ya kufa Msalabani.

Ilikuwa tu baada ya maombi haya kwamba Yesu aliwaambia umati:

> ".....lakini hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza." Luka 22:53

Sheria ya uzima na utoaji na baraka haingekoma. Kristo aliwapenda na kuwasamehe adui zake hadi mwisho. Hii inaonyesha asili isiyobadilika ya sheria ya Mungu. Yesu aliposema "Baba uwasamehe," alionyesha kwamba hatabadili tabia yake kamwe. Hatawapiga adui zake kamwe; Angewapenda tu na kuwasamehe na kuwaruhusu kupokea matokeo ya uchaguzi wao wenyewe kama tulivyoona katika uharibifu wa Yerusalemu miaka 40 baada ya kifo chake.

Sheria ya Mungu ni sheria ya upendo, uhuru, na uzima tele. Ni sheria ya msamaha na rehema. Hii ndiyo mbegu inayokaa ndani ya moyo wa Kristo. Popote itakapopandwa, itazaa matunda ya namna hiyo.

Shetani alijifanya kuwa adui wa Mungu kwa kusema uongo kuhusu tabia yake. Shetani alipoanzisha nadharia yake kuhusu haki na kufanya uharibifu kwa kuifanya sheria ya Mungu ionekane kama chombo kinachodai kifo, ilisababisha vita mbinguni - vita vya maneno. Malaika wengi waliungana na Lusifa na walikuwa wakijaribu kurekebisha serikali ya Mungu. Hata hivyo, ndani kabisa, Shetani alikuwa akitumia wazo hilo kama njia ya kumwua Mwana wa Mungu. Kama katika kisa cha Danieli, alitaka kumnasa Kristo kuhusiana na sheria ya Mungu wake. Shetani alijua tabia ya Mungu. Tunaambiwa:

> “Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.” Ezekieli 28:14

Mawe ya moto yanawakilisha uwepo wa Mungu katika nafsi. Tunaitwa mawe yaliyo hai na uwepo wa Mungu ni kama moto. Shetani alijua tabia ya Mungu na aliwazia kwamba ikiwa angeweka sheria ya Mungu kama kitu kinachohitaji kifo na kisha kusababisha viumbe kuasi, basi angeweza kumlaumu Mungu na kudai kwamba aliye sawa na Mungu alipe gharama ya kuwaokoa. Mpango wa upatanisho mbadala ulitungwa katika akili ya Shetani kama mpango wa kumuua Kristo.

Ilikuwa ni mpango wa kawaida wa mateka. Shetani alitumia sheria ya Mungu kujenga ngome ili kuwanasa mateka wake.

> “Nikaona ile amri iletayo uzima ya kuwa kwangu mimi ilileta mauti. Kwa maana dhambi, kwa kupata nafasi kwa ile amri, ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua.” Warumi 7:10-11 (KJV)

Paulo aliiona ile amri kuwa ya mauti kwa sababu ya dhambi; dhambi ambayo Shetani alikuwa ameianzisha hapo mwanzo.

> “Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake;” Ufunuo wa Yohana 12:7 (KJV)

Akijua ni nini kilichokuwa akilini mwa Shetani, Mungu alimsihi Lusifa mara nyingi kumtia moyo aache njia aliyokuwa akielekea. Tunaona kanuni hii ikidhihirishwa kwa jinsi Mungu alivyowafikia Israeli.

> Lakini kwa Israeli asema, “Mchana kutwa naliwanyoshea mikono watu wasiotii na wakaidi.” Warumi 10:21

Hivi ndivyo baba yeyote anayewapenda watoto wake angefanya. Mungu alimpenda mwanawe Lusifa na alitaka kumwokoa.

> BWANA alinitokea zamani, akisema, “Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu.” Yeremia 31:3

Baba aliwaeleza malaika kwamba alikuwa amemfanya Mwanawe kuwa sawa na Yeye mwenyewe na kwamba maneno ya Mwanawe yangefuatwa sawa na yeye mwenyewe.

> Lakini kwa habari za Mwana asema, "Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili." Waebrania 1:8

> "Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote; ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka." Yohana 5:22-23

> …"Huyo ndiye mpinga Kristo, yeye amkanaye Baba na Mwana. Kila amkanaye Mwana, hanaye Baba; amkiriye Mwana anaye Baba pia." 1 Yohana 2:22-23

Hizi ni kanuni za milele; wao ni sehemu ya sheria ya uzima. Wao ndio wapo katika kiini cha vita vilivyoanza mbinguni. Cha kusikitisha, Shetani alikataa kutubia kutokuridhika kwake kuhusu Kristo. Badala ya kumwabudu Mwana wa Mungu, alitaka Mwana wa Mungu amwabudu.

> Akamwambia, "Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia." Mathayo 4:9

Tunakumbuka kwamba kinachodhihirika duniani ni ufunuo wa kile kilichotokea tangu mwanzo. Shetani alidhihirisha yale yaliyokuwa moyoni mwake alipomjaribu Kristo. Anafunua mbegu ya nafsi yake. Alitaka kuchukua nafasi ya Kristo na kuabudiwa badala yake. Kisha alitumaini kumuua Kristo na kufuta kumbukumbu yake milele. Tunajua hili kwa sababu ya jinsi Shetani alivyomuua Kristo Msalabani na kisha kujaribu kumweka kaburini milele.

Ukweli huu wote ulikuwa umefichwa ndani ya moyo wa Shetani awali. Hata Shetani mwenyewe hakuelewa kabisa hapo mwanzo kiwango kamili cha alikoelekea. Baada ya Mungu kumfunulia Shetani kwamba uhai unakuja tu kupitia Mwana Wake, yeye na malaika zake walipaswa kufanya uamuzi.

Malaika wengi waliungana na Lusifa. Kuna kidokezo katika kisa cha Herode na kucheza kwa binti wa Herodia. Herodia alitaka kumuua

Yohana Mbatizaji. Alikuwa amepanga binti yake acheze na alijua kwamba binti yake angepewa zawadi. Tamaa yake ya kumuua nabii ilifichwa. Aliwakilisha nia zilizofichwa za Shetani. Mfalme anawakilisha serikali ya Shetani na mkakati wa kisiasa. Salome anayecheza anawakilisha kitu kinachotamaniwa. Wakati mfalme, chini ya ushawishi wa mvinyo, alipotoa ombi lake, alisema:

> "....Niombe lo lote utakalo, nitakupa. Akamwapia, Lo lote utakaloniomba **nitakupa, hata nusu ya ufalme wangu**." Marko 6:22-23

Herode anawakilisha mambo yanayochukiza ufalme wa Mungu. Usemi wa "nusu ufalme wangu" sio usemi wa kiholera bali usemi wa mtu aliye chini ya ushawishi wa moja kwa moja kwa njia za Shetani. Usemi huu huu unaonekana pia katika kisha cha Esta.

> Mfalme akamwambia, "Malkia Esta, wataka nini? Nayo ni haja gani uliyo nayo? Utapewa hata nusu ya ufalme." Esta 5:3

Ofa hii inarudiwa mara mbili zaidi kwa Esta na mfalme. (Esta 5:6; 7:2). Hadithi hii ina kipengele sawa na kwamba Hamani alibeba nia iliyofichwa ya kumwangamiza Mordekai. Mfalme ana hamu ya kumpa mke wake zawadi. Lakini hapa Esta anafanya kazi ya kuokoa yule anayemwakilisha Kristo, kinyume na Salome ambaye alikuja kuwa wakala wa kumwua Yohana Mbatizaji. Vyovyote iwavyo, mada inafanana na ina muundo huu wa msichana anayetolewa hadi nusu ya ufalme wake na mfalme.

Shetani alikuwa tayari kuua nusu ya ulimwengu ili kutimiza lengo lake la kutawala ulimwengu wote mzima. Wazo hili lina usemi wa kisasa katika mfululizo wa hivi karibuni wa Avenger ambapo mhusika Thanos (maana yake kifo) anaangamiza nusu ya ulimwengu ili kujihakikishia utawala wa ulimwengu mzima.[29]

Hii ingedokeza kwamba nusu ya malaika walikuwa pamoja na Kristo na nusu walikuwa pamoja na Shetani. Mara baada ya kuunda ngome yake akipendekeza haki ya Mungu ilidai kifo, alijaribu kuwafanya malaika chini ya ushawishi wake kuwa watumwa kwa kuwaambia kwamba Mungu hatawasamehe kwa kuwa upande wake. Tunapata

---

[29] https://en.wikipedia.org/wiki/The_Infinity_Gauntlet

dokezo lingine kwa hili kwa kile alichomfanyia Kaini. Baada ya kumvuta Kaini katika mauaji ya Abeli, alimtia muhuri katika ngome yake kwa kumsadikisha kwamba Mungu hatamsamehe.

> Kaini akamwambia Bwana Mungu, kosa langu ni kubwa mno hata siwezi kusamehewa. Mwanzo 4:13 (Brenton, translation from Greek OT)

Huu ni uzao wa Shetani. Hutoa matunda yale yale na hufanya kazi kwa njia ile ile. Maisha ya Kaini yanaonyesha kile Shetani alichokifanya kwa malaika. Aliwaambia Mungu hatawasamehe.

Hii ndiyo hatua ambayo Lusifa aligeuka na kuwa Shetani kabisa na Mshitaki wetu kikamilifu. Aliweka muhuri wa hatima yake katika hatua hii. Alijua tabia ya Mungu ni upendo. Alijua kwamba Mungu ni mwenye rehema. Tunatoa kwenye kisa cha Yona, ambapo Yona anakatishwa tamaa kwamba Ninawi haikufutiliwa mbali.

> "Akamwomba BWANA, akasema, Nakuomba, Ee BWANA; sivyo hivyo nilivyosema, hapo nilipokuwa katika nchi yangu? Hii ndiyo sababu nalifanya haraka kukimbilia Tarshishi; kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya." Yona 4:2

Shetani sasa anaasi kikamilifu sheria ya upendo. Alijua Mungu angesamehe lakini alidanganya na kuwaambia malaika wake waliomtazama kuwa Mungu hatasamehe. Hili liliwaingiza katika giza na utawala wa Shetani. Tunaona kanuni hii ikionyeshwa kinyume kama ifuatavyo:

> ".....uwafumbue macho yao, na kuwageuza **waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao**, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi." Matendo ya Mitume 26:18

Shetani alivunja sheria kwa kusema Mungu hatasamehe. Huu ni uzao wa Shetani, na wa wote wanaorudia wazo hili kwamba Mungu hatasamehe uvunjaji wa sheria yake - sheria ya uzima na uhuru.

Malaika walioamini uongo wa Shetani walitia muhuri hatima yao pia. Hakukuwa na tumaini la wao kusamehewa kwa sababu hawakuamini kwamba Mungu angesamehe, na kwa hiyo hawakuomba msamaha kamwe.

Biblia inasema kwamba Baba ni mwenye rehema sikuzote. Rehema zake hazina mwisho.

> "Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni mwema; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. Mshukuruni Mungu wa miungu; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. Mshukuruni Bwana wa mabwana; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. Yeye peke yake afanya maajabu makuu; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**. Yeye aliyefanya mbingu kwa fahamu zake; **Kwa maana fadhili zake ni za milele**." Zaburi 136:1-5

Mungu daima yuko tayari kusamehe, lakini wale wanaosadiki kwamba hatasamehe, wanatenda dhambi dhidi ya nafsi zao na watakufa wote kwa sababu hawataomba kamwe. Msamaha wa Mungu huleta uzima na tabia ya Kristo ambayo huponya na kurejesha, kuturejesha kwenye sheria ya uzima. Ukiomba tu utapokea. Ukila matunda ya mti huu aliouumba Shetani, hakika utakufa. Ikiwa unaamini katika tabia ya Mungu wazo la kwamba Mungu anaweza kufika mahali ambapo hatasamehe, basi utakufa. Huu ni utawala wa mauti. Hii ni nguvu ya Shetani juu ya nafsi.

Ushindi mkubwa zaidi wa mbinu ya Shetani ni kuusadikisha ulimwengu kwamba Mungu ni Mungu wa mauti na kwamba Atatumia nguvu kuadhibu, na ikibidi, kuwaua wale wanaoendelea kuasi. Biblia inatuambia:

> "Kwa kuwa hatuna budi kufa, nasi tu kama maji yaliyomwagika chini, yasiyowezekana kuzoleka tena; **wala Mungu haondoi maisha** ila hufikiri shauri, kwamba yeye aliyefukuzwa asiwe mkimbizi kwake." 2 Samweli 14:14

Mstari huu ni wa thamani kwa sababu unahusiana na kisa cha Absalomu. Tunakumbuka kwamba Daudi hakumwadhibu mwanawe Amnoni, kwa kumbaka dada yake Absalomu, kwa namna ambayo Absalomu alitaka. Absalomu alichukua mambo mikononi mwake na kumuua Amnoni, ndugu yake wa kambo kwa ajili ya tendo lake.

Daudi alikuwa amemfukuza mwanawe Absalomu kwa kosa lake la kumuua Amnoni. Katika jitihada ya kupatanisha Daudi na Absalomu, Yoabu, kamanda mkuu wa jeshi la Daudi, alipanga njama ya kutuma mwanamke kwa Daudi ili kukata rufaa kwake kuhusu kesi iliyodhaniwa kuwa alikuwa nayo ambayo ilikuwa sawa na kesi ya Amnoni na Absalomu. Daudi alitambua mpango huo mara moja lakini mwanamke huyo akamsihi kwamba Mungu haondoi uhai (Mungu haui) bali anatafuta kurejesha watu wake waliofukuzwa. Kupitia mwanamke huyu mnyenyekevu Mungu alieleza moja ya ukweli wa maana sana wa mbinguni.

Katika mfumo wa Muundo wa Kimungu, uzima na mauti havitapatana kamwe. Uhuru na woga haviwezi kuwepo pamoja. Mungu ni upendo (1 Yohana 4:8) na tunapojua upendo huu basi hofu yote inatupwa nje. (1 Yohana 4:18). Hakuna hofu katika upendo (Agape). Lakini kuna hofu katika kifo. Kwa hiyo, Mungu hawezi kuwa na uhusiano wowote na mauti.

> "Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti." 1 Wakorintho 15:26

> "Ya kwamba atatujalia sisi, Tuokoke mikononi mwa adui zetu,
> Na kumwabudu pasipo hofu," Luka 1:74

Mauti ni utawala wa Shetani. Aliuunda kwa kuendeleza mfumo wa haki wa uongo kupitia sheria, akiwashawishi wengi kwamba uvunjaji wa sheria lazima uadhibiwe. Uhalifu mkubwa lazima uadhibiwe kwa kifo. Shetani alipata wazo la kifo kupitia tamaa yake ya Mwana wa Mungu kutokuwepo tena. Aliuwazia ulimwengu usiokuwa na mwana wa Mungu. Hili lilifungua mlango wa kanuni ya kifo.

Cha kusikitisha ni kwamba, njia pekee ambayo ulimwengu ungeweza kugundua ukweli wa kile ambacho Shetani alikuwa akikipanga ilikuwa ni kwa Mwana wa Mungu kumwacha Shetani amfanyie kile alichokitamani. Kusulubishwa kwa Yesu ni ufunuo wa mbegu ya mauaji iliyokaa ndani ya moyo wa Shetani tangu mwanzo.

Pale tabia ya kweli ya Baba itakapofunuliwa na ulimwengu ukafanya uchaguzi wake kuhusu Mungu wanayemtumikia, kila goti litapigwa na kukiri Yesu Kristo ni Bwana kwa utukufu wa Mungu Baba.

Wengine watafanya hivi kwa upendo. Wengine watafanya hivi kwa kulia na kusaga meno.

Kisha kifo na kuzimu vitangamizwa. Mwanzilishi wa kifo na wale waliomwamini watangamizwa na uzito wa hatia zao wenyewe. Moto utawaka ndani ya mioyo yao kwa kutambua kwamba walipoteza umilele na hawana wa kulaumiwa ila wao wenyewe.

> "Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto." Ufunuo wa Yohana 20:14

Kama vile tetemeko la ardhi ambalo liliitikisa dunia kwa nguvu sana wakati Kristo alipokufa Msalabani, ndivyo nchi pia itakavyolipuka, ikidhihirisha mawazo ya jeuri na chuki ya wale waliolaaniwa na kuwaangamiza. Dunia yenyewe itawatapika wakaaji wake. (Mambo ya Walawi 18:25). Wale ambao wamevunja Agano la Milele watachomwa mizizi na matawi. (Isaya 24:5-6; Malaki 4:1-2).

SURA YA 14

# ANGUKO LA LUSIFA NA MALAIKA ZAKE

Hakukuwa na sababu ya kimantiki kwa Shetani kuchagua njia aliyokuwa nayo. Alijua kwamba Mungu alikuwa mwenye upendo, mwenye rehema na mwenye kusamehe. Alijua kwamba Mwana wa Mungu alikuwa amemuumba yeye na malaika wote na ulimwengu. Kukataa kwake kwa makusudi kiuhalisia hakuwezi kuelezewa. Hii ndiyo siri ya uovu. Inawezekanaje malaika huyu mzuri na mpole aitwaye Lusifa angewezaje kuwa Shetani? Hakuna maelezo kwa nini Shetani alichagua kutafuta kimbilio katika uongo, udanganyifu na machafuko.

Shetani lazima alitetemeka kwa muda kwa kuwa alikuwa tayari kusema uongo kama huo kuhusu tabia ya Mungu. Katika maisha ya Kaini, tunaona kutetemeka na kutetereka alikokupata katika kutembea katika njia ya Shetani. Kaini alidhihirisha msukosuko wa ndani wa Shetani na kuwa na wasiwasi, woga, na mfadhaiko kwa kupoteza utambulisho wake.

Alijiuliza ikiwa kama angeendeleza mpango wake wa awali; je, angejitia rasmi katika vita dhidi ya Mungu na Mwanaye?

> “Mbona mataifa wanafanya ghasia, Na makabila wanatafakari ubatili Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya BWANA, Na juu ya masihi wake, Na tuvipasue vifungo vyao, Na kuzitupia mbali nasi kamba zao.” Zaburi 2:1-3.

Katika giza hili zito ambalo Shetani alikuwa amelitupa kwa malaika, Mungu alisababisha nuru ya kweli iangaze katika uso wa Mwanawe.

> **"Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani**, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo." 2 Wakorintho 4:6.

Andiko hili ni udhihirisho wa kile kilicho ndani ya Mwana. Yeye ni Nuru daima; Yeye daima ni ukweli wa Baba na yeye daima ni njia ya Baba. Mwana wa Mungu aliingia Katika giza ili kutangaza upendo, rehema na neema ya Mungu.

Maneno yake yalikuwa kama upanga kutoka kinywani Mwake, na macho yake kama mwali wa moto. Utukufu wa Bwana ulikuwa tumaini na furaha kwa malaika waliomwamini, lakini alikuwa kama moto ulao (Kut 24:17) machoni pa wale malaika walioamini uongo wa Shetani. Nuru ikaingia gizani, na Neno la Mwana wa Mungu likaleta utengano kati ya wale waliokuwa na Shetani na wale walio pamoja na Mungu.

> "Ee BWANA, mito imepaza, Mito imepaza sauti zake, Mito imepaza uvumi wake. Kupita sauti ya maji mengi, maji makuu, Kupita mawimbi ya bahari yaumkayo, BWANA Aliye juu ndiye mwenye ukuu." Zaburi 93:3-4.

> "Joka akatoa katika kinywa chake, nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto, amfanye kuchukuliwa na mto ule." Ufunuo wa Yohana 12:15.

> "Basi, wataliogopa jina la BWANA toka magharibi, na utukufu wake toka maawio ya jua; **Adui atakapokuja kama mto , Roho wa BWANA atainua viwango dhidi yake.**" Isaya 59:19, KJV.

Maandiko hapo juu yanawasilisha maneno ya adui kama gharika inayokuja kuwachukua waaminifu. Joka kwa uongo wake alitaka kuwachukua malaika wote, lakini Mwana wa Mungu alidhihirisha utukufu wa Baba kama nuru ing'aayo na hii ikasababisha utengano katika maji kati ya malaika waliobaki juu na malaika walioshuka chini....(Mwanzo 1:6,7).

Kwa uchungu wa kukatishwa tamaa kwake Shetani ni theluthi moja tu ya malaika waliochagua kujitoa kikamilifu katika vita vyake dhidi ya Mungu na mtiwa-mafuta Wake.

> "**Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi**. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake." (Ufunuo wa Yohana 12:4).

Katika maono Yohana aliona ishara ya mwanamke aliye karibu kumzaa Kristo. Ingawa ishara za joka na nyota zinarejelea kiunabii kazi ya Shetani kupitia Rumi katika kuangamiza baadhi ya viongozi wa watu wa Mungu, pia hutupatia rejea ya chimbuko halisi la awali lililosababisha mchakato huo mbinguni.

Shetani alikuwa amewaambia malaika kwamba Mungu hatawasamehe na theluthi moja ya malaika walimwamini Shetani na kuingia kwenye kifungo cha mauti pamoja na Shetani.

> "Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu." (Yuda 1:6).

Sababu ya Mungu kusemwa kwamba amewaweka malaika hao katika "vifungo vya milele chini ya giza" ni kwa sababu Shetani aliwazuia malaika wasiamini kwamba wanaweza kumrudia Mungu.

> "uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache **giza na kuielekea nuru**, **waziache na nguvu za Shetani** na kumwelekea Mungu; kisha wapate **msamaha wa dhambi zao**, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi." Matendo ya Mitume 26:18.

> "Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa." (Mathayo 7:2).

Vifungo vya giza vilikuwa ni nguvu ya Shetani kwamba HAWATAPOKEA msamaha wa dhambi. Kwa kuamini uongo kwamba Mungu hawezi kuwasamehe basi waliaminishwa kwamba Mungu angewaangamiza. Kwahiyo jambo pekee ambalo wangeweza

tu kulitumainia ni adhabu ambayo walikuwa wamedai kwamba Mungu aitekeleze dhidi yao.

> "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; **bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.**" Waebrania 10:26-27.

Baadhi ya malaika - tofauti na wale theluthi moja ya malaika, walirudi kwa Mungu, maana mwanzo wa udanganyifu wa shetani mbingu iligawanyika nusu kwa nusu. Walikataa kukubali uongo kwamba Mungu hatasamehe. Walikubali ukweli wa tabia ya Mungu yenye rehema, upendo. Ingawa hawakuweza kujibu mashtaka yote ya Shetani, walichagua kubaki waaminifu kwa Mungu. Yesu alipokufa msalabani, njama za Shetani zilifichuliwa na hatimaye malaika walipata majibu waliyokuwa wakiyatafuta.

> "na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni." Wakolosai 1:20, KJV.

Kristo alipokufa, kulikuwa na mambo yaliyopatanishwa na Mungu mbinguni. Hatimaye, mawazo ya Shetani, ushawishi na mvuto wake viliondolewa mbinguni.

> "Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku." (Ufunuo wa Yohana 12:9-10).

Mpaka kufikia kipindi cha Msalaba, Shetani bado alikuwa na uwezo wa kwenda mbinguni. Uwezo wa Shetani kutembelea mbinguni uliruhusiwa tu kwa sababu kulikuwa na maswali ambayo yalikuwa hayajatatuliwa akilini mwa malaika. Jambo hili huthibitishwa katika kitabu cha Ayubu.

> "Ilikuwa, siku moja ambayo hao wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za BWANA, Shetani naye akaenda kati yao. BWANA akamwuliza Shetani, Umetoka wapi wewe? Ndipo Shetani akamjibu BWANA, na kusema, Natoka katika kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo." (Ayubu 1:6-7).

Yesu alipokuwa amekaribia kuuchukua Msalaba, alijua kwamba hivi karibuni Shetani angefunuliwa na angeanguka kama umeme kutoka mbinguni. Shetani hangekuwa na ushawishi wowote tena mbinguni, na hivyo hangekuwa na sababu ya kwenda huko tena.

> "Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme." (Luka 10:18).

Mwana wa Mungu alimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni katika umbo la mwili tangu mwanzo, lakini mawazo yake hayakuondoka mbinguni kikamilifu hadi Kristo alipokufa juu ya Msalaba. Bado imebakia kuonekana ni akina nani kutoka duniani watakaokubali ukweli wa tabia ya Mungu na kujiweka huru kutoka kwenye utawala wa mauti. Mwishoni mwa wakati, hivi karibuni, Mungu ataweka wazi pambano hilo kwa ulimwengu wote na mwanadamu atahitajika kufanya uamuzi, kama vile malaika walivyofanya uamuzi.

Ni upendo wa thamani kiasi gani kujua kwamba rehema za Mungu zinawafikia wote bure. Ingawa Shetani aliigawa mbingu nusu kwa nusu, bado masalio ya malaika hawa walirudi kwenye kifua cha Baba.

Ni huzuni kiasi gani iliyowapata Malaika kwa kuona pengo kubwa ambalo liliachwa wazi katika nyua za mbinguni. Wenzao wengi ambao walikuwa wameshiriki nao kumbukumbu za thamani walikuwa wametoweka. Jinsi gani malaika walivyoweza kulia kwa hasara hii kubwa iliyotokana na upotevu huu. Lakini ni nani anayeweza kupima hisia ya hasara ambayo Baba na Mwana waliipata? Wale waliowaumba, kuwalea, na kuwapenda malaika hawa. Uchungu, machozi, na mshtuko wa moyo lazima vilikuwa ni vitu visivyoweza kuchukulika kirahisi.

SURA YA 15

# JOKA AANZISHA MAKAZI YAKE DUNIANI

Je, Shetani alifukuzwa kutoka mbinguni? Au ni yeye mwenyewe aliamua kuhamishia nguvu zake kimkakati katika sayari ambayo mwanadamu angeumbwa?

> "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. **Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote**; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." Ufunuo wa Yohana 12:7-9.

Je, Mungu alimfukuza kutoka mbinguni kama kutupa takataka? Hili haliwezekani kwani tunapojua tabia ya Mungu tutajua:

> "Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; **maana dunia itajawa na kumjua BWANA**, kama vile maji yanavyoifunika bahari." Isaya 11:9.

Kuhusu Mwana wa Mungu Mandiko husema kwamba Yeye hana hila/jeuri yoyote na hivyo hana madhara kabisa.

> “Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.” Isaya 53:9.

> “**Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu**, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu;” Waebrania 7:26.

Je, ni kwa vipi sasa Shetani na malaika zake walitupwa? Tunaposoma katika Yuda 1:6, malaika hawa waliacha enzi yao ya kwanza. Ni nini basi kilichowafanya “watupwe” kutoka mbinguni?

> “Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake.”Ufunuo wa Yohana 12:4.

Mkia wa joka unawakilisha nini?

> “Mzee mwenye kuheshimiwa ndiye kichwa, **na nabii afundishaye uongo ndiye mkia**.” Isaya 9:15.

Nabii anayefundisha uongo wa Shetani na tabia mbaya ya Mungu amewafanya malaika wengi kumwona Mungu kama adui yao. Mungu alijaribu kuwaonyesha ukweli, lakini kila hatua ilionekana kwa malaika kama shambulio juu yao.

> “Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu; kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao.” Isaya 63:10.

Mwanamke anayeonekana mbinguni akiwa amevikwa jua na mwezi chini ya miguu yake ni nani? Mstari wa 4-6 unazungumza juu ya mwanamke aliyezaa mtoto wa kiume duniani ambaye angetawala mataifa na alinyakuliwa mbinguni. Adam Clarke anatoa ufafanuzi huu:

> Wafafanuzi wengi wanakubaliana Kwamba mwanamke hapa anawakilisha Kanisa la kweli la Kristo. Katika sehemu zingine za unabii, Kanisa safi la Kristo linaonyeshwa kama mwanamke. Katika Ufu 19:7, umati mkubwa unawakilishwa ukisema, “Na

> tufurahi na kushangilia, tukampe utukufu wake; kwa maana arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na Mkewe amejiweka tayari."

Kwa hakika ni kweli kwamba mwanamke safi anawakilisha bibi-arusi wa Kristo, Kanisa Lake pendwa.

> "Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili." Waefeso 5:23.

Kwa nini mwanamke huyu anaonyeshwa akiwa mbinguni katika mstari wa 1-3 na kisha katika mistari ya 4-6 baada ya joka kuja duniani, mwanamke huzaa mtoto wa kiume duniani?

Mpango wa dunia hii ulikuwa kufunua utukufu wa Mungu na Mwanawe. Tuliumbwa kwa sura yao. Wakaaji wote wa ulimwengu huu walipaswa kuwa bibi-arusi wa Kristo. Mwana wa Mungu alitamani kuwa na watu ambao wangeakisi kabisa tabia yake na tabia ya Baba yake. Katika uumbaji wa mwanamke kutoka katika ubavu wa Adamu, tumefunuliwa kanuni ya mwanamke, kanisa, lililotoka katika moyo wa Kristo. Mzaliwa wa Baba, Kristo ndiye ambaye angefanya mapenzi ya Baba yake aliye kichwa chake; wanadamu, ambao wamezaliwa na Kristo wangefanya mapenzi ya Kristo aliye Kichwa chao.

> "Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu." Marko 3:35.

> "Yesu akamwambia. Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu." Yohana 20:17.

Mwanamke, anayewakilisha watu wa Kristo ambao ndani yake kuna tabia yake, angevikwa Jua. Kristo ni Jua la haki, nuru ya ulimwengu. Hatima ya bibi-arusi wake ilikuwa kufunua ukweli wa tabia ya Mungu kwa ulimwengu.

Mazingira yanayoonekana ya Ufunuo 12 ni ya wakati wa kuzaliwa kwa Kristo miaka elfu mbili iliyopita. Mwanamke ni Kanisa la Mungu lililo karibu kumzaa Masihi. Joka anadhihirishwa kupitia mamlaka ya Kirumi na nyota ni viongozi wa watu wa Mungu waliouawa. Hata

hivyo kiini cha kisa hiki hupata chimbuko lake hapo mwanzo kabisa. Mungu na Mwana wake walikuwa wakipanga kumuumba mwanamke, bibi-arusi wa Kristo ili kuonyesha kwa ulimwengu wote uhusiano wa kweli uliopo kati ya Mungu na Mwana Wake. Lusifa hakujumuishwa katika mijadala kuhusu uumbaji wa ulimwengu huu. Majadiliano yalikuwa kati ya Mungu na Mwanawe tu kwa kuwa Mwana wa Mungu peke yake ndiye aliyejua ukweli wa tabia ya Baba yake.

> "Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, **asilolijua mtu ila yeye mwenyewe**." Ufunuo wa Yohana 19:12.

Ilikuwa ni tamaa ya Shetani kuwa mkuu wa ulimwengu huu. Pale Adamu na Hawa walipokabidhi utawala wao kwa Shetani, alipata cheo alichotaka.

> "Mimi sitasema nanyi maneno mengi tena, kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu." Yohana 14:30.

Shetani alitaka kuonyesha kanuni zake za serikali pamija na mfumo wake mpya wa haki katika dunia hii, lakini Mungu alimruhusu Mwanawe awe muumbaji na mtawala halali wa ulimwengu huu.

> "Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. **Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele**, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa." Danieli 7:13-14.

Kile alichokiona nabii Danieli katika maono ni utimizwaji wa mpango wa awali ambao Baba alikuwa nao tangu mwanzo; kwamba Mwanawe angekuwa mtawala wa dunia. Kabla ya Mwana wa Mungu kuumba dunia hii, Shetani alihamisha majeshi yake yote kwenye eneo la dunia ili kujitayarisha kumeza na kuchukua mateka kile ambacho Kristo alikuwa karibu kukiumba.

> “Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake.” Ufunuo wa Yohana 12:4.

Kisa cha kuzaliwa kwa Kristo miaka 2000 iliyopita ni udhihirisho wa kile kilichotokea kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu huu. Yesu alipozaliwa, Shetani alijaribu kumwangamiza na kudai ulimwengu huu kuwa utawala wake halali.

Kristo alipokuwa karibu kuumba ulimwengu huu na kumleta bibi-arusi Wake duniani, Shetani alisimama tayari kuupokonya kutoka katika utawala wa Mwana wa Mungu. Ajabu ya yule mwanamke aliyepangwa, kukusudiwa, na kubuniwa mbinguni, alikuwa sasa tayari kuletwa duniani kutoka kwenye mikono ya Kristo Muumbaji wake.

> “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.” Mwanzo 1:1.

Mara tu Mwana wa Mungu alipoumba mahali hapa panapoitwa dunia, Shetani alijaribu mara moja kumiliki mahali hapo kwa maana katika mwanzo kabisa palikuwa na giza mahali hapa.

> “Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.” Mwanzo 1:2.

Tunajua giza hili halikuwa jema kwa sababu Mungu hakuliita giza kuwa jema. Aliita nuru peke yake kuwa ni njema.

> “Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza.” Mwanzo 1:3-4

Mungu ni nuru. Shetani ni giza. Uwepo wa giza ambalo halikuitwa jema linatuambia kwamba Shetani joka alikuwa amekuja duniani akiwa tayari kumeza kile ambacho Mwana wa Mungu alikuwa akikiumba na kujifanya kuwa mkuu wa ulimwengu huu.

Kisa cha uumbaji si mfululizo wa hatua zisizokuwa na mpangilio maalumu. Uumbaji ni dhihirisho la uzao ulio ndani ya Mwana wa Mungu na pia ni ufunuo wa pambano kati ya uzao wa Kristo na uzao wa nyoka.

Tunakumbuka kwamba sheria ya uzima haitumii nguvu ya kulazimisha. Mungu hakumlazimisha Shetani kwa njia yoyote ile. Hakuzuia harakati zake kwa njia yoyote. Hivi ndivyo sheria ya uhuru inavyofanya kazi.

Ushahidi mwingine wa uhuru huu unafunuliwa katika ukweli kwamba ingawa Shetani na malaika zake walimwasi Mungu lakini waliendelea kuishi, hawakuishi kwa nguvu zao wenyewe. Kuna mmoja tu ambaye hafi na huyo ni Mungu. Malaika hawa waliendelea kuishi kama kawaida huku wakipokea uzima uliokuwa ndani ya Kristo.

> "Mara moja amenena Mungu; Mara mbili nimeyasikia haya, Ya kuwa nguvu zina Mungu," Zaburi 62:11.

Kristo aliendelea kuwapa uhai malaika hawa walioanguka. Kila mdundo wa maisha waliokuwa nao, ulitoka kwa Kristo. Yeye na Baba yake waliendelea kuwa na uwezo wa kusoma kila wazo walilokuwa nalo. Walijua kila wazo na tendo la chuki la Shetani dhidi yao. Bado Mungu aliwapa uzima. Kwa nini ilikuwa hivi?

Kwanza, kama tulivyoona Mungu hawezi kuua. Pili, malaika wengi bado walikuwa na maswali ambayo hayajatatuliwa na hivyo wakati ulihitajika kutolewa ili Shetani aendeleze mawazo yake na kuona matunda yake. Kwa sababu hiyo, Mwana wa Mungu analazimika kusikia na kutazama uchafu na maneno ya hila ya malaika hawa walioanguka. Huu ni msalaba ulioje kwa Kristo kuubeba. Kristo angali amemshikilia Shetani mikononi mwake kwa njia fulani, huku Shetani akimpiga makofi, kumjeruhi, kumdhihaki na kumuumiza Mwana wa Mungu. Kumbuka hili:

> "Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, ...ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote." Matendo ya Mitume 17:24-25.

Baba na Mwana huendelea kumpa Shetani uhai ili kanuni zake ziweze kufichuliwa na kanuni zao za kutotumia nguvu kamwe zidumishwe. Shetani anatumia maisha hayo kuiba, kuua na kuharibu. Kristo ni hekima na nguvu za Mungu. (1Kor 1:24). Shetani huchukua nguvu na kukataa hekima. Shetani anajifanya kichwa ngumu sana dhidi ya Mwana wa Mungu na huku kila pumzi ya uhai wake hutoka kwake.

Kila wakati Shetani anapoangamiza ni kama fimbo iliyokuwa mkononi mwa Musa ambayo ilipowekwa chini, ilikuwa nyoka.

> "BWANA akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo. Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake. BWANA akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;)" Kutoka 4:2-4.

Kristo ni fimbo katika mkono wa kuume wa Baba. Mungu anapomruhusu Shetani kuharibu, nguvu ndani ya Kristo inaruhusiwa kutoka na kwenda kwa Shetani kufanya matendo haya maovu. Mwana wa Mungu hapendi kufanya hivi, lakini kwa sababu ya uhuru wa kuchagua lazima aruhusu nguvu hizi kwenda kwa Shetani. Kila wakati Shetani anapoua na kuharibu mmoja wa watoto wa Mungu, Kristo anachomwa kwa maumivu ya msalaba. Amejeruhiwa kwa makosa haya.

Kwa nini hamzuii Shetani kufanya hivi? Kwa sababu Shetani mwenyewe anaelewa kanuni ya uhuru wa kuchagua, na anadai kwamba wanadamu wapokee matokeo ya matendo yao na kutawaliwa na mungu wa chaguo lao ambaye, ikiwa wanatenda dhambi, ni Shetani, anayewatawala kwa kuwadanganya, na kuwachochea, kuwatesa, na hatimaye kuwaangamiza. Kristo hawezi kumzuia Shetani kuwatesa wale wanaokataa kutembea katika sheria ya Bwana na kushika sheria na hukumu zake. Anaweza tu kuwasihi warudi kwake ili kutoka kwenye njia yenye madhara.

Wengine wanaweza kuhoji hapa kwamba wasio na hatia pia wanaumizwa; Mungu anaelezaje hilo? Watoto wengi wanateseka chini ya vita, au baba walevi, au serikali za kikatili nk. Neno muhimu hapa ni chini ya. Mungu alitengeneza mfumo wa hiari ambapo matendo na imani ya kila mmoja wetu ingeathiri wale walio karibu nasi. Hili ni kweli hasa tunapokuwa na mamlaka; kila tunachofikiria na kufanya kitakuwa na athari za moja kwa moja kwa wale walio chini yetu. Hii ilikuwa ni kutusaidia sisi na malaika kuelewa nafasi yetu wenyewe, na nafasi ya wale walio juu na chini yetu, katika mlolongo mkubwa wa uwepo wetu; na kwamba matendo yetu hayatuathiri sisi wenyewe tu bali yanafanya kazi katika uhusiano na kila kitu kingine. Wanadamu

na malaika wanapochagua kumkataa Kristo, si kwamba hujiumiza wao wenyewe tu, bali kila mtu anayewazunguka.

Baada ya Shetani na malaika zake kukimbia kutoka mbinguni, Mungu na Mwana Wake waliamua kusonga mbele na kuumba ulimwengu huu. Sehemu kubwa ya ulimwengu (universe) mzima ilikuwa imeathiriwa na uongo wa Shetani na mfumo wake wa haki wa uongo kuhusiana na sheria ya Mungu. Mungu na Mwanawe walitazamia kwa matumaini kwamba ukweli wa tabia ya Mungu uliofunuliwa katika jamii ya wanadamu; bibi-arusi wa Mwana wa Mungu, angeweza kusaidia kujibu mashtaka ya Shetani dhidi ya Mungu. Lakini hawangezuia harakati za Shetani.

Shetani alikuwa huru kuzunguka-zunguka katika maeneo ya ulimwengu mpya ulioumbwa. Chuki yake kwa Mwana wa Mungu ilimsukuma kuja mahali hapa na kujaribu kupatawala. Hii ndiyo sababu ya giza lililokuwepo siku ya kwanza ya uumbaji. Shetani alikuja hapa pamoja na malaika zake katika maandalizi ya yale yatakayokuja.

Vizuizi juu ya Shetani vilikuja kutoka kwenye mfumo wake wa haki na kile alichowazia Mungu angemfanyia. Uumbaji mpya haungekuwa na chochote cha kuogopa kutoka kwa Shetani ilimradi tu wangebakia wamejazwa na Roho wa Kristo. Asingeweza kukaa muda mrefu mbele yao bila ya haja ya kukimbia. Angetupiliwa nje na usadikisho wa dhati wa imani na hofu ya adhabu.

SURA YA 16

# UNABII WA JUMA LA UUMBAJI

Pambano kati ya Shetani na serikali ya Mungu lilikuzwa kikamilifu katika uzao wa nyoka. Ni Mungu tu na Mwanawe walijua mwisho wa mambo haya ungekuwa nini. Mungu katika hekima yake, kupitia matukio ya uumbaji, aliweza kufichua vipengele vya uzao katika Kristo na uzao uliokuwa ndani ya Shetani. Baba yetu aliweza kuweka kwa kanuni kile ambacho kingetokea katika pambano hili kati ya ufalme wa Mungu na ufalme wa Shetani.

Hatima ya ulimwengu huu haikuamriwa kuwa jukwaa kuu ambapo pambano hili lingefanyikia, lakini mlolongo wa uumbaji unaeleza hatua muhimu za pambano kati ya Kristo na Shetani. Ni hakika kwamba uzao wa nyoka ungepata mahali pa kudhihirisha kanuni zake, lakini haikujulikana kwa hakika kwamba dunia hii kwa huzuni ingekuwa ndipo mahali ambapo zingedhihirika, kwa kuwa Mungu ni mwenye hekima yote lakini si mjua yote. Tofauti, kama tulivyojadili, inapatikana katika kujua mwisho tangu mwanzo. Yaliyoko kabla ya mwanzo hayajui. Hayajulikani na kwa hiyo yanahusisha kipengele cha matazamio.

Kabla ya Lusifa kujitolea kuasi kikamilifu dhidi ya Muumba Wake, Roho wa Mungu alikuwa akitembea juu ya mioyo ya malaika ili kuwavuta kutoka kwenye njia ambayo wengi walikuwa wakielekea. Kisa cha uumbaji kinaonyesha ukweli huu.

> "Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji." Mwanzo 1:2

Neno la Kiebrania linalomaanisha vilindi (kina kirefu) lina maana ya maji mengi. Udhalimu wa Shetani wa upotoshaji wa sheria ya Mungu kupitia uongo wake kuhusu kutokufa ulikuwa unasababisha ghasia miongoni mwa malaika. Alikuwa amejiweka kama kielelezo cha jinsi ya kuishi, tofauti na Mwana wa Mungu. Roho wa Mungu alikuwa akitembea juu yao, akihimiza dhamiri zao zisikilize maneno ya Mwana wa Mungu na malaika waaminifu.

Lusifa alikuwa akimlaumu Mungu na serikali yake, lakini Kristo alikuwa nuru ya mbinguni ambaye alifunua ukweli wa tabia ya Mungu. Lusifa alikuwa akihimiza kwamba haki ilidai kifo kwa ajili ya makosa, lakini Kristo alidhihirisha kwamba Baba hakutaka dhabihu na kafara kwa ajili ya dhambi.

> "Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza.Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja." Mwanzo 1:3-5

Mungu hakusema "fanya iwe nuru." Alisema "iwe nuru." Hili ni jambo tunalopaswa kuliweka katika akili zetu na kupokea kwa shukrani. Shetani aliikataa nuru; na ikiwa jicho lako linatiwa giza, halitaki na kisha haliwezi kupokea nuru, basi ulimwengu unaokuzunguka unaweza kuwa giza jinsi gani?

> "Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!" Mathayo 6:22-23

Kama tulivyosema katika sura iliyotangulia, Mungu aliita nuru kuwa njema. Hakuliita giza kuwa jema. Hapa kuna ushahidi wa hadithi ambayo inafunuliwa katika matukio ya uumbaji. Mungu alitenganisha nuru na giza. Katika kufunua ukweli wa Baba yake, Mwana wa Mungu alifichua giza lililokuwa ndani ya Shetani.

Maneno aliyosema Mwana wa Mungu yalibebwa na Roho yake katika nia za malaika na ilitambua mawazo yao na matamanio yao (Waebrania 4:12). Roho ni kama mkondo wa upepo unaotenganisha. Hivi ndivyo tunavyoona katika anga: anga hewa kati ya maji juu ya dunia na maji ya chini ya dunia.

> "Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji. Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo. Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili." Mwanzo 1:6-8

Matokeo ya ufunuo wa nuru ni kuleta uamuzi. Je, kutakuwa na kukubalika kwa nuru au kutakuwa na kujiepusha kutoka kwenye nuru[30] na kusababisha utengano? Tunaona kwa shauku kwamba Mungu hasemi kwamba kutenganishwa kwa maji ni jambo jema bali tu kwamba ndivyo ilivyokuwa. Hii ndiyo kanuni ya mbegu iliyofunuliwa katika uumbaji. Tutaona mchakato huu tena katika siku ya nne na ya tano ya uumbaji. Kwa mara nyingine tena, nuru huangaza siku ya nne na kuna utengano siku ya tano. Tutakuja katika hili hivi punde. Hoja yetu kutoka siku ya pili ya uumbaji ni kwamba Roho wa ukweli anagawanya. Yesu alieleza kanuni hiyo alipokuwa duniani.

> "Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake." Mathayo 10:34-36

Mungu anawasihi walio gizani wamgeukie Yeye. Kuendelea kuusihi moyo daima kunaufanya ulainike au kuwa mgumu daima. Hivi ndivyo Mungu alivyoufanya moyo wa Farao kuwa mgumu; Mungu aliendelea kumwomba aulainishe moyo wake na Farao alikataa mara kwa mara. Hiki ndicho husababisha kutengana.

Siku ya tatu inapanua utengano ulioanza siku ya pili ya uumbaji. Inafunua zaidi juu ya maendeleo ya uzao wa Kristo na uzao wa Shetani.

---

[30] Maana ya neno la kiebrania usiku linamaanisha "kwenda kinyume mbali na nuru". Kwa njia ya kitamathali inamaanisha dhiki.

> Mungu akasema, [1] Maji yaliyo chini H8478] ya mbingu na [2] yakusanyike [H6960] mahali pamoja, na [3] nchi kavu [H3004] ionekane; ikawa hivyo. Na Mungu akaiita nchi kavu Dunia; na kusanyiko la maji akaliita Bahari, Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mwanzo 1:9-10 (KJV).

Neno la Kiebrania "*chini*" linamaanisha:

> H8478 tachath (*takh'-ath*) - chini, (kama huzuni) kutoka H8430 tôach (*to'-akh*) - huzuni, unyenyekevu.

Kwa kukataa kwake kuwa mwana kwa Mungu, Shetani alikuwa mtu wa huzuni. Vipengele vya tabia yake vilianza kuteteleka na kutikisika. (Mwanzo 4:12). Wale walioungana naye katika kukataa uwana wao kwa Mungu, walijikuta wamefungwa pamoja na Lusifa. Maneno "kukusanyika pamoja" kwa Kiebrania humaanisha:

> H6960 qâvâh; (*kaw-vaw'*): Mzizi wa awali; kuunganisha pamoja (labda kwa kupotosha), yaani, kukusanya; (kwa lugha ya mfano) kutarajia: - kukusanya (pamoja), tazama, subira, ngoja, subiria (kwa, endelea, juu ya).

Shetani na malaika zake kwa pamoja walijitenga mbali na nuru ya kweli katika Mwana wa Mungu. Walijawa na hasira, jeuri, wivu, na hukumu dhidi ya Mungu na Mwana wake. Pia walijawa na kutazamia kwa hofu hukumu. Tunaona mbegu hii ya Shetani ikidhihirika kwa Adamu na Hawa walipotenda dhambi. Mungu alipowaendea bustanini, walikimbia na kujificha kwa hofu. Walifungwa na woga, hatia na uadui kwa Mungu. Mbegu hii inaonyeshwa zaidi kwa njia hii.

> "Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya BWANA, Na juu ya masihi wake," Zaburi 2:2

Kwa hiyo, udhihirisho wa nuru una matokeo ya kuwafunga malaika walioanguka kutokana na mwitikio wao dhidi ya ile nuru. Ni hofu yao wenyewe na hukumu, katika kukabiliana na nuru, ambayo inawafanya watumwa na kuwakusanya pamoja.

> "Huyafunga maji ndani ya mawingu yake mazito [GIZA]; Na hilo wingu halipasuki chini yake." Ayubu 26:8

> "Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu." Yuda 1:6

Tunaona hofu ambayo malaika walioanguka huidhihirisha pale Mwana wa Mungu anapokuja mbele yao.

> "Na tazama, wakapiga kelele, wakisema, Tuna nini nawe, Mwana wa Mungu? Je! Umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?" Mathayo 8:29

Siku ya tatu ya uumbaji inafunua kukusanyika pamoja kwa maji yaliyo chini. Hii inawakilisha Shetani na malaika zake wakiwa wameunganishwa pamoja katika chuki yao kwa Mungu na Mwana Wake na hofu yao ya hukumu inayokuja. Kisha tunaona kwamba kukusanyika pamoja kwa maji kuliruhusu nchi kavu kuonekana.

> Kisha Mungu akasema, "Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, na nchi kavu [H3004] na ionekane"; na ikawa hivyo. Mwanzo 1:9

Hapa tunaona kanuni ya mbegu ya kufikiwa kwa Shetani. Katika kukusanya majeshi yake pamoja dhidi ya Bwana na mpakwa mafuta wake, nchi kavu, kutokea kwa mwanamke, iliruhusiwa kuonekana na katika nchi hii kavu mbegu, ambayo ni Kristo, iliwezeshwa kupandwa.

> Mungu akasema, "Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi;" ikawa hivyo. Mwanzo 1:11

Neno la Kiebrania la nchi kavu linachukua mada ya njia ya wokovu kwa njia zifuatazo.

> "Aligeuza bahari ikawa nchi kavu; ;[H3004] Katika mto walivuka kwa miguu; Huko ndiko mlikomfurahia." Zaburi 66:6

> "Lakini wale watu wakavuta makasia kwa nguvu, ili wapate kurudi pwani, [H3004] wasiweze; kwa maana bahari ilizidi kuwachafukia sana." Yona 1:13

Ijapokuwa Shetani na malaika zake walikuwa wameazimia kuifanya dunia kuwa makao yake makuu na kukatiza mipango ya Mungu na

Mwanawe, mfumo wao wenyewe wa haki, chuki dhidi ya Kristo na hofu yao iliyofuata kwake iliwazuia kumzuia Kristo kudhihirisha nchi kavu na kupanda mbegu. Mbegu iliyodhihirishwa siku ya tatu ya uumbaji ni ishara ya Kristo.

> Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, "Kwa wazao," kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, "Kwa mzao wako", yaani, Kristo. Wagalatia 3:16

Tunafuata kanuni hii kwa uangalifu kwani ni onyesho la injili. Kristo alipofunua ukweli wa Baba yake kama ulivyoonyeshwa katika siku ya kwanza ya uumbaji, ilisababisha utengano kati ya malaika. Kisha Shetani akakusanya majeshi yake na kuhamia duniani ambako "wanainuka ... juu ya BWANA na juu ya Masihi wake." (Matendo 4:26, NIV). Kina cha dhambi kinaanza kufichuliwa giza linapozidi pale linapokusanyika, na kusababisha neema kuwa nyingi zaidi ambayo inaruhusu mbegu kupandwa katika ardhi.

Mwanadamu aliumbwa kwa mavumbi ya dunia na siku ya tatu ya uumbaji ni ishara ya mbegu ya Kristo iliyopandwa katika mioyo ya wanadamu iwavutao kwenye nuru ya ukweli. Ni ishara ya Roho wa Yesu akiendelea kumsihi mwanadamu kujisalimisha kwenye nuru. Kama vile ambavyo Roho haonekani, kitendo cha mbegu ndani ya moyo wa mwanadamu hakionekani. Kitendo chake kimefichwa hadi kitakapoonekana.

Kwa muhtasari, tunaona kwamba muundo wa siku ya tatu ya uumbaji unafuata mpangilio huu:

> "Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi;" Warumi 5:20

Tukiiweka aya hii katika muktadha wa uumbaji tunaona:

- Siku ya 1 - Nuru: "Zaidi ya hayo sheria [tabia] iliingia"
- Siku ya 2 - Kutengana: "Ili kosa liwe kubwa sana"
- Siku ya 3a - Maji yalikusanyika pamoja: "Lakini dhambi ilipozidi"
- Siku ya 3b - Mbegu inapandwa: "Neema ilikuwa nyingi zaidi"

Warumi 5:20 hutuonyesha mpangilio wa mwingiliano kati ya mbegu ya shetani na mbegu ya Kristo.

Kupitia kanuni ya mbegu, tunaweza kuona kwamba uumbaji wa ulimwengu huu unafichua asili ya Pambano Kuu kati ya Kristo na Shetani.

| | | |
|---|---|---|
| Siku ya 1<br>Ukweli ulifunuliwa<br>Giza kutokana na uongo wa sheatani kuhusu tabia ya Mungu.<br>Kristo anafunua ukweli wa tabia ya Mungu.<br>Na iwe nuru. | Siku ya 2<br>Utengano<br>Shetani na malaika zake wanaiacha mbingu.<br>Wanampinga Roho na kukataa kutubu<br>Maji kugawanywa. | Siky ya 3<br>Mbegu<br>Maji ya chini yanakusanyika pamoja. Hili linaruhusu Dunia kuonekana. Mbengu inapandwa.<br>Njia kupitia baharini. Mbegu inaleta uhai. Mzizi katika nchi kavu. |
| Kuingia kwa sheria/tabia | Kosa likawa kubwa | Neema ikawa kubwa zaidi |
| Vita mbinguni kabla ya dunia kuanza | Vitambinguni muda mfupi kabla ya dunia kuanza | Anguko la Mwanadamu mpaka kuzaliwa kwa Kristo |

Siku tatu za kwanza za uumbaji ni ufunuo wa vita iliyotukia mbinguni iliyopelekea Shetani na malaika zake kuja duniani ili kupinga Uzao unaokuja. Mfuatano huu wa matukio unaweza kupatikana katika maneno ya Yesu katika Yohana 16:8

> "Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu." Yohana 16:8

| | | |
|---|---|---|
| Usadikisho: | Dhambi | Haki |

Matukio haya pia yameelezwa katika lugha ya Ufunuo 12:1-4

| Siku ya 1 | Siku ya 2 | Siku ya 3 |
|---|---|---|
| Ukweli ulifunuliwa<br>Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.<br><br>Nuru ilidhihirishwa | Utengano<br>Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa.<br><br>Maji kufumuka | Mbegu<br>Ikaonekana ishara nyingine mbinguni: na tazama joka kubwa jekundu… Mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni na kuziangusha katika nchi. Na Yule Joka akasimama mbele ya Yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo amle mototo wake. |

Tunaona akidhihirishwa hapa mwanamke, nyoka/joka, na Mzao. Hii ni tafakari ya matukio yaliyotukia katika bustani ya Edeni ambapo tunamwona mwanamke, joka, nyoka na mzao.

> "nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." Mwanzo 3:15

Lengo kuu la vita hivi kama inavyoonyeshwa katika siku tatu za kwanza imejikita huko mbinguni. Siku ya nne ya uumbaji ni ufunuo wa kazi inayoonekana ya Kristo duniani ambapo tabia ya Mungu ilifunuliwa kikamilifu. Kufichuliwa kwa nuru hii duniani, kulianza mchakato ule ule kama ule uliokuwa umetukia mbinguni hapo mwanzo, kwa uwazi zaidi, na kusababisha dhambi kuwa kubwa sana ili kwamba neema iweze kuwa nyingi zaidi.

> "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza." Yohana 1:4-5

> "Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:12

Huduma ya Yesu ilisababisha utengano kati ya watu wa Mungu.

> "Basi wakamshutumu, wakasema, Wewe u mwanafunzi wake yule; sisi tu wanafunzi wa Musa. Sisi tunajua ya kuwa Mungu alisema na Musa; bali yule hatujui atokako." Yohana 9:28-29

> Naye Yesu akasema, "Nimekuja ulimwenguni kwa ajili ya hukumu, ili wale wasioona wapate kuona, na wale wanaoona wawe vipofu." Yohana 9:39 (NASB)

Kazi ya Kristo iliwafanya wale waliomkataa Roho wa Mungu wakusanyike pamoja dhidi ya Kristo ili wamuue.

> "Na ilipokuwa asubuhi, wakuu wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu, wapate kumwua;" Mathayo 27:1

> "Basi tangu siku ile walifanya shauri la kumwua." Yohana 11:53

Matendo ya Shetani na hawa waovu yaliunganishwa pamoja katika mawingu mazito ya giza.

> "Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa." Mathayo 27:45

Katika kumuua Kristo, dhambi za Shetani na viongozi zilifunuliwa. Walijidhihirisha wenyewe na mbegu ya ukweli iliweza kugusa moyo wa mwanadamu. Dhambi ya kumwua Kristo Msalabani ilisababisha neema kuwa nyingi zaidi kwa sababu kazi za giza zilifichuliwa.

> "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye [Kristo] naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi," Waebrania 2:14

Nuru ambayo Kristo alidhihirisha kwa ulimwengu ilifichua giza lililokuwa ndani ya maji yaliyokusanyika pamoja. Pia ilifunua mkuu wa uwezo wa anga, (Waefeso 2:2). Kazi za malaika (roho safi) na mapepo (roho wachafu) zililetwa kwenye nuru.

Shetani alipomuua Kristo, Shetani alianguka kama umeme kutoka mbinguni. Hakuwa na uwezo tena wa kuufikia ufalme wa mbinguni kama alivyokuwa hapo awali. Hakuna malaika mbinguni aliyeathiriwa na mawazo yake tena. Malaika wote wa mbinguni walipatanishwa na Mungu kupitia ufunuo wa nuru katika maisha ya Kristo iliyofananishwa na uumbaji wa jua na mwezi katika siku ya nne ya uumbaji.

> "Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku." Ufunuo wa Yohana 12:9-10

Matukio yaliyoelezewa katika mistari hapo juu yanalenga wakati wa ufufuo wa Kristo. Mawazo ya Shetani yalitupwa nje ya akili za ulimwengu wa mbinguni. Shetani alitupwaje hapa chini?

> **...tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu**; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; 2 Wakorintho 10:5

Ilikuwa ni hoja za Shetani na wafuasi wake ambazo zilitupwa kutoka mbinguni wakati wa ufufuo wa Kristo. Malaika wa mbinguni si wadhalimu, na kama Mungu na Mwana Wake walivyo hawatumii nguvu. Shetani alikuwa ameondoka mbinguni kimwili wakati wa kuumbwa kwa dunia kama inavyoonyeshwa katika Ufunuo 12:4. Mawazo ya Shetani yalitupwa kutoka mbinguni miaka 4000 baadaye wakati nuru ya Mwana wa Mungu ilipofunua utukufu wa Baba.

> "Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume." Ufunuo wa Yohana 12:13

Shetani alipoona kwamba amepoteza ushawishi wake mbinguni, alielekeza fikira zake kwa wakazi wa dunia tu na kuamua kumwangamiza bibi-arusi wa Kristo.

> "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari." Ufunuo wa Yohana 12:17

Sasa dunia ingepitia hatua zile zile tatu ambazo mbingu ilikuwa imezipitia kama ilivyoonyeshwa katika siku tatu za kwanza za uumbaji.

> Mungu akasema, Maji na yatoe kwa wingi kiumbe chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. Mungu akaumba nyangumi wakubwa, [H8577] na kila kiumbe chenye uhai kiendacho, ambacho maji yalijawa kwa wingi kwa jinsi zao, na kila ndege arukaye kwa jinsi zake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mwanzo 1:20-21 (KJV)

Katika siku ya tano ya uumbaji kiumbe mmoja hupewa jina maalum wakati wengine hupewa kwa maneno ya jumla. Neno la Kiebrania kwa nyangumi mkubwa linamaanisha nini?

> [H8577] (Aina ya pili iliyotumiwa katika Ezekieli 29:3); yenye nguvu sawa na H8565; mnyama wa baharini au wa nchi kavu, yaani, nyoka wa baharini au mbweha: - joka, hayawani wa baharini, nyoka, nyangumi.

Kabla ya Kristo kuja, malaika na hasa wanadamu walikuwa na uelewa mdogo juu ya Shetani na matendo yake. Nyangumi mkubwa, au nyoka/joka, anayeogelea ndani ya maji yaliyokusanywa pamoja anawakilisha Shetani.

> "Katika siku hiyo BWANA, kwa upanga wake ulio mkali, ulio mkubwa, ulio na nguvu, atamwadhibu lewiathani, nyoka yule mwepesi, na lewiathani, nyoka yule mwenye kuzonga-zonga; naye atamwua yule joka [H8577] aliye baharini. Isaya 27:1 (KJV)

Je! ni upanga gani ambao Bwana anatumia?

> [Kristo] alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kulia, na upanga mkali wenye makali kuwili ulitoka kinywani mwake, na uso wake ulikuwa kama jua liking'aa kwa nguvu zake." Ufunuo 1:16

> “Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Waebrania 4:12

Yalikuwa ni kwa maneno ya upendo na rehema tuliyoambiwa na Kristo ambayo kwa hayo joka alifichuliwa. Matendo yake ya huruma na upole yalionyesha ukweli wa maneno Yake. Haya yalimfunua joka katika bahari ambayo imekusanywa pamoja katika giza lililofananishwa na siku ya tatu ya uumbaji.

Katika kukamata kwa Shetani jamii ya wanadamu, jamii ya wanadamu imewasilishwa kama samaki ambao Kristo anatafuta kuwavua na kuwaokoa kutoka kwa joka katika maji.

> “Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.” Mathayo 4:19

Kwa hiyo maji ya bahari yana viumbe safi na najisi. Ndege wa angani wana viumbe safi na najisi. Hizi zinaashiria utengano kati ya wale wanaoyapokea maneno ya Kristo na wale wasioyapokea. Yesu alisema hivi kuhusiana na wanafunzi:

> “Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia.” Yohana 15:3

Siku ya tano na ya sita inaashiria utengano unaoendelea kati ya wale wanaomfuata Mwana-Kondoo asiye na udhalimu, mtakatifu na asiye na unajisi, na wale wanaokataa maneno ya Kristo na kuinuka na kula nyama.

> “Na tazama, mnyama mwingine, wa pili, kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyo hivi, Inuka, ule nyama tele.” Danieli 7:5

> “Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, Umpende jirani yako kama nafsi yako. Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana.” Wagalatia 5:14-15

Wale wanaojazwa na roho chafu ya Shetani watafanya, kama bwana wao anavyokula nyama nyingi. Tunaona katika maono ya Danieli, kwamba mnyama anayewakilisha mojawapo ya falme za ulimwengu huu aliinuka na kula nyama nyingi. Falme zinazotawala za ulimwengu huu huishi kwa kuua wengine. Kula nyama ni kiwakilishi cha matendo ya Shetani.

Tofauti na Roho wa Kristo asiye na ubinafsi, roho ya Shetani ina sifa ya ubinafsi - kile ambacho Shetani anataka kufanya, anafanya, bila kujali maumivu anayosababisha kwa wengine. Hatimaye anachotaka Shetani ni kuwaangamiza wengine; wale anaowameza wamethibitishwa kuwa dhaifu kuliko yeye na hivyo anajisikia vizuri zaidi.

> "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." 1 Petro 5:8

> "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo." Yohana 8:44

Mwana wa Mungu hatendi jeuri wala hali nyama. Tunaona kwamba Kristo ni kinyume na Shetani. Kristo hasemi uongo na wala haui. Kwa habari zaidi kuhusu hili tazama vitabu hivi ***Acts of Our Gentle God*** na ***Agape*** vinavyopatikana katika *fatheroflove.info*

> "Mwanzi uliopondeka hatauvunja, Wala utambi utokao moshi hatauzima, Hata ailetapo hukumu ikashinda. Na jina lake Mataifa watalitumainia." Mathayo 12:20-21

> "......Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake." Isaya 53:9

Utengano kati ya samaki, ndege, na viumbe vya nchi kavu vilivyo safi na samaki, ndege, na viumbe vya nchi kavu ambavyo ni najisi vinawakilisha uwezo wa kutenganisha wa injili, kama vile ulivyo mgawanyo wa maji katika siku ya pili na siku ya tatu ya uumbaji.

> “Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.” Wagalatia 5:17

Sio bahati mbaya kwamba siku ya sita ya uumbaji mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Mwanamume na mwanamke wako katika mfano wa Mungu na Mwanawe. Pale sura ya tabia ya Mungu inaporejeshwa basi kunakuwa na kuingia katika pumziko la sabato.

> “Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake.” Waebrania 4:9-10

| Siku ya 4 | Siku ya 5 | Siku ya 6 |
|---|---|---|
| Ukweli ulifunuliwa<br>“ Mimi ni nuru ya ulimwengu ”<br>Kristo anafunua ukweli wa tabia ya Mungu.<br>Jua, mwezi na nyota vinaangaza dunia | Utengano<br>Samaki na ndege wanatokea. Wengine safi na wengine najisi.<br>Joka anafunuliwa | Sura ya Mungu<br>Wanyama na Binadamu walifunuliwa kuwa kama safi au najisi. Wanakula nyama au wanaishi bila kuwa na madhara na wenye kujali.<br>Mcheni Mungu na Kumtukuza. |
| Sheria/tabia inaingia | Kosa likawa kubwa sana | Neema ikawa ngingi zaidi |
| Maisha ya Kristo duniani | Kutoka uangamivu wa yerusalemu mpaka mwishio wa zama za giza na siku 1260 | Siku za mwisho. Kristo anadhihirishwa ndani ya wanadamu. |

Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kusemwa kuhusu juma la uumbaji, lakini lengo letu hapa ni kwa Mungu kusimulia kisa cha namna ambavyo mbegu mbili zingejidhihirisha zenyewe na utengano ambao ungetokea. Kwa mara nyingine tena, tunarudia kusema, hilo halikuamriwa au kupangwa litokee duniani, bali Mungu angeweka

wazi kwa ulimwengu kielelezo cha jinsi mambo ambavyo yangetokea kutokana na yale ambayo Mungu aliyajua kutokana na kusoma mawazo ya Shetani akiyalinganishwa na ya Mwana Wake.

Upatanisho wa malaika wa mbinguni wakati Kristo alipokuja duniani na kufunua tabia ya Baba Yake na tabia ya Shetani utajirudia wakati, mwishoni mwa historia ya dunia, wale 144,000 watakapoonyesha kikamili tabia ya Kristo.

> "Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao." Ufunuo wa Yohana 14:1

Bibi arusi anajiweka tayari. Wale wanaozishika amri za Mungu na imani ya Yesu wataonyesha ulimwengu jinsi tabia ya Mungu inavyoonekana. Ulimwengu wote utaamua wenyewe ni nani watamtumikia. Shetani atatupwa nje ya fikira za wale wanaomfuata Mwana-Kondoo wa Mungu popote anapowaongoza.

Itatangazwa:

> "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo wa Yohana 22:11

Ndipo Kristo atakuja kudai watoto wake. Waovu waliotiwa muhuri wa tabia ya Shetani, wanatishwa na ujio wa Kristo na malaika zake duniani. Wanaangamizwa na mng'ao wa kuja kwake, (2 Wathesalonike 2:8). Ni hatia ya dhambi pamoja na hofu yao ya Mungu ambayo inawalemea. Mungu hawaangamizi kwa kutumia nguvu bali wanakandamizwa na ujira walioupata. Uovu utawaangamiza waovu, (Zaburi 34:21).

Kuna maelezo zaidi katika hadithi hii ya mwisho wa dhambi lakini ningependa kutaja wazo hili la kuvutia. Siku sita za kwanza za uumbaji hufuata mzunguko wa mchana na usiku. Lakini siku ya saba usiku hautajwi. Mwishoni mwa pambano kati ya wema na uovu tunaambiwa:

> “Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.” Ufunuo wa Yohana 22:5

Siku ya saba inaonyesha pumziko ambalo huja kwa ulimwengu baada ya pambano na giza kumalizika. Wote waliosalia watampenda Mungu kwa mioyo yao yote na wanajua kwamba ndani yake hamna giza lolote. (1 Yohana 1:5).

SURA YA 17

# KUUMBWA KWA MFANO WA MUNGU

Shetani na malaika zake, ingawa mwanzoni walikuwa tayari kumkiri Mungu Baba, walikataa kukubali mamlaka na uongozi wa Mwana wa Mungu. Shetani alijigamba kwamba angefanana na Aliye Juu Zaidi, akimaanisha Baba. Alikana kwamba Mwana wa Mungu alikuwa sawa na Baba. Kwa kadri mbegu ya uasi huo inavyoendelea kujitokeza, tunaona picha wazi ya masuala yanayohusika.

> …**ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba**. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka. Yohana 5:23

Urithi wa Mwana wa Mungu kutoka kwa Baba yake unathibitisha kwamba usawa hauwezi kupimwa kwa nguvu, utukufu na akili. Urithi wa Mwana wa Mungu ni uthibitisho mkuu kwamba Baba ni pendo; kwamba kwa asili Yeye mtoaji.

> "Baba ampenda Mwana, naye amempa vyote mkononi mwake." Yohana 3:35

Shetani alichagua kupuuzia urithi wake kutoka kwa Kristo lakini badala yake alijivunia hekima, nguvu na utajiri wake. (Tazama Yeremia 9:23; Ezekieli 28:17). Mwana wa Mungu alipopokea kila kitu kutoka kwa Baba Yake, ibada kwa Mwana wa Mungu ikawa suala lisilovumilika kwa Shetani. Kumwabudu Mwana wa Mungu ilikuwa ni ukumbusho wa daima kwamba vitu vyote vinatoka kwa Baba na kutokea kwake tumevipewa sisi.

Ni katika muktadha huu ndipo tunaweza kufahamu kikamili zaidi sababu iliyomfanya Mungu kuwaumba Adamu na mke wake kwa mfano wa Mungu. Utawala ambao Mungu alikuwa nao juu ya Mwana Wake ungeonyeshwa katika utawala ambao Adamu alikuwa nao juu ya mke wake, ambaye baadaye alimwita Hawa.

> "Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu." 1 Wakorintho 11:3

Mbele kidogo tunajifunza jinsi ambavyo utawala wa Adamu ungetumika kuwafundisha malaika kuhusu somo la mamlaka.

> "Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, **kwa ajili** ya malaika." 1 Wakorintho 11:10

Neno kwa hiyo (sababu) hapo juu linatokana na neno la Kiyunani διά - ambalo linamaanisha mkondo wa kitendo. Linaweza pia kutafsiriwa kama:

> baada ya, daima, kati ya, saa, kuepuka, kwa sababu ya (hiyo), kwa ufupi, kwa, **kwa ajili** (sababu)... mbele, kutoka, ndani, **kwa tukio la, la, kwa sababu ya, kwa ajili**, kwamba, kwa hiyo, X ingawa, kupitia (-nje), hadi, kwa hiyo, na (-ndani).

Tunaweza kutafsiri kifungu hiki kama:

1. Kwa ajili ya Malaika
2. Kwa sababu ya Malaika
3. Kwa kusudi la Malaika

Kwa kutazama uhusiano kati ya Adamu na Hawa, malaika wanaweza kujifunza vizuri zaidi msingi wa serikali ya kimungu mbinguni.

> "…..Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru;" Warumi 1:19-20

Biblia inatuambia ni nani aliyeumba ulimwengu huu.

> …na kuwajulisha wote jinsi ulivyo ushirika wa siri hiyo, ambayo tangu zamani za kale ilikuwa imefichwa katika **Mungu aliyeviumba vitu vyote kwa Yesu Kristo**. Waefeso 3:9

> ...mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, **tena kwa yeye aliufanya ulimwengu**. Waebrania 1:2

Baba na Mwanawe ndio walioumba ulimwengu huu. Baba ndiye alikuwa chanzo na Mwanawe alikuwa njia ambayo kupitia kwake uliumbwa. Hii inaongeza umuhimu mkubwa kwa aya ifuatayo.

> Mungu akasema, **Na tumfanye mtu kwa mfano wetu,** kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mwanzo 1:26

Mungu alipoumba vitu vyote kupitia Mwanawe, ni dhahiri kwamba Mungu aliposema "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu" kwamba Mungu alikuwa akizungumza na Mwanawe. Paulo yuko sahihi anaposema kwamba hatuna udhuru kwa swali hili kwa sababu Adamu na Hawa ni viumbe wawili, mmoja akitoka kwa mwingine. Sifa zisizoonekana za Mungu zinaonekana wazi katika uumbaji wa mwanamume na mwanamke.

> Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mwanzo 1:27

Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake, kila mmoja katika umbo na sura yake binafsi pamoja na ukweli kwamba kulikuwa na nafsi mbili. Fundisho la Utatu linaharibu taswira hii. Linaficha ukweli wa uhusiano kati ya Mungu na Mwanawe. Linaharibu mojawapo ya mambo muhimu zaidi ambayo Mungu alitaka kuufundisha ulimwengu.

Mungu hakuumba watu watatu walio sawa katika bustani kuwakilisha sura ya Mungu. Aliumba watu wawili na mmoja akitokea ndani ya mwingine. Urahisi wa hili ni dhahiri kwa wote ambao wako tayari kulipokea.

BWANA Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Mwanzo 2:21-23

Hawa alitolewa kutoka kwa Adamu kama mfano wa ukweli kwamba Mwana wa Mungu alitolewa kutoka kwa Baba.

Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, **wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako**, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Yohana 17:8

Yesu akawaambia, Kama Mungu angekuwa baba yenu, mngenipenda mimi; kwa maana nalitoka kwa Mungu, nami nimekuja; wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma. Yohana 8:42

Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Mithali 8:24

Lakini wewe, Ee Bethlehemu Efrata, ni kijiji kidogo tu kati ya watu wote wa Yuda. Lakini mtawala wa Israeli atakuja kutoka kwako, ambaye asili yake ni kutoka zamani za kale. Mika 5:2 (NLT)

Hawa alitoka kwa Adamu na bado yuko sawa na Adamu. Hapo mwanzo kulikuwa na mwanamke na mwanamke alikuwa kwa binadamu na mwanamke alikuwa binadamu. (Angalia mfanano huu katika Yohana 1:1).

mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa. Mwanzo 5:2

Kama vile Kristo alivyo mng'ao wa utukufu wa Baba, vivyo hivyo mwanamke ni mng'ao wa utukufu wa mwanamume.

...Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha

> kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; Waebrania 1:3

> “Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. **Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume**.” 1 Wakorintho 11:7

Kama vile Mungu alivyoujaza ulimwengu kupitia Mwanawe, ndivyo ambavyo Adamu angeijaza dunia kupitia mke wake. Kama vile ambavyo Mwana wa Mungu alivyofanya vionekane vile visivyoonekana kwa Mungu, vivyo hivyo Hawa angefanya uonekane uzao ambao haukuonekana katika Adamu.

Uhusiano wa Adamu na Hawa ulipaswa kuwa kitabu cha mafundisho kwa ulimwengu kuelewa uhusiano wa kweli wa Mungu na Mwanawe.

> …mambo hayo, ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo hayo malaika wanatamani kuyachungulia. 1 Petro 1:12

Mwanaume alimgawia mke wake vyote alivyopewa. Alizungumza maneno ya upendo, baraka na furaha juu yake. Alitamani kumtunza kama sehemu yake mwenyewe. Alihisi kuwa na jukumu la kumtunza kwa sababu alikuwa ametoka kwake.

Hawa alishiriki utawala aliopewa Adamu; alirithi yote ambayo Mungu alikuwa amempa. Usawa wake na mwanamume haukujengwa juu ya nguvu kwani mwanamume aliumbwa akiwa na nguvu kuliko mwanamke. Haukutegemea urefu kwa maana mwanaume alikuwa mrefu kuliko mwanamke. Haukutegemea umri kwani mwanamume aliumbwa kabla ya mwanamke. Hata hivyo wote wawili walikuwa binadamu sawa.

Maelewano yangekuwepo kati ya mwanamume na mwanamke kwa kadri ambavyo hawakuweka thamani yao juu ya sifa zao za asili bali juu ya uhusiano walioshiriki pamoja. Mwanamke ndiye peke yake katika bustani aliyekuwa na uwezo wa kumjua mwanaume. Hakuna mnyama yeyote aliyekuwa na uwezo wa kuthamini shangwe na

matarajio ya Adamu. Kama vile Mwana asemavyo juu ya Baba yake ndivyo Hawa peke yake angeweza kusema.[31]

> Kama vile Baba [Adamu] anijuavyo Mimi, vivyo hivyo nami namjua Baba [Adamu]… Yohana 10:15

Hawa hakufikiri kuwa vibaya kuwa sawa na Adamu. Alishiriki ubinadamu wake; aliumbwa kutokana na ubavu uliokuwa ndani yake. Hakuwa na wazo la haja ya kujilinganisha naye, wala haikuingia akilini kwamba alihitaji kusisitiza sifa zake za asili ili kumvutia mwanaume huyo. Alijitosheleza katika utambulisho wake kama mwenye tumbo la uzazi (womb-man), akitoka katika tumbo la mwanamune.

Kutoka kwa mwanamume na mwanamke wa awali walioumbwa kwa mfano wa Baba na Mwana, dunia ingejazwa na mamilioni ya familia zilizofanywa kwa mfano wa Mungu, zikiwakilisha Baba na Mwana na kuwafundisha malaika zaidi jinsi ambavyo uhusiano kati ya Baba na Mwana ulivyo.

Ni hatima ya thamani kiasi gani ilitolewa kwa jamii ya wanadamu. Ni upendo gani ulikuwa umewekezwa katika uumbaji huu. Mwanamume na mwanamke walipewa uhuru uleule uliokuwa ndani ya moyo wa Mwana wa Mungu. Mwana mzaliwa wa pekee hangeweza kutoa chochote zaidi ya kile ambacho Yeye mwenyewe alikuwa amekipokea. Mwanamume na mwanamke walikuwa huru kuchagua kumtumikia Mungu na kuakisi tabia Yake au kuchagua njia tofauti.

Kuchagua njia tofauti sio mchakato rahisi kivile. Unahitaji kutoamini wema wa Mungu, vipawa vyake vya ajabu, na kukana kwamba ametoa uhuru kamili ndani ya ukweli huo. Inahitaji mpokeaji kuamini uongo juu ya Mungu ili kuhalalisha kuvunja uhusiano wake na Yeye; kuamini kwamba maisha yetu yangekuwa bora zaidi bila Mungu, mbele ya uthibitisho wote unaotuonyesha kwamba kutegemea hekima yetu wenyewe kutatusababishia kujiangamiza.

Baba yetu wa mbinguni ni uzima, upendo, uhuru, na furaha. Amejaa wema na ukweli. Yeye ni mwingi wa rehema na neema, na ni

---

[31] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na hili tazama kitabu *Original Love* kinachopatikana katika fatheroflove.info

mvumilivu wa ajabu na mpole. Mungu hangeacha ubinadamu ingawa ilionekana, hasa kwa malaika, kwamba ubinadamu ulikuwa umekata tamaa juu Yake. Baba yetu alikuwa na mpango.

Baba yetu alikuwa ameuunda uumbaji kwa njia ambayo ingemsaidia mwanadamu kujielewa mwenyewe na uhusiano wake na Mungu. Alikuwa amempa Adamu uhusiano fulani na ardhi ili kutoa hoja kuhusu uhusiano wa Mungu mwenyewe na uumbaji Wake. Kwa sababu ya ukweli kwamba kulikuwako katika ulimwengu mtazamo mpya wa ukweli, Bustani ya Edeni ingeonyesha ukweli huu. Mfumo mpya wa haki wa Shetani ulikuwa umeathiri ulimwengu mzima. Theluthi moja ya malaika walijitolea kufuata kanuni hizi za ufalme mpya. Upendo lazima utoe uhuru wa kuchagua.

SURA YA 18

# UTAWALA KATIKA BUSTANI YA EDENI

Ilikuwa vema na ya kuvutia kiasi gani kuishi katika bustani ya Edeni. Paradiso hai, iliyojaa manukato mazuri ya upendo, amani, na furaha. Akiwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu na Mwanawe, mwanamke alipata pumziko katika kifua cha mumewe; kama ukumbusho wa alikotoka; mahali salama na tulivu zaidi kwake kukaa.

> …Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua. Yohana 1:18

Mungu alimpa Adamu na mke wake mbaraka. Ulijumuisha mambo matano muhimu:

> Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, "**Zaeni**, **mkaongezeke**, **mkaijaze** nchi, na **kuitiisha**; **mkatawale** samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi." Mwanzo 1:28

Kuzaliana ni zaidi ya furaha ya kuzaa watoto kwa sura yako mwenyewe. Mbaraka wa Mungu wa kwanza kabisa ulikuwa kuzaa matunda ya Roho .

> Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Wagalatia 5:22-23

Katika uhusiano waliopewa mwanamume na mwanamke, kulikuwa na fursa ya kukuza uzuri kama huo wa tabia. Kipengele cha kwanza na cha thamani zaidi ni upendo, upendo wa Agape. Tabia ya kupenda kwa uhuru, utu wema na upole ya Mwana wa Mungu iliandikwa katika kila nyuzi ya akili, moyo na nafsi ya Adamu na mke wake. Katika kukawia kwake kumuumba mwanamke kutoka kwa mwanamume, furaha na hazina iliongezeka ya kuwa na mwanamke akitembea naye, kuzungumza naye na kushiriki naye safari yake ya maisha.

Kila asubuhi, mwanamume huyo angetoa shukrani zake kwa Mungu, nyakati ziingine machozi yakibubujika, kwa ajili ya hazina ya mke wake. Akiwa amejazwa na Roho wa Mwana wa Mungu, basi angemmwagia maneno ya upendo, na fikra za jinsi anavyomthamini, zikiunganishwa na matendo ya fadhili na mapenzi ya dhati.

Hili lingepanda mbegu za kiroho katika moyo wa mwanamke huyo na kuzidisha shangwe yake katika kujua kwamba alithaminiwa, alikubaliwa na kupendwa na mume wake. Tamanio lake la kumtumikia, kumpendeza na kuleta furaha kwa mumewe lingeongezeka na katika ushirika wa upendo wao, tabia ya mwanamume na mwanamke ingeongezeka katika tunda la Roho. Wangezidi kukua katika neema kupitia mwangwi wa uhusiano wao kuhusiana na kazi waliyopewa na Mungu na shukrani zao kwa Mungu.

Nafsi ya mwanadamu ina uwezo wa kupitisha na kupokea masafa ya mtetemo. Utafiti wa kisayansi wa Manfred Clynes[32] ulionyesha uwezo wa mtu wa kutoa masafa yanayounganishwa na hali ya kihisia anayokumbana nayo. Masafa yaliyotolewa kwa ajili ya upendo, fadhili, furaha au ibada yalionekana kuwa marefu na ya taratibu. Masafa yanayohusiana na chuki na hasira yalionekana kuwa mafupi na makali. Kutokana na hili tunaweza kujifunza kwamba tunda la Roho likidhihirika ndani ya mtu hutoa masafa ambayo yangejaza bustani nzima.

Kama ambavyo Mwanamume na mwanamke walivyoumbwa kwa kutumia udongo uleule wa dunia yenyewe, masafa waliyotoa ambayo

[32] https://en.wikipedia.org/wiki/Manfred_Clynes

yalipatana na sheria ya Mungu yangeleta matokeo chanya na yenye kuzaa matunda kwenye mazingira. Majaribio mengi yamefanywa kuonyesha athari za kuzungumza na mimea na wanyama kwa maneno ya wema na kujali.

Kinyume na hili, nafsi ya mwanadamu ina uwezo wa kutoa masafa ambayo huathiri vibaya mazingira.

> Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Wagalatia 5:19-21

Orodha hii ya mawazo na matendo hasi ni zao la kuvunja sheria ya Mungu. Sheria ya Mungu ambayo ni sheria ya uhuru haitoi masafa yanayoharibu dunia. Siri ya mwanamume na mwanamke kuzaa na kuongezeka na kuijaza dunia kwa wema ingepatikana katika mkondo unaoendelea wa upendo, furaha, shukrani, subira, fadhili na wema unaoshuka kutoka katika akili na mioyo yao hadi kwa ulimwengu unaowazunguka.

Uthibitisho wa uhusiano huu kati ya mwanadamu na dunia unaweza kugunduliwa kwa upande mbaya kupitia athari kwenye bustani kupitia dhambi ya Adamu, pamoja na athari juu ya dunia kupitia mauaji ya Kaini ya kumuua Abeli ndugu yake.

> Akamwambia huyo mtu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mkeo, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema, usile, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula matunda yake siku zote za maisha yako, nayo miiba na michongoma itakuzalia, nawe utakula mboga za shambani. Mwanzo 3:17-18 (YLT)

Nimenukuu tafsiri ya "Young's Literal" kwa madhumuni ya kuonyesha kwa nini dunia ililaaniwa. Tafsiri nyingi zinaonyesha kwamba Mungu aliilaani ardhi ili kuwafundisha somo. Bado ukweli ni kwamba ardhi ingelaaniwa kupitia kwa masafa yasiyo sahihi yanayotolewa kutoka kwa Adamu na mke wake. Maneno makali yangeathiri mimea kutoa miiba na michongoma mikali. Mambo haya yanatokana na hali ya dhambi ya mwanadamu, badala ya Mungu

kumwadhibu mwanadamu kwa kuumba vitu hivi kama wengine wanavyofikiri.

Angalia athari juu ya dunia pale Kaini alipomuua Abeli:

> Kaini akamwambia Habili nduguye, [Twende uwandani]. Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua. BWANA akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. Mwanzo 4:8-12

Hisia za chuki zilizopelekea Kaini kufanya mauaji ziliharibu rutuba ya dunia. Kabla tu ya kifo cha Abeli, uchungu, mshtuko na huzuni katika mwili na akili yake katika utambuzi wa kile Kaini alichomfanyia pia ilimezwa na ardhi na kuiharibu, kiasi kwamba isingeweza kuzaa kwa kiwango sawa na ilichopaswa kuzaa hapo awali.

Bustani ya Edeni ilikuwa sehemu ndogo tu ya dunia. Adamu na Hawa walipokuwa wazuri zaidi katika tabia, wangezaa watoto katika sura hii. Watoto wangelelewa katika mazingira yenye manukato mazuri ambapo maneno ya upendo na huruma pekee yangesemwa na hakuna mitetemo mibaya ambayo ingegusa akili au miili yao.

Ni hatima nzuri kiasi gani ilikuwa imepangwa kwa jamii ya wanadamu. Dunia nzima ingekuwa imejaa upendo, shangwe, na baraka. Maua, matunda, miti, na bustani zingejaza dunia yote. Kadri ambavyo mwanadamu angekuwa na tabia ya kupendeza zaidi, ndivyo ambavyo dunia chini ya utawala wake ingeakisi jambo hili.

Jinsi tunavyoelewa maneno matatu ya kwanza ya kivitendo katika Mwanzo 1:28 itaamua muktadha wa maneno mawili ya mwisho ya kivitendo.

> Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, "**Zaeni**, **mkaongezeke**, **mkaijaze** nchi, na **kuitiisha**; **mkatawale** samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. Mwanzo 1:28

Yesu alipokuwa duniani, mara kwa mara ilimbidi kujaribu na kuwaongoza wasikilizaji wake kutoka kwenye mawazo ya mwili hadi mawazo ya Roho. Yesu alipomwambia Nikodemo kwamba lazima azaliwe mara ya pili, wazo la kwanza ambalo Nikodemo alieleza lilikuwa kuzaliwa kwa asili ya kimwili. Lakini Yesu alikuwa anazungumza mambo ya kiroho.

> Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho. Yohana 3:6-8

Yesu alionyesha kwa wanafunzi wake kwamba kuchukulia mambo katika ufahamu wa kimwili kwanza ni matokeo ya moyo mgumu.

> Akawaagiza, akasema, Angalieni, jihadharini na chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode. Wakabishana wao kwa wao, kwa kuwa hawana mikate. Naye Yesu akatambua, akawaambia, Mbona mnabishana kwa sababu hamna mikate? Hamfahamu bado, wala hamjaelewa? Je! Mioyo yenu ni mizito? Marko 8:15-17

Hebu tuangalie kwa makini baadhi ya mawazo ya wafafanuzi:

> …kama hii si amri ya wazi, kama Wayahudi wanavyoielewa, kwa ndoa na uzazi wa watoto, inaonekana kuwa ni zaidi ya ruhusa tupu; angalau ni mwelekeo na ushauri kwa kile kilichofaa na kinachofaa **kwa ongezeko la wanadamu, na kwa ajili ya kuijaza dunia wakaaji**, ambao ulikuwa hatima ya mwisho wa kufanywa kwake. — Isaya 45:18 . John Gill Commentary

> Aliwatia alama kuwa wako chini ya ulinzi wake maalum, na akawapa **uwezo wa kueneza na kuzidisha aina zao** duniani. — Isaya 45:18 . Adam Clarke Commentary

Tukichukua maneno zaeni na kuzidisha/kuongezeka katika ufahamu wa kiroho wa tabia, basi tutakuwa na utambuzi wa wazi zaidi wa nini kinapaswa kuijaza dunia na jinsi inavyotiishwa na nini maana ya kuitawala.

Tukiangalia maneno *kuitiisha* na *kutawala* katika Kiebrania, tuna nyanja zifuatazo za maana:

> Kutiisha [H3533] kâbash
>
> kuwekanyagia chini; hivyo katika hali hasi kupuuza; katika hali chanya kushinda, kupindua, kukiuka: - kuleta katika utumwa, kulazimisha, kuweka chini, kutiisha, kuwa chini ya.
>
> Utawala [H7287] râdâh
>
> kukanyaga, yaani kupindua; haswa ili kubomoa: - (kuja, fanya) kuwa na mamlaka, shinda, tawala, (kubeba, fanya) tawala, (-tawala, juu), chukua.

Katika hali ya kimwili, andiko hili linaweza kusomeka kama vile Mungu anampa Adamu mamlaka ya kukanyaga dunia na kutiisha na kulazimisha kutii amri zote za chini za uumbaji. Katika Roho, andiko hili linatimizwa katika maisha ya Yesu alipozungumza na upepo na mawimbi na kuyaamuru yatulie. Amri hii haikuwa ya mabavu au nguvu, ilikuwa ni kumtoa Roho huyo ndani yake ambaye alijawa na amani na utulivu. Mazingira yanayomzunguka Kristo yalitiisha kila kitu kilichomzunguka kupitia amani, upendo, na furaha.

Adamu na mke wake walipaswa kuijaza dunia kwa tabia yao ya kujitolea na ya upole. Wanyama na viumbe vinatiishwa si kwa mjeledi au amri ya nguvu bali kupitia mzunguko wa upendo, utulivu, na maelewano.

Roho wa Yesu ni Roho wa uhuru, uhuru usio na kizuizi. (Yohana 8:36). Njia pekee ya kuitiisha dunia na kuwa na mamlaka katika muktadha huu ni kuangaza angahewa hii kwa wote katika nyanja iliyotolewa. Kwa wale walio na masikio ya kusikia na wasikie utawala wa asili ulihusu nini hasa.

SURA YA 19

# PARADISO ILIYOPOTEA

Nje ya bustani hii nzuri, joka alikuwa akitembea juu na chini akiwaza ni jinsi gani angeweza kuwaangamiza wanandoa hawa wanaovutia waliofanana na Mungu na Mwanawe katika umbo, sura na tabia. Kwa namna iliyo sawa na jinsi ambavyo nuru iling'aa juu ya uso wa Musa kwa kutazama kwake uzuri wa tabia ya Mungu, Adamu na mkewe waling'aa kwa utukufu wa Mungu; nembo halisi ya hekima ya Mungu iliyodhihirika ndani yao.

> Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele. Danieli 12:3

Kama tulivyogundua katika Ufunuo 12:4 kuhusu kuzaliwa kwa Kristo, joka alisimama tayari kummeza Mtoto mara tu atakapozaliwa. Katika kuzaliwa kwa Kristo, tunaona udhihirisho wa kile kilichotokea hapo mwanzo. Kristo alikuwa ametoka tu kuzaliwa ndani ya mioyo ya Adamu na mke wake.

> ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni **Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.** Wakolosai 1:27

Ingawa waliishi katika miili iliyokamilika, Adamu na Hawa walianza kukua katika hekima na kimo cha kiroho na kupendwa na Mungu na

malaika. Kupitia njia ambayo Shetani alimtumia Herode tunapata taswira ya mambo yaliyotokia hapo mwanzo.

> Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie. Mathayo 2:7-8

Herode alitumia udanganyifu kutafuta njia ya kufika mahali ambapo Kristo alizaliwa. Alijifanya kuwa na hamu ya kumwabudu mtoto Yesu lakini nia yake ya kweli ilikuwa kumuua.

Tunakumbuka kwamba malaika walipaswa kujifunza mambo kuhusu Baba na Mwana kupitia Adamu na mke wake. Kama vile mamajusi walivyokuja kutoka nchi ya mbali kuleta zawadi za kumbariki na kumtegemeza Yusufu, Mariamu na Yesu, ndivyo malaika walivyokuja kutoka bara la mbinguni wakiwa wamebeba baraka na zawadi kwa Adamu na Hawa, wanandoa walioumbwa hivi karibuni. Kwa namna sawa na jinsi mamajusi walivyopiga magoti katika kumwabudu Masihi, malaika walistaajabia Adamu na mke wake, wale walioumbwa kwa mfano wa Mungu, na walizingatia wema na hekima ya Muumba wao. Katika uchunguzi wa Adamu na Hawa, malaika wangejifunza ukweli kuhusu Baba na Mwana.

Je, Shetani aliwashutumu malaika hao waliokuwa wakienda na kurudi kutoka katika bustani hiyo ili wamruhusu apate kuingia kwa wanadamu wapya ili kuwaangamiza? Kama wale mamajusi, je, malaika walitiwa moyo wasimshirikishe Shetani katika mazungumzo walipokuja na kwenda kwenye bustani ili kushirikiana na Adamu na mke wake?

Inapendeza kutambua kwamba mamajusi walitoka mashariki. Ni muhimu pia kwamba neno hili hili la Kiyunani linalozungumzia bustani ambayo Mungu aliipanda hapo mwanzo katika Septuagint, tafsiri ya Kigiriki ya Agano la Kale.

> Baada ya Yesu kuzaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi kutoka Mashariki[G395] walifika Yerusalemu. Mathayo 2:1

> BWANA Mungu akapanda bustani upande wa **mashariki**[G395] **katika Edeni**, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. Mwanzo 2:8

Kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa kitabu hiki, neno la Kiebrania linalomaanisha mashariki linabeba pia maana ya mambo ya kale au ya nyakati za kale. Tunaona hapa kiungo cha kuunganisha kati ya mamajusi wakati wa Kristo na malaika waliokuja na kuwatembelea wanandoa wapya.

Kuhusu zawadi walizoleta; zawadi ya dhahabu iliwakilisha kujengwa kwa imani, (1 Petro 1:7) iliyojaribiwa hivi punde katika moto wa vita iliyokuwa imetokia mbinguni. Katika huduma ya patakatifu, ubani uliochanganywa na unga na mafuta ulifanyiza dhabihu ya chakula, (Mambo ya Walawi 2:1). Ilikuwa ni utambuzi wa nani aliye chanzo cha uzima, mkate wa uzima, (Yohana 6:48). Mkutano wa malaika pamoja na wanadamu uliwaruhusu kuwafundisha kuhusu masuala ya Pambano Kuu kati ya Kristo na Shetani. Mafuta ya manemane yalitoa ishara ya uwepo wa kimungu walipokutana pamoja. Kwa kweli, hazina za mamajusi kutoka nchi ya mbali zilithibitika kuwa baraka kwa Yusufu na mke wake.

Kwa kadri ambavyo Adamu na mkewe walienenda katika tabia ya Mungu wao; maadamu Kristo alikuwa anakaa ndani yao kwa imani, Shetani hangeweza kuwashambulia wala kuwasumbua. Kama vile kitabu cha sheria cha Kumbukumbu la Torati kinavyoeleza:

> Itakuwa utakaposikia sauti ya BWANA, Mungu wako, kwa bidii, **kutunza kuyafanya maagizo yake yote** nikuagizayo leo, ndipo BWANA, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani; na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya BWANA, Mungu wako. Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo. **BWANA atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako; watakutokea kwa njia moja, lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.** Kumbukumbu la Torati 28:1-2,6-7

Ingawa Shetani hangeweza kupata nafasi ya kuwafikia moja kwa moja wenzi hao watakatifu, Shetani alipewa nafasi ya kukaa mahali pa

katikati ya bustani ambapo Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ulipokuwa.

> BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. Mwanzo 2:16-17

Roho wa Yesu daima ni Roho wa uhuru. Hakuwezi kuwa na uhuru bila kuchagua. Kama vile kulivyokuwako katika ulimwengu uwepo wa ufalme mwingine, udhihirisho wa ufalme huo lazima uwepo. Ili kuwatayarisha watoto wake kwa ajili ya uhalisia wa maisha, Hakuwahifadhi kwa njia ambayo isingewapa nafasi ya kukuza tabia kwa kuchagua haki.

Kwa kadri ambavyo Adamu na mke wake waliuepuka mti uliokuwa katikati ya bustani, walikuwa wakikuza tabia na kutumia chaguo lao la kumpenda na kumtumikia Mungu. Shetani angeweza kutoa masafa yake ya chuki, hasira na huzuni kutoka katikati ya bustani, lakini upendo kwa neno la Mungu na ngao ya imani ungewalinda wawili hao watakatifu kutokana na madhara.

Biblia inatuambia:

> Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa. 1 Timotheo 2:14

Kwa hivyo, Huthibitisha ukweli wa kauli:

> Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua! Mhubiri 4:9-10

Jinsi Adamu na mkewe walivyotengana hatukuambiwa. Hekima iliyoonyeshwa kutoka kwa Sulemani katika kifungu hapo juu ni udhihirisho wa mbegu iliyokuwepo tangu mwanzo. Lilikuwa jambo la hekima kwa Adamu na mke wake kukaa pamoja. Halikuwa jambo la busara kuwa peke yake kwenye bustani wakati ambapo Shetani angeweza kutoa ushawishi wa masafa yake kutokea kwenye Mti wa ujuzi. Mtazamo wa Adamu juu ya kile kilichokuwa kikifanyika ulikuwa mpana zaidi kuliko mtazamo wa Hawa; alikuwa amepewa

amri ya awali ya kuepuka tunda la mti uliokatazwa kutoka kwa Kristo kabla ya Hawa kuumbwa, ambayo Adamu kisha akamhabarisha mke wake. Kama jinsi Kristo alivyoishi chini ya ulinzi wa Baba yake, ndivyo Hawa alivyokuwa akiishi chini ya ulinzi wa Adamu. Angebarikiwa na mwongozo wake kama angekuwa naye.

Huenda wengine wakahoji, kwa nini Mungu aliwaleta Adamu na mke wake katika mazingira ambayo yalikuwa na vigezo kadhaa vya hatari? Swali laweza kuulizwa, kwa nini wazazi huwaleta watoto katika ulimwengu uliojaa hatari? Kwa nini kuruhusu watoto kucheza kwenye uchafu au kuendesha baiskeli au idadi yoyote ya mambo ambayo yana hatari? Ukweli wa ulimwengu ni kwamba kulikuwa na adui ambaye alitaka kuharibu yale ambayo Mungu na Mwana wake walikuwa wakiyafanya. Njia pekee ya kuishi katika mazingira haya ilikuwa ni kwa shetani kupewa fursa ndogo ya kuwafikia ili kuweza kuchagua dhidi yake na hivyo kusitawisha tabia ya kweli. Kupewa fursa kwa Shetani pia kungetoa tofauti katika tabia ya Mungu na tabia ya Shetani. Hili pia lingewasaidia kutambua na kuelewa kwa nini Mungu na Mwanawe walikuwa wema sana, na kwa nini dhambi ilikuwa ni hatari sana.

Kadiri Hawa alivyokuwa akisonga mbele kuelekea katikati ya bustani na kadiri alivyokuwa mbali zaidi na Adamu, ndivyo alivyokuwa karibu na masafa ambayo Shetani alikuwa akiyatoa kutoka katika Mti wa ujuzi.

Sababu ya nyoka kuwezeshwa kutumiwa na Shetani ni fumbo. Nyoka, au joka, alikuwa kiumbe mzuri mwenye mabawa. Nyoka huyu alikuwa mmoja wa viumbe waliokuwa chini ya utawala wa Adamu. Shetani hangeweza kumtumia nyoka kwa ajili ya makusudi yake bila kuwepo kwa udhaifu fulani katika utawala wa Adamu. Je, inawezekana kwamba Hawa kutengwa na Adamu kuliwezesha udhaifu huu? Ilikuwa ni wajibu wa Adamu kumtunza mke wake. Je, kupuuzia wajibu huo wa kumtia moyo kukaa karibu naye pia kulituma masafa kwenye bustani na kuathiri viumbe wengine? Ni vigumu kusema ndivyo, lakini mwanamke huyo alipomsikia nyoka akizungumza naye, alionekana kuakisi mawazo yake ya ndani.

> Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, “Ati!

> Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" Mwanzo 3:1

Ingekuwa jambo la kushangaza kuona nyoka akiongea naye. Hawa alikuwa ameonywa juu ya ujio wa malaika huyu mbaya, lakini alikuwa akitazamia malaika amshukie pasipo kutambua angeweza kutumia njia ya udanganyifu ya nyoka. Shetani alijua kwamba Hawa angeshangazwa na jambo hilo na angeweza kusoma lugha ya mwili wake.

Mawazo, mihemko na hisia za Hawa pia zilizalisha masafa ambayo Shetani angeweza kuyasoma. Hakujua mawazo yake haswa, lakini alishangazwa na namna alivyoulizwa.

Katika kumjibu Hawa anazidisha maneno ya Mungu, akionyesha wasiwasi wake.

> Mwanamke akamwambia nyoka, "Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa." Mwanzo 3:2-3

Mungu hakuwa amesema "Msiyaguse." Alikuwa amesema tu "hupaswi kula." Kuligusa ingekuwa hatari lakini hili lisingesababisha kifo. Kula tu tunda hilo kungesababisha kifo. Hawa aliongeza kwenye ujumbe ambao Adamu alimwambia kuhusu kile ambacho Mungu alikuwa amekisema.

Hivi ndivyo Musa alivyoandika kuhusiana na kile ambacho Mungu alimwambia Adamu:

מוֹת תָּמוּת׃

Alichosema Mungu kiliandikwa katika mfumo wa kitenzi cha Kiebrania kinachoitwa Qal imperfect. Maana yake ni kwamba Mungu alikuwa amesema kwamba kula matunda ya mti huo kutaanzisha mchakato unaopelekea kwenye kifo. Neno Musa aliloliandika kwa ajili ya 'kufa' katika Kiebrania lilileta maana zifuatazo katika umbo la Qal:

1. (Qal)

1a1) kufa
1a2) kufa (kama adhabu), kuuawa
1a3) kufa, kuangamia (kwa taifa)
1a4) kufa kabla ya wakati (kwa kupuuza mwenendo wa busara wa maadili)

Neno hilo linaweza kumaanisha kuuawa au linaweza kumaanisha kufa mapema kwa kupuuza mwenendo wa kiadili wenye hekima. Je, Adamu alitafsirije kile ambacho Mungu alikisema? Hivi ndivyo Musa alivyoandika kuhusiana na Hawa alivyomwambia nyoka.

פֶּן־תְּמֻתוּן׃

Mabadiliko kidogo kwenye maneno aliyoyasema Hawa kulileta maana kwamba ukila tunda lazima ufe.

Hivi ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa.

לֹא־מוֹת תְּמֻתוּן׃

Alisema kwamba “Si lazima ufe.” Alichoambiwa na Shetani kilikuwa sahihi kiufundi wakati huu. Mungu alikuwa amesema mtaangamia lakini Hawa alikuwa amesema ni lazima ufe na Shetani akamwambia hili si sahihi. Kuangamia ni matokeo ya asili ya matendo yako mwenyewe. “Lazima ufe” inamaanisha kwamba matokeo yanahitaji matumizi ya nguvu mbaya kutoka kwenye chombo cha nje. Kisha Shetani anaongeza uongo huu:

> kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanzo 3:5

Shetani alimwambia Hawa kwamba angepatwa na hali ya kutokufa kwa kula matunda ya mti huo na pia kwamba angepata ujuzi sawa na wa Mungu; ujuzi wa mema na mabaya. Ukweli ni kwamba Mungu hakuwa na ujuzi wa uovu. Mungu alijua uovu ni kitu gani lakini hakujua uovu kwa kuwa hajawahi kuupitia. Shetani ndiye aliyekuwa

amejua mema na mabaya kwa uzoefu. Alikuwa akijionyesha kama Mungu kwa Hawa.

Tunaweza kulifananisha hili na mvulana anayesoma shule ambaye ameanza kuvuta sigara akimpatia rafiki yake sigara ambaye hajawahi kuvuta kamwe. Mvulana huyu anaonekana kuwa na uelewa zaidi kuhusiana na sigara kwa sababu ana ujuzi ambao mvulana mwingine hana. Lakini ujuzi wa uovu ndio unaopelekea kwenye kifo. Shetani alimwasilishia Hawa Mungu anayejua mambo yote mema na mabaya. Alimtambulisha Mungu kama anayejua yote.

Hili ni sawa na dai la Elihu. Kijana huyo alikasirishwa na wanaume wazee kushindwa kumsadikisha Ayubu kwamba maafa yake yamempata kwa sababu ya dhambi zake. Elihu anasema kwamba Mungu ni mkamilifu au anayejua kila jambo, wakati ni Elihu mwenyewe anayefikiri kwamba anajua kikamilifu njia za Mungu kuhusu dhambi na adhabu.

> Je! Wajua jinsi mawingu yalivyowekwa sawasawa, Hizo kazi za ajabu za huyo mkamilifu wa maarifa? Ayubu 37:16

Hata hivyo katika Zaburi tunaambiwa kwamba ufahamu wa Mungu ni mkubwa ambao hauwezi kuhesabiwa.

> Bwana wetu ni mkuu, na mwenye uweza; Ufahamu wake hauna mwisho. [H4557] Zaburi 147:5

Je, Mtunga Zaburi yuko sahihi? Je, ufahamu wa Mungu hauwezi kuhesabika au ni jinsi Elihu anavyoeleza kuwa kamili au ajuaye maarifa yote?

Elihu anamlaumu Ayubu kwa kunywa dharau kama maji, na kushirikiana na watenda maovu na kutembea na watu waovu (Ayubu 34:8). Dai hili ni la uongo kwa kuwa Mungu alikuwa amesema kwamba Ayubu alikuwa mnyofu, alimcha Mungu na aliepuka maovu, (Ayubu 1:1).

Ayubu anajaribiwa na shambulio ambalo Elihu alimfanyia. Lakini kama vile ambavyo Elihu hakuwa sahihi kuhusu tathmini yake kwa Ayubu, pia hakuwa sahihi kuhusu tathmini yake kwa Mungu. Elihu anaendelea:

Yeye huwavunja-vunja mashujaa pasina kuwachunguza, Na kuwaweka wengine mahali pao. Kwa sababu hiyo yeye huyatafiti matendo yao;

> Naye huwapindia usiku, wakaangamia. Yeye huwapiga kama watu wabaya Waziwazi mbele ya macho ya wengine; Ayubu 34:24-26

Anasema kwamba Mungu katika haki yake atawaponda na kuwapiga waovu. Kisha anatamani sana Mungu amjaribu Ayubu na kufichua uovu wake.

> Laiti Ayubu angejaribiwa hata mwisho, Kwa kuwa amejibu kama watu waovu. Ayubu 34:36

Yesu anatuambia kwamba Mungu hamhukumu mtu yeyote, (Yohana 5:22). Mtazamo wa Elihu kuhusu Mungu, kama walivyo watu wengi, si sahihi. Anamwasilisha Mungu katika nuru ya uongo. Anamwabudu Mungu anayejua yote. Mungu wa kweli anajua mwisho tangu mwanzo na hana ujuzi binafsi wa uovu kupitia kutenda maovu.

Hawa anashawishiwa na maneno ya Shetani kupitia nyoka. Anavutiwa kwamba nyoka inaonekana alipata nguvu ya kusema kwa kula tunda. Hawa alitazamia kwamba kula tunda hilo kungeleta adhabu ya haraka na ya papo hapo, hata hivyo nyoka hakuonekana kuwa ameumizwa kwa njia yoyote ile. Hili lilisaidia kumsadikisha Hawa kwamba kula tunda hakutaleta adhabu ya haraka na ya papo hapo na kumfanya atilie shaka ukweli wa neno la Mungu.

Ukweli kwamba Hawa amejitenga mbali na mumewe na kuwa karibu na Mti wa Maarifa ikimaanisha kwamba hisia zake za uadilifu zilipunguzwa. Udadisi wake na maswali ya ndani vilimvuta kuelekea upande wa Shetani kwenye mti. Uwepo wake ulikuwa ukitoa masafa ya kumchanganya na kumshawishi.

Biblia inasema mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, akatwaa matunda ya mti huo. Akiwa na tunda hilo mikononi mwake, Hawa hakuhisi usumbufu wowote au adhabu kwa njia yoyote ile. Kwa sababu alikuwa amesema kwamba kugusa tunda hilo kungeleteleza kifo, hilo lilimthibitishia zaidi kwamba hakuna jambo lolote baya ambalo lingempata kwa kula tunda hilo.

Kwa nini Mungu asiingilie kati na kukomesha hali hii? Kwa nini anaruhusu hili kujitokeza bila kuingilia kati? Baada ya kumpa Hawa maagizo yote muhimu ya kufanya uchaguzi, kuingilia na kumzuia kufanya kile alichotamani sio kumpa uhuru wa kuchagua. Kumruhusu mwanamke kufanya chaguo hili kulimsababishia Kristo mateso mabaya sana. Roho yake ilikuwa ikikaa moyoni mwake, lakini alipokula tunda, alikataa Roho wa Kristo na kukubali roho ya Shetani.

Hawa alikuwa akizungumza na pepo mchafu. Alipokula tunda hilo na kuamua kuunga mkono yale ambayo roho hiyo ilimwambia, aliruhusu roho hiyo kuongoza akili yake. Kwa hiyo, alipomkaribia Adamu, aliongozwa na pepo. Mbaya zaidi alikuja akiwa na ujumbe wa pepo mchafu aliyeahidi nguvu za kimiujiza kuwa kama Mungu, na kwa ufafanuzi huo unamfanya mama yetu wa kwanza kuwa mchawi.

Mwanamke aliporudi kutoka kwenye mti alikuwa chini ya mamlaka ya Shetani. Sasa anakuja kwa mume wake si kama mke mtiifu, bali kama mwalimu wa dini mpya. Adamu anaposimama mbele ya Hawa, tunaona kufananishwa kwa wanaume katika enzi zote ambao wamesimama mbele ya maneno ya kike, kama vile Delphi na wengine, ambao wamewaahidi ujuzi wa hatima yao ya wakati ujao. Adamu anapomtazama mkewe ambaye alikuwa mfupa wa mfupa wake, anakutana na roho ambayo haimtambui tena kama kichwa na mfadhili wake.

Alikuwa amepata mwenzi mwingine wa roho, mwalimu mwingine ambaye alimuahidi yote ambayo moyo wake ulikuwa unatamani bila kuhitaji kujisalimisha kwa mtu yeyote. Hakuja kufundishwa, bali kufundisha; si kutii, bali kuamuru kutiiwa. Roho hii ya kike, ambayo sasa inatawaliwa na nguvu za giza, itatumiwa kuwa chombo cha kushawishi cha Lusifa ili kumshawishi Adamu ajiunge na uasi. Hawa amevunja sura ya Mungu. Kwa kusukumwa na Shetani, amepoteza Roho wa Yesu ambaye ni mtiifu na anayefundishika. Hawa anakuwa na uthubutu zaidi, akiwa na hakika kwamba yale waliyokuwa wameelewa hapo awali hayakuwa sahihi. Kuna jambo la ajabu la kuvutia kuhusu mwanamke huyu anayejiamini ambaye analazimisha tunda mkononi mwa Adamu.

Adamu anatathmini hali; anaona amekula tunda. Maneno ambayo amemwambia kuhusu hukumu ya kifo kwa kosa yanagongana akilini

mwake. Ana hakika kwamba lazima afe na kwamba Mungu atamuua. Hisia ni mpya kwake na hana uhakika jinsi ya kuzishughulikia. Kuna haja ya kutoa lawama mahali fulani kwa hali hii mbaya. Kulichoinuka moyoni mwake ni uasi dhidi ya Mungu, ingawa yeye hajui jambo hilo. Shetani anavutiwa mara moja na masafa yanayotoka kwa Adamu. Mawazo yote ya shukrani kwa Mungu yamemezwa chini ya dhana potofu kwamba Mungu atamuua mke wake.

Mtazamo wa Adamu ni wa uongo lakini badala ya kupeleka mkanganyiko wake kwa Bwana na rafiki yake mpendwa, anaanza kufanya maamuzi peke yake. Roho wa Yesu anamwita Adamu akilini mwake. Roho anamsihi Adamu kupeleka suala hilo kwa Mwana wa Mungu au malaika, ili kujadili jambo hilo kabla ya kuruka hadi kwenye hitimisho. Lakini, hasira yake inakua, chuki ile ile iliyopo ndani ya Shetani inaanza kupata nafasi ya kuingia ndani ya moyo wa Adamu. Anafikiria maisha yangekuwaje bila Hawa. Hawezi kuvumilia. Shetani, akiwa ameambatana na Hawa, anamnong'onezea kwamba Mungu hakuwa na kusudio bora zaidi moyoni mwake na ingekuwa afadhali kujiunga na uasi huo.

Bustani nzima inasimama tuli Adamu anapoinua tunda mkononi mwake na kuliweka kinywani mwake. Baba na Mwana wanamsihi Adamu kwa wakati huo kufikiria upya, lakini anazuia sauti ya kusihi kama ilivyokuwa kwa ndugu zake Yusufu walizuia sauti yake ya kusihi walipomuuza utumwani. Adamu anakula tunda kwa hasira, huzuni na huku akiwa na uelewa kamili kwamba lilikuwa ni tendo la uasi.

Wakati huo, kuna majeraha makubwa ndani ya nafsi ya Mwana wa Mungu. Adamu amezamisha kisu cha kiroho cha uchungu na chuki ndani ya Roho ya Kristo iliyokuwa ndani yake na kumrarua Kristo kutoka kwenye kiti cha enzi cha akili yake. Kristo kwa wakati huu amechinjwa moyoni na akilini mwa Adamu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. (Ufunuo 13:8).

Mwana wa Mungu hawezi kuwaacha Adamu na Hawa kwa sababu akifanya hivyo, hakika wataanguka chini na kufa mara moja. Akiwa amebeba majeraha moyoni mwake, Kristo anawashikilia Adamu na Hawa na anaendelea kuwapa uzima hata wakati ambapo roho ya

Shetani inawatawala. Kristo lazima akae katikati ya adui zake ili kuwaweka hai wanadamu.

Ingawa uwezekano ulikuwapo kwa Adamu na Hawa kuanguka, Mungu hakuagiza kwamba jambo hilo litokee. Haikuwa mapenzi yake kwa Adamu kuchagua kuasi na kumpinga. Haikujulikana kwa hakika kama hili lingefanyika. Mara tu Adamu alipofanya dhambi na kumeza uzao wa nyoka, Mungu alijua kabisa mahali ambapo hili lingeelekea na nini kingetokea kwa jamii ya wanadamu, kwa maana alijua uzao uliokuwa ndani ya Shetani. Alikuwa ameweka wazi katika siku sita za uumbaji matokeo ya uzao wa nyoka dhidi ya uzao wa Mwanawe.

Swali kuu linalotuvutia ni hili: Mungu atafanya nini?

SURA YA 20

# NIA YA MWILI

Mabadiliko yaliyofanyika katika akili ya Adamu yalikuwa ni janga. Alikuwa ametia muhuri mawazo yake ya uongo juu ya Mungu katika tendo la kula tunda lililokatazwa. Sikiliza kile ambacho maneno ya uvuvio hukisema kuhusu hali ya kuanguka ya mwanadamu.

> Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Warumi 8:7

> Moyo huwa mdanganyifu kuliko *vitu* vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Yeremia 17:9

> Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa. Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya, wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema; ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao. Warumi 1:28-32

Sifa hizi zote sasa zilikaa ndani ya Adamu. Zilikuwa katika umbo la mbegu. Hakujua ukubwa wa mabadiliko ambayo yalikuwa yametokea ndani yake. Hakuwa na wazo lolote la misukumo

iliyokuwa ikiongezeka ndani yake, kama maji ya kilindi katika siku ya kwanza ya uumbaji.

Adamu alipokea nia ya Shetani na akaungana naye katika kumtupia Mungu sifa zote mbaya ambazo kiuhalisia zilikuwa zake[Adamu] mwenyewe. Adamu aliwazia kwamba Mungu alitaka kumuua mke wake na yeye mwenyewe kwa sababu ya kula tunda lililokatazwa. Alimwazia Mungu kuwa mwangamizi wa watoto wake mwenyewe. Aliwazia kwamba Mungu alidai kifo kwa uvunjaji wa sheria.

> Kwa maana dhambi, kwa kupata nafasi kwa ile amri, ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua. Warumi 7:11

Sheria ya Mungu ni takatifu kama yeye mwenyewe. Ni onyesho la tabia yake kamilifu. Kama vile ilivyo kwa Mungu, sheria ni takatifu, ya haki na njema.

> Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema. Warumi 7:12

Katika sheria tumefunuliwa ukweli kwamba Mungu ni mwenye huruma kwa wale wampendao na kuzishika amri zake kwa sababu kuzishika amri ni kujua tabia ya Mungu. Mungu huwezeshwa na imani ya mpokeaji katika rehema yake. Matendo yote ya Mungu huonekana kuwa ya uadui kwa wale wanaomchukia Mungu.

> …nikiwaonyesha rehema maelfu [ya vizazi], kwa wale wanipendao na kuzishika amri zangu. Kutoka 20:6

Kama tulivyojifunza katika sura ya 13, rehema za Mungu hudumu milele; hazina mwisho. Kwa hiyo, tunapoacha kumwamini Mungu wa kweli, rehema hukoma. Adamu alipochagua kuamini wazo la kwamba Mungu angemuua mke wake, alichagua kuvunja sheria ya tabia ya Mungu; alichagua kuamini kwamba Mungu hana huruma kwa wale wanaokosa kutii. Hii ndiyo sababu sheria iliyovunjwa ilidai kifo cha mvunja sheria na ni mvunja sheria anayefikia hatua ya kuliamini hili.

> Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo. Waebrania 9:22

Mstari huu ambao umenukuliwa hapa hauongelei nia ya Mungu bali nia ya mwanadamu aliyeanguka. Mungu kamwe hakutamani dhabihu kwa ajili ya dhambi.

> Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo, Masikio yangu umeyazibua, Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka. Zaburi 40:6

Hili ni gumu sana kwa mwenye dhambi kulielewa. Ulimwengu wa Kikristo karibu ulimwenguni pote unaamini kwamba Mungu anadai kifo cha mkosaji na kwamba ni dhabihu ya damu ya Mwanawe tu ingelipa fidia kwa ajili ya uasi wa mwanadamu dhidi yake. Je, itawezekanaje kwa Mungu kudai kifo na kutotamani dhabihu kwa wakati mmoja? Haiwezekani. Adamu aliamini uongo wa kwamba Mungu alidai kifo kwa ajili ya makosa yao na hii ndiyo sababu alikula tunda na kuasi.

Hivyo ndivyo ilivyo kwamba ili kumwokoa mwanadamu, Mungu alipaswa kulipa deni ambalo mwanadamu aliamini lilihitajika kulipwa ili kumkomboa. Adamu alikuwa amekataa imani katika rehema ya Mungu alipochagua kuamini kwamba Mungu alitaka kumuua mke wake. Kama angeamini rehema za Mwenyezi Mungu, angekwenda kwa Mungu na kuomba rehema. Lakini hakufanya hivi.

Katika akili ya wanadamu, sheria iliyovunjwa ilihitaji kifo, na kifo pekee ndicho kingetupatanisha na sheria. Hadi hili lilipotokea, tuliishi katika uhusiano wa kukata tamaa na Mungu. Mungu alikuwa tayari kufanya hivi kwa ajili yetu, akituwezesha kujisikia tena kupatanishwa na Mungu (ingawa Mungu alikuwa tayari daima kutupatanisha bila kifo, lakini tusingeamini). Kutokana na hatua hii ya kwanza Mungu angetufundisha kwa usahihi zaidi sheria yake na serikali yake, akionyesha kwa upole mawazo yetu potofu na hali yetu ya dhambi kwa kadiri ambavyo tungeendelea kukua katika neema na ufahamu wa tabia yake.

> Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Waebrania 2:14-15

Kimsingi Mungu anatutaka tuelewe hili: Msingi wa uvunjaji wa sheria ni kuamini kwamba Mungu anahitaji kuua mtu au kitu ili kuweza kusamehe. Hii ndiyo sababu pekee ambayo hupelekea sheria iliyovunjwa kudai kifo cha mvunja sheria.

Mwanadamu anapokataa ukweli wa tabia ya Mungu, katika nafasi ya Mungu anasimamisha sanamu ya mawazo yake mwenyewe; na mwanadamu anapoabudu sanamu, Mungu anakuwa Mungu mwenye wivu. Katika ibada yake ya sanamu mwanadamu hupita nje ya uzio wa ulinzi wa Mungu na Shetani anaweza kuanza kumsumbua, kumdhuru na hatimaye kumwangamiza. Kadiri mwanadamu anavyozidi kutanga mbali kutoka kwa Mungu mwenye rehema, ndivyo madhara yanayompata yanavyokuwa makubwa zaidi na ndivyo mtu huyo anavyoamini zaidi kwamba ni Mungu anayemletea adhabu hii. Lakini ni uovu unaoharibu waovu, si Mungu.

> **Uovu utamwua asiye haki**, Nao wamchukiao mwenye haki watahukumiwa. Zaburi 34:21

> BWANA amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; **Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake.** Zaburi 9:16

Biblia hutuambia kwamba hukumu ambayo Mungu hutoa dhidi ya waovu ni kuwaacha wanaswe katika kazi ya mikono yao wenyewe. Kwa sababu wanakataa urafiki wa Mungu wa kweli, waovu wanakufa chini ya imani ya uongo kwamba Mungu ndiye anayewaua.

Mungu angewezaje kufikia akili ya Adamu? Adamu alikuwa na hakika kabisa kwamba Mungu alitaka kumuua. Je, Mungu angewezaje kusema naye sasa alipokuwa chini ya utawala wa kifo? Hakukuwa na kitu kizuri kwa Adamu kumjibu Mungu. Hakukuwa na kitu ndani yake ambacho kilimtamani Mungu au hata kumtafuta.

> Kama Maandiko yanavyosema, "Hakuna aliye mwadilifu, hata mmoja. Hakuna aliye na hekima ya kweli; hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamekengeuka; wote wamekuwa bure.Hakuna atendaye mema, hata mmoja." Warumi 3:10-12 (NLT)

Baba na Mwana walihuzunishwa sana na matazamio ya wanadamu. Kama mtu yeyote anavyojua jinsi ilivyo kwa yule ambaye alikuwa ni rafiki yake anapogeuka dhidi yake, mara mtu anaposhawishika kuwa

mawazo yako kwake ni ya uovu na yenye madhara tu, hakuna chochote unachoweza kukisema ili kumshawishi vinginevyo. Joka lililokuwa limengoja tayari kumeza uzao wa kristo lilionekana kuwa limemshinda Mungu na Mwanawe. Shetani angeweza tu kufikiria kwamba Mungu angewaachia wanadamu awafanye vile apendavyo.

Lakini Mungu hakushtukizwa bila kuwa na cha kufanya. Alijua kwamba kulikuwa na uwezekano wa viumbe Wake kuchagua kuamini uongo juu Yake na kujifungia kwenye ngome ya kifo. Shetani alikuwa ameikataa tabia ya Mungu katika ufahamu kamili wa Mungu alikuwa nani. Adamu na Hawa walikuwa wameishi kwa miaka michache tu na ujuzi wao wa Mungu ulikuwa mdogo sana. Kulikuwa na nafasi ya ukombozi kwa jamii iliyoanguka.

Kwa kutuhurumia sana, Mwana wa Mungu alimwendea Baba ili kumwomba kwamba aweze kumpa ruhusa kutimiza kile kilichohitajika kwa ajili ya watoto Wao walioanguka.

SURA YA 21

# KUJIHATARISHA KWA UPENDO WA AGAPE

> Yeye ndiye atakayejenga hekalu la BWANA; naye atauchukua utukufu, na kuketi na kutawala juu ya kiti chake cha enzi; naye atakuwa kuhani katika kiti chake cha enzi, na **shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili**."—Zekaria 6:13 (KJV).

Baba na Mwana walifanya shauri la amani pamoja ili kujadili hatua ambazo wangechukua ili kuwakomboa wanadamu. Katika maombi ya Yesu katika Yohana 17 tunaona matunda yaliyodhihirishwa ya shauri hilo. Katika sala hii, yale yaliyofichika yanadhihirika.

Tunakumbushwa ukweli kwamba Kristo alipewa mamlaka kuhusiana na jamii ya wanadamu.

> …kama vile **ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili**, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele. Yohana 17:2

Mpango huo ulihusisha jamii ya wanadamu kupata kujua ukweli juu ya Baba kupitia Mwana pekee.

> Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3

Katika maombi yake duniani, Yesu aliweka wazi kutimizwa kwa mpango waliojadiliana wakati wa anguko la mwanadamu. Shetani alikuwa amejaribu kuficha ukweli kwamba Mwana wa Mungu alirithi

vitu vyote kutoka kwa Baba Yake ili kwamba yeye mwenyewe adai kwamba hakupokea chochote kutoka kwa Mwana wa Mungu.

> Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako. Yohana 17:7

Kiini kikuu katika maombi ni ufunuo wa tabia ya Baba, au jina, na kwamba Mwana wa Mungu kweli alitoka Kwake.

> **Jina lako nimewadhihirishia** watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika. **Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako**. Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, **wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako**, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nilipokuwapo pamoja nao, mimi naliwalinda kwa jina lako ulilonipa, nikawatunza; wala hapana mmojawapo wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu, ili andiko litimie. Yohana 17:6-8,12

> Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua; **lakini mimi nalikujua, na hao wamejua ya kuwa ndiwe uliyenituma. Nami naliwajulisha jina lako, tena nitawajulisha hilo**; ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao. Yohana 17:25-26

Katika maombi haya, Yesu alitangaza kwamba alikuwa amemaliza kazi ambayo Baba alimpa kuifanya. Kazi hii ilikuwa ni kufunua tabia ya Baba kupitia matendo yake, kuonyesha kwamba uwezo wa kutubu na kusamehewa ulitolewa bure kutoka mbinguni, na kutangaza asili ya uhusiano wao na jinsi inavyotegemeza uumbaji: kwamba Mwana wa Mungu alikuwa Mwana wake kweli, aliyezaliwa kutoka Kwake katika umilele na kisha kutumwa ulimwenguni kwetu.

> Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. Yohana 17:4

Lakini kulikuwa na zaidi ya kumaliza tu kazi ambayo Baba aliitamani. Ili kumaliza kazi, iliwabidi kulipa adhabu ya dhambi ambayo Shetani alikuwa ameitengeneza na kumshawishi mwanadamu kuiamini. Yohana sura ya 18 na 19 hufunua sehemu ya mpango wa kumwokoa mwanadamu kutoka katika imani yake kwamba Mungu alidai kifo na

kwamba ni dhabihu ya damu pekee ya aliye mbadala ingeweza kuwaokoa.

Kwa kadri ambavyo Mungu na Mwanawe walivyoweza kusoma mawazo ya Shetani, waliweza kutazamia kwa shauku wakati unaofafanuliwa katika Yohana 18 na 19; waliweza kumwona Mwana katika bustani ya Gethsemane akihisi hisia mbaya za hatia ambayo mwanadamu alijiletea kupitia wazo potofu kwamba Mungu alidai kifo cha mkosaji. Kitabu cha Mathayo kinaeleza wakati huu:

Ndipo akawaambia, Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa, mkeshe pamoja nami.

> Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe. Mathayo 26:38-39

Hatua zilizokuwa za lazima kumwokoa mwanadamu ziliwekwa wazi katika mfuatano wa sikukuu za Bwana unaopatikana katika Mambo ya Walawi 23. Maisha makamilifu yasiyotiwa chachu ya Kristo na kifo chake hufunuliwa katika sikukuu ya kwanza ya Pasaka. Kumwagwa kwa tabia yake ya kweli kupitia Roho Mtakatifu ni katika sikukuu ya pili ya Pentekoste. Mfuatano wa mwisho wa matukio unaoleta upatanisho kamili kati ya Mungu na mwanadamu unapatikana katika sikukuu za mwezi wa 7: Baragumu, Upatanisho, na Vibanda. Majira hayo ya kuburudisha yaliwakutanisha watu wa Mungu mara tatu kwa mwaka.

> **Mara tatu kila mwaka utaniwekea sikukuu**. Utaiweka sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu; utakula mikate isiyochachwa muda wa siku saba kama nilivyokuagiza, kwa wakati uliowekwa, mwezi wa Abibu (kwa maana ndio mwezi uliotoka Misri); wala hapana mtu atakayeonekana mbele yangu na mikono mitupu; tena, sikukuu ya mavuno, hayo malimbuko ya kazi zako za kupanda mashambani; tena, sikukuu ya kukusanya, mwisho wa mwaka, hapo utakapokusanya hayo uliyoyataabikia shambani. **Mara tatu katika mwaka watu waume wako wote watahudhuria mbele ya Bwana MUNGU.** Kutoka 23:14-17

Mikusanyiko hiyo mitatu ya watu wa Mungu ni udhihirisho wa mbegu iliyositawishwa katika shauri la amani. Mwana wa Mungu alikuja mbele ya Baba mara tatu ili kujadili vipengele mbalimbali vya mpango wa wokovu na utekelezaji wake. Kanuni hii pia imefunuliwa katika nyakati tatu ambazo Kristo aliomba katika bustani ya Gethsemane.

> Akaenda tena mara ya pili, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe. Akaja tena, akawakuta wamelala; maana macho yao yamekuwa mazito. Akawaacha tena, akaenda, **akaomba mara ya tatu**, akisema maneno yale yale. Mathayo 26:42-44

Idadi hii ya maombi si kwamba haina maana; ni ufunuo wa uzao wa Kristo ambao ulifanywa kikamilifu na kuelezewa katika Mwanzo 3:15 kama uzao wa mwanamke.

Kabla ya Mungu na Mwanawe kutekeleza mpango huu, matokeo halisi hayakujulikana kiukweli. Kipengele hiki kisichojulikana kilidhihirishwa katika maneno ya Yesu Msalabani.

> Yapata saa tatu Yesu akaita kwa sauti kuu, "Eli, Eli, lemasabakthani?" maana yake, "Mungu wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46 (NLT)

Ili Mwana wa Mungu achukue uzito wa hatia ya Adamu, alitakiwa kupiga hatua hadi mahali ambapo mwenye dhambi hangeweza kuona upendo na huruma ya Mungu. Kitu pekee ambacho angeweza kukiona katika wakati huo kilikuwa kifo. Haya ndiyo yaliyokuwa mawazoni mwa Adamu. Katika kuchukua asili yetu, Kristo angepitia haya kwa ajili yetu.

Je, imani ya Yesu inaweza kumshikilia Baba yake katika wakati huo wa giza kuu? Hapo mwanzo haikujulikana kwa uhakika. Mwana wa Mungu alionyesha kutokuwa na uhakika kulikozungumziwa katika shauri la amani katika sala hii: "Ee Baba, kikombe hiki kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe. (Mathayo 26:39).

Maelfu ya miaka kabla ya Msalaba wa Kalvari Walikuwa wamejadili wakati ambapo Yesu angehitajika kutengwa kutoka kwa Baba yake -

jinsi gani angehitajika kushikilia ukweli kwamba Baba yake alimpenda katika wakati ambapo hakuweza kulihisi hilo, bali kuhisi tu uhakika wa kifo cha milele. Hili lilikuwa jambo ambalo Yesu hakuwahi kulipitia katika uzoefu; Siku zote alikuwa ameunganishwa na Baba Yake; mawazo yake ya kuhisi kutengwa yalikuwa yakimsumbua sana.

Je, Mwana angeweza kushikilia imani kwa Baba yake? Katika shauri la amani, Baba alitetemeka kwa wazo kwamba angeweza kumpoteza Mwanawe milele. Hii inaelezwa katika Zaburi 18:

> Lakini katika shida yangu nalimlilia BWANA; naam, nilimwomba Mungu wangu anisaidie. Alinisikia kutoka patakatifu pake; kilio changu kwake kilifika masikioni mwake. Kisha nchi ikatikisika na kutetemeka. Misingi ya milima ikatikisika; walitetemeka kwa sababu ya hasira yake. Moshi ulitoka puani mwake; miali mikali iliruka kutoka kinywani Mwake. Makaa yanayowaka yalitoka Kwake. Zaburi 18:6-8 (NLT)

Neno hasira katika Kiebrania linaweza kubeba maana ya huzuni. Hapa panaonyeshwa roho iliyo katika huzuni kubwa na uchungu kwa wazo la kumpoteza Mwanawe milele. Hebu fikiria kwa muda shauri hilo la amani, Baba anapomtazama Mwanawe mpendwa na kufikiria madai ya kikatili ya mteka-nyara Shetani. Je, nimkabidhi Mwanangu wa pekee ili kuokoa wanadamu? Baba anapata maumivu makali sana katika nafsi yake anapoyafikiria haya. Anawezaje kumtoa Mwanawe wa thamani, aliye mfano wake halisi; Yule ambaye amemlea, ambaye amemfundisha kila kitu alichojua? Je! Anawezaje kumtoa mshirika Wake wa karibu zaidi, Yule pekee anayemwelewa katika ukweli wake wote? Tunamwona Baba akifunuliwa katika aya hii:

> Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza. Zekaria 12:10

Hatima nzima ya jamii ya wanadamu ilining'inia katika uwiano sawia. Sasa tunakuja kwenye mada kuu ya kitabu hiki. Upendo wa kweli

ulisambaa kote ili kuokoa jamii ya wanadamu. Baba anachagua njia ya kuwa na imani kwamba yote ambayo Amemfundisha Mwanawe na upendo kati yao ungeshikamana na haungeweza kugawanywa. Ilikuwa ni imani ya pekee sana.

Mwana mpole na mwenye upendo anamshika Baba yake kwa mkono, anamtazama machoni pake, na katika tabia ile ile ambayo Amefunzwa, anamwomba Baba yake ruhusa ya kuja na kutuokoa.

Je, unaweza kuelewa aina hii ya upendo? Siwezi kuandika maneno katika kutafakari upendo wa ukubwa huu. Mwana wa Mungu alikuwa tayari kupotea milele ili kutuokoa. Aliweka uzima Wake wa milele hatarini ili kutupatia nafasi ya kuishi. Hatujui ni upendo kiasi gani alionao Mungu na Mwanawe kwetu. Kujitolea kwao wote wawili walikokuonyesha hakueleweki. Hakika nimetekwa na kujitolea huku. Kunanifunika kwa hisia tamu za usafi wa upendo wao na kujitolea kutuokoa.

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16

Ni hatari ambayo Baba aliibeba kutuokoa ndiyo hutoa maana ya kauli KWA MAANA JINSI HII; MUNGU aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee. Moyo wa Baba ulilemewa na maumivu makali sana katika uwezekano kwamba angeweza kumpoteza Mwanawe lakini hakuziacha kanuni Zake za tabia. Hakujisalimisha chini ya kanuni za Shetani. Angeweza kujigeuza Mwenyewe, kama wanadamu wengi wanavyofanya watoto wao wanapotishwa, na kumwangamiza Shetani mara moja, lakini Shetani angetabasamu anapokufa akijua kwamba kanuni zake za maisha zingeishi milele na kwamba Mungu alikuwa ameshindwa na Lusifa.

> Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu; ndio maana ninyi hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo. Malaki 3:6

Baba hangebadilisha tabia yake ili kukabiliana na shida hii. Asingejihusisha na namna fulani ya ajabu “nje na tabia yake” ili kuuangamiza uasi kwa kutumia nguvu kwa ajili kulinda kile ambacho kilikuwa cha thamani zaidi Kwake.

Tunaona utulivu kamili wa nafsi katika bustani ya Gethsemane baada ya Kristo kumaliza maombi yake. Huu ni udhihirisho wa mbegu kutoka kwenye shauri la amani. Baada ya kukutana pamoja kila mara ili kuazimia kutekeleza mpango wa wokovu, mwishowe amani kamili ilijaa katika moyo wa Baba na kutokea kwake ilimwagika juu ya Mwanaye.

Roho hiyo ya utulivu huja kwa wale walio safi moyoni; inakuja kwa wale ambao hawatapunguza utimilifu wao. Uzoefu wa Sabato umejaa pumziko hili lenye baraka la ufahamu na kuamini katika makusudi na mapenzi yanayotoka kwa Baba. Mara tatu kwa mwaka tunaweza kuingia katika mkondo huo wa fahamu ambao hutoa kabisa, kutimiza na kuinua matamanio na fadhila bora zaidi za mwanadamu, kwamba hutoa hisia safi ya amani katika nafsi.

Ni hatari ya Baba na Mwana - hatari ya upendo wa Agape - ambao utakuwa mada ya waliokombolewa katika umilele. Upendo huu wa Baba hautasahaulika kamwe; itakuwa mada ya kila mkusanyiko.

> Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele. Ufunuo wa Yohana 5:13

SURA YA 22

# UDHAIFU WA MUNGU

Kama tulivyojadili hapo awali, Mwana mzaliwa wa Mungu ambaye alifundishwa kila kitu anakichojua anangamiza uwezekano wa maarifa kuwa kipimo cha uungu. Vivyo hivyo, ukweli kwamba Mwana wa Mungu alipokea nguvu zote kutoka kwa Baba Yake pia inamaanisha kwamba nguvu au uweza wote hauwezi kutumika kama kipimo cha uungu.

Ni kweli kwamba Mungu wa Biblia ana nguvu na hekima ya ajabu lakini mara tu akishawekwa huru kutoka kwenye ngome ya Utatu, vipengele hivi havitakiwi tena kama vipimo vya uungu.

Mojawapo ya hoja kuu za watu ulimwenguni dhidi ya Mungu ni kwamba ikiwa Yeye ana uwezo wote, basi kwa nini asikomeshe maumivu na mateso haya yote? Ikiwa ana uwezo wa kutatua matatizo yote ya ulimwengu, basi kwa nini anamfanya kila mtu aendelee kuteseka?

Kama tulivyozungumzia katika sura ya 8 kuhusu uhuru wa kuchagua, tunaona katika Mwana wa Mungu Mtu ambaye hana kizuizi kabisa. Hii ina maana kwamba Baba hatumii nguvu au shinikizo lolote kwake. Katika fundisho la Utatu, uhuru wa kuchagua unachukuliwa katika msingi wa kwamba nguvu za Mwana ni sawa na zile za Baba. Dhana ya msingi hapa ni kwamba Baba hawezi kulazimisha mapenzi ya Mwana kwa sababu Mwana ana nguvu sawa na Baba.

Wazo hili linaeleweka vyema duniani. Sababu ya kwamba nchi kama China haiishambulii nchi kama USA ni kwa sababu wote wana silaha za maangamizi makubwa. Ni kiwango cha juu cha nguvu

wanachomiliki wote wawili ambacho kinawazuia kushambuliana na kudai utawala wa ulimwengu wote.

Katika kielelezo cha kibiblia cha Mungu, Baba kamwe haonyeshi mamlaka au nguvu juu ya Mwanawe ingawa alimpa kila kitu alichonacho. Mungu angeweza kutumia nguvu juu ya Mwanawe, akiwa kwamba Baba ndiye kichwa cha Kristo, lakini anaamini kwamba Kristo atamtii kwa hiari Yake mwenyewe.

> Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Yohana 12:49 (NASB)

Yesu anafanya tu kile ambacho Baba yake anakisema si kwa sababu amelazimishwa, bali kwa sababu anaamini kile ambacho Baba yake anamwambia akifanye ni sahihi. Kristo kwa hiari hufanya mapenzi yake kuwa kitu kimoja na ya Baba yake, na kujisalimisha huku kwa upendo ndio ufunguo wa uzima wa milele ambao Kristo huwapa wote wanaokubali Roho wake. Uhuru wa mapenzi wa Mwana wa Mungu ndilo jiwe kuu la pembeni la serikali ya ulimwengu.

Uhusiano huu unatusaidia kuelewa jinsi ambavyo nguvu ya Mungu inaweza na haiwezi kutumika. Nguvu ya Mungu haitumiki kamwe kulazimisha mapenzi ya yeyote wa watoto Wake.

Ni jambo la kustaajabisha sana kuhusiana na wazo la uhuru wa kuchagua ambao Baba anampa Mwanawe hivi kwamba Paulo anamrejelea Mwana wa Mungu kama uweza wa Mungu.

> Lakini kwa wale walioitwa, Wayahudi kwa Wagiriki, **Kristo ni nguvu ya Mungu** na hekima ya Mungu. Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu; na **udhaifu wa Mungu una nguvu** zaidi **ya wanadamu.** 1 Wakorintho 1:24-25 (KJV)

Nguvu ya Mungu ni tabia yake. Tabia yake inadhihirishwa katika hiari anayowapa watoto wake. Ni ufunuo mzuri sana wa tabia ya Mungu. Nguvu hii huonekana kwa ulimwengu kama udhaifu. Paulo anasema hiki kinachodhaniwa kuwa udhaifu kina nguvu zaidi kuliko wanadamu.

> Akawaambia, "Wafalme wa Mataifa huwatawala, na wenye mamlaka juu yao huitwa Wenye fadhili; lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye." Luka 22:25-26

Usiku wa kabla ya kifo cha Yesu, aliwaambia wanafunzi wake kwamba katika ufalme wake hakuna matumizi ya mamlaka ya nguvu lakini badala yake aliye mkubwa ni yule anayetumikia. Wanadamu hutamani kutumia mamlaka juu ya wengine kwa sababu tamaa hii inatoka kwa Shetani.

> Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Isaya 14:13

Shetani alisema atakiinua kiti chake cha enzi juu ya nyota au malaika wa Mungu. Angewalazimisha kujisalimisha kwake pale inapobidi. Kama tulivyozungumzia katika sura ya 12 kuhusu kisa cha Danieli na tundu la simba, tunaona kwamba wale waliokuwa chini ya Danieli walipanga ibada kwa kutumia amri ya kifo. Ikiwa huabudu, basi utakufa. Hili ni zoezi la kutawala kimabavu. Ni matumizi ya nguvu kulazimisha watu kumtumikia mfalme.

Baba yetu aliye mbinguni hamlazimishi mtu yeyote kumtumikia. Hatumii mabavu juu yetu, lakini badala yake anatutumikia na kutujali, kama baba anayejali awezavyo kufanya. Ni katika Mwana mzaliwa wa Mungu pekee ndipo tunaweza kuanza kufahamu muundo wa kweli wa nguvu za Mungu. Mwana wa kweli wa Mungu anamwita Baba yake Mungu wake.

> Yesu akamwambia. Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, **kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu**. Yohana 20:17

Yesu anamwabudu Baba yake kama Mungu wake, Mungu wa pekee wa kweli. (Yohana 17:3). Katika ibada hii ya Baba yake, hakuna nguvu inayotumiwa na Baba kumfanya aabudu. Hakuna tishio la adhabu bali uhuru na upendo tu. Sharti pekee ni Mwana kukiri kwamba yote aliyo

nayo yanatoka kwa Baba na hili linasababisha upendo kuchipuka kutoka moyoni mwake kwa ajili ya Baba yake.

Uhuru wa mapenzi wa Mwana wa Mungu unafika kwetu kupitia Kristo.

> Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli. Yohana 8:36

Uhuru wa Mwana wa Mungu ndio uhuru wetu. Tunapofahamu kwamba Baba hamlazimishi au kumtishia Mwanawe, tunaweza kuja kwa Baba kupitia uelewa huu na kujua kwamba hatatumia nguvu juu yetu ili kutulazimisha kumfuata.

Mtume Yohana aliandika katika waraka wake wa kwanza kwamba "Hakuna woga katika upendo…hofu inahusisha mateso. (1 Yohana 4:18). Neno mateso lina maana ya "adhabu." Hakuna hofu ndani ya moyo wa Mwana wa Mungu kwamba Baba yake atatumia nguvu juu yake kama adhabu kwa kukosa utii. Hiki ni kipengele muhimu cha Mwana kutozuiliwa. Hakuna hofu ya adhabu. Tunapoukubali ukweli huu ndipo hofu yetu itakapokoma.

Kutokuwa tayari kwetu kumfuata Mungu jinsi Kristo anavyomfuata Mungu ndiyo sababu wanadamu wanaendelea kuteseka na taabu za ulimwengu huu. Njia pekee ambayo Mungu anaweza kukomesha mateso ni kupitia kutufanya kumfuata na kutubidisha kutii sheria. Baba yetu hawezi kukomesha mateso kwa sababu hatatulazimisha kubadilika. Atatusihi na kutuonyesha matatizo ya njia tunayoitembea, lakini hatatulazimisha. Utambuzi huu huangamiza uelewa wa uongo wa mwanadamu wa uweza wa Mungu wa kujua yote ambao hutumiwa kumwonyesha Yeye kama katili na asiye na hisia kuhusiana na haya mateso.

Yeyote aliye na watoto wanaochagua njia mbaya na kujiletea matatizo anajua kwamba huwezi kuwalazimisha watoto wako kubadilika. Ikiwa utatumia nguvu, wataenda mbali zaidi au kukuchukia kwa kuzuia uhuru wao.

Njia mbadala kando na ya kulazimisha ni kutembea na mtoto wako anayeteseka na kujaribu kumsaidia kuona Nuru. Kutembea na watoto wako huku wanajidhuru ni huzuni kwa mzazi. Kwa kawaida, kadiri

watoto wanavyodanganywa zaidi katika njia zao, ndivyo wanavyokuwa na uwezekano mkubwa wa kuwalaumu wazazi wao au watu wengine wenye mamlaka yanayohusiana matatizo yao. Hivi ndivyo hasa ubinadamu umemfanyia Mungu.

SURA YA 23

# KUMJERUHI BABA

Fundisho la Kikristo la uweza wa Mungu wa kujua yote, likiunganishwa na mfumo wa haki unaodai kifo cha mkosaji, hupofusha roho kuhusiana na mateso ya kweli ya Baba.

Kristo anatuambia waziwazi:

> Yeye aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wawezaje kusema, Utuonyeshe Baba? Yohana 14:9

> Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Yohana 5:19

Katika muktadha huu, mateso ya Kristo katika bustani ya Gethsemane, kupigwa kwa Yesu katika jaribu lake, kuanguka kwa Yesu chini ya Msalaba kwenye njia ya Golgotha, na kifo chake juu ya Msalaba siyo kwa ajili ya kukidhi haki ya Baba, badala yake ni ufunuo wa mateso ya Baba yanayotokana na ubinadamu ambao umemkataa kwa chuki.

Uadui wa asili ulioko ndani ya mwanadamu (Warumi 8:7) dhidi ya Mungu huuchukulia Msalaba kwa namna ya kumwasilisha Mungu kama anayehitaji bei yake kwa ajili ya dhambi zetu. Ikiwa tungeruhusiwa kuona ukweli kamili - kwamba ukahaba wetu umeurarua moyo wa Baba yetu na kumfanya azimie chini ya uzito wa upotovu wetu - hatia yetu isingevumilika kabisa bila neema inayodumisha. Ndio maana ubinadamu hujipofusha kwa makusudi kabisa ili usitazame ukweli huu:

> Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza. Zekaria 12:10

Anayezungumza katika mstari huu ni Mungu. Inahitajika neema ya pekee kuweza kutambua kwamba tumemjeruhi kwa dhambi zetu.

Baba anapotazama kukataliwa kwa Mwanawe na kukataliwa kwake Mwenyewe, kama Baba wa kweli, Yeye hubeba huzuni inayomjeruhi sana. Kwa maana Yesu alisema kwamba kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu. (Mathayo 24:37). Ulimwengu utakwisha pale utakapomkataa Mungu kabisa.

> BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. Mwanzo 6:6

Je, tunaweza kumwona Baba akijeruhiwa katika mstari huu? Amelemewa na huzuni ya kutisha kwa kupotelewa na watoto wake ambao anawapenda sana. Tunaona dhiki ya Baba wakati Israeli ilipokaribia kuchukuliwa utumwani na Babeli. Baba anakumbuka uchungu Wake kwa kulazimika kuiachilia miji iliyokaa kando kando ya Sodoma na Gomora.

> Niwezeje kukuacha, Efraimu? Niwezeje kukuponya, Israeli? Niwezeje kukufanya kama Adma? Niwezeje kukuweka kama Seboimu? Moyo wangu umegeuka ndani yangu, huruma zangu zimewaka pamoja. Hosea 11:8

Moyo wa Baba unamdunda ndani Yake. Huzuni yake inamlemea. Anachomwa moyo kwa ajili ya kupoteza watoto Wake. Tunapozingatia jinsi Yesu alivyotendewa katika matukio ya Msalaba, lazima tuzingatie kwamba hili pia lilikusudiwa na Yule aliyemtuma.

> Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea huyo. Yohana 5:43

Matendo yaliyofanywa kwa Yesu katika mwili yalifanywa kwa Baba katika Roho. Ikiwa shomoro hawezi kuanguka chini bila Baba yetu kuhisi anguko lake, basi anahisi nini Mwanawe anapodhihakiwa, kupigwa, na kuuawa?

Ndipo askari wa liwali wakamchukua Yesu ndani ya Praitorio,

wakamkusanyikia kikosi kizima. Wakamvua nguo, wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! Kisha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi, wakampiga-piga kichwani.

> Walipokwisha kumdhihaki, wakalivua lile vazi, wakamvika mavazi yake, wakamchukua kumsulibisha. Mathayo 27:27-31

Kadri mambo haya yalivyofanyika kwa Mwana wa Mungu, ndivyo yalivyofanyika kwa Baba. Tunakumbushwa kwamba ikiwa tumemwona Kristo, tumemwona Baba. Kosa la kibinadamu la kufikiria uweza mkuu wa Mungu wa kuweza yote kwa njia inayomfanya asiguswe huuficha ukweli wa kwamba wanadamu walikuwa wakiuvunja moyo wa Baba. Uchungu huu wa Baba ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba dunia ilifunikwa na giza Baba alipolia.

> Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa. Mathayo 27:45

Giza liliakisi tabia ya Shetani kuushika ulimwengu wakati huo ubinadamu ulipodhihirisha chuki yake kwa Mungu na Mwanawe. Muda kidogo kabla ya kifo cha Kristo, tunaona Yesu alikuwa amepanda mwana-punda akilia juu ya Yerusalemu.

> Alipofika karibu aliuona mji, akaulilia, akisema, Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Lakini sasa yamefichwa machoni pako. Luka 19:41-42

Je, tunaweza kuona maneno ya Yesu kwa Filipo yakitumika hapa? Yeye aliyeniona mimi, amemwona Baba. Je, tunamwona Baba aliyevunjika moyo akiwalilia watu wake?

> Nami nitawaficha uso wangu kwa kweli siku hiyo, kwa maovu yote waliyoyafanya, kwa kuigeukia hiyo miungu mingine. Kumbukumbu la Torati 31:18

Unapoondoa mawazo yaliyoundwa kwa uongo ya kujua yote na kuweza yote, unaweza kuanza kuuona ukweli wa Baba anayeteswa na dhambi za watoto Wake waasi. Unaweza kuuona ukidhihirishwa katika Kristo na kukataliwa kwake na ulimwengu.

Na tumtazame Baba yetu tuliyemchoma na kumlilia kwa namna alivyomlilia mwanawe wa kwanza na kwa ajili yetu. Na hatimaye tuwajibike kwa matendo yetu na tuone kwamba tunawajibika kumsababishia Baba huzuni mbaya sana.

Ndipo tupate faraja kubwa katika ukweli kwamba Yeye hatuhukumu bali anatusamehe kwa yale tuliyomtendea Yeye na Mwanawe. Ukweli wa msamaha na upendo wa Mungu utaanza kuzama polepole ndani ya nafsi zetu tunapotambua kile ambacho Mungu ametufanyia.

SURA YA 24

# TOKENI GIZANI

Utukufu wa upendo wa Mungu kama unavyodhihirishwa katika Mwanawe una nguvu ya mvuto kiasi kwamba, unapoonekana katika usafi wake, unaweza kuwavuta watu wote kwa Kristo.

> Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. Yohana 12:32 (KJV)

Shetani ilimbidi kuficha mwangaza wa upendo huu vinginevyo angepoteza udhibiti wake juu ya ubinadamu, na kumfanya ajisikie asiye na nguvu na mnyonge asioweza kuustahimili. Shetani alikuwa ametumia faida ya Hawa kuongeza maneno katika agizo la Mungu kuhusiana na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Tena na tena, Shetani angetumia mbinu ya kuinua wazo fulani - linaloonekana kuwa lenye maana lakini kwa kweli ni lenye kudhoofisha - kuwashinda wanadamu. Katika mafundisho ya Kikristo, Shetani anaonekana kumwinua Mwana wa Mungu kuwa 'Mungu Mwana', kuwa ambaye hajawahi kufundishwa chochote wala kupokea chochote. Hili huonekana kama Kristo ameinuliwa na kuheshimiwa zaidi kuliko Kristo aliyetoka kwa Baba na kisha kupokea vitu vyote.

Shetani anachanganya dhana hii na kanuni ya haki iliyounganishwa na uweza wa nguvu unaodai kifo kwa ajili ya ukuu Wake uliotukanwa. Mfumo huu unaficha nguvu ya kweli ya Msalaba wa Kristo. Ni muujiza kwamba Msalaba bado una nguvu ya kuwavuta wanadamu wakati umejaa mawazo haya ya uongo.

Shetani ametumia chombo hiki cha kuinua kuhusiana na maarifa ya Mungu. Ikiwa angeweza kuwashawishi wale waliomwamini Mungu

kwamba Mungu anajua kila kitu - kwamba Alijua kwamba mwanadamu angeanguka na alijua kwamba Kristo angefaulu katika utume Wake - basi Shetani angeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa athari ya zawadi ambayo Mungu aliitoa katika Mwanawe na ingepoteza nguvu zake kwa watu wengi.

Ikiwa Mungu alijua kwa hakika kwamba Mwanawe angefaulu katika utume Wake, basi Mungu hakutoa chochote. Ukweli wa upendo wa Agape ni kutoa kikamilifu na kabisa bila uhakika kwamba kile unachotaka kitatokea. Wengi wetu tunajua madhara ya udanganyifu kwa mtu. Ghafla unamwagiwa zawadi na sifa, lakini kuna mtego: mtoaji anatoa ili kupata kitu kutoka kwako ambacho kinahitaji usalimishe uhuru wako kwa kiwango fulani.

Upendo wa Agape unaweza tu kujidhihirisha katika mfumo wa kujihatarisha. Mungu ajuaye yote, mdhibiti wa wote, na mwenye kuangamiza hawezi kudhihirisha upendo wa kweli.

> Katika pendo[Agape] hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. 1 Yohana 4:18

Katika muktadha huu, ulimwengu haujapata kuonyeshwa upendo wa kweli wa Mungu. Popote alipo mungu anayejua kila kitu, anayedhibiti kila kitu, na kisha kuhukumu-kulaani-kuangamiza, kuna hofu, mateso na uasi. Upendo wa kujitolea usio na masharti wa Agape unaharibiwa, kwa sababu hakuwezi kuwa na kujitolea wakati kila kitu kinajulikana, na upendo unakuwa na masharti pale watu wenye maisha ya asili wanapoangamizwa moja kwa moja na mtunga sheria (badala ya kuangamia kwa sababu ya kujitenga kutoka kwenye chanzo cha uzima). Hii ndiyo sababu ya kwa nini watu wote sasa hawavutwi kwa Mwana wa Mungu. Ndiyo maana watu wengi duniani wanatafuta faraja katika dini nyingine au hawana dini kabisa.

Upendo wa Agape ukiwa katika hali yake safi kabisa unahusisha kujihatarisha, kwa sababu Mungu anapompa mtu uhuru wa kuchagua Yeye hujihatarisha katika kumpa uhuru wa kuchagua. Mungu alifanya hivi akijua kwamba viumbe vilivyoumbwa vinapochagua mapenzi yao wenyewe badala ya mapenzi yake, ingemuumiza. Mungu alikuwa tayari kuteseka ili kudumisha upendo wa Agape.

Kabla ya Adamu kufanya dhambi na kabla ya mwanzo wa dhambi mbinguni, Mungu hakuwa na uelewa wa uhakika wa kuanguka kwa mwanadamu. Alikuwa na ufahamu wa uwezekano wake. Mara tu mwanadamu alipofanya dhambi, alijua kile ambacho uzao wa nyoka ungekizaa na kwa hivyo angeweza kutabiri matukio miaka mingi katika siku zijazo.

Inasikitisha kama nini kwamba Shetani ameyaathiri mafundisho ya Ukristo kwa dhana isiyo ya kibiblia ya Mungu mwenye nguvu ambaye anajua kila kitu kabisa. Hili limeuondoa moyo kutoka kwenye upendo wa Agape na kuuficha nyuma ya wingu jeusi.

Ingia katika nuru ya ukweli wa Biblia na upate tena uhuru wako wa kuchagua ambao Baba yako wa mbinguni amekupatia.

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu.

Upendo huo ulikuwa mkubwa sana
Hata akahatarisha hazina yake aliyoipenda sana,
Mwana wake wa pekee
ili kutuokoa.

FATHER
OF LOVE
fatheroflove.info